ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri waMiundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake

29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

51.Mhe. Kazija Khamis Kona Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid Jimbo la Kiembesamaki

55.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili - Tarehe 10 Oktoba, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

TAARIFA YA KUWA WAZI KWA KITI CHA UWAKILISHI CHA JIMBO LA KIEMBE SAMAKI

(Kwa mujibu wa Kifungu 71 (2) cha Katiba ya Zanzibar 1984 na Kanuni ya 27 (1) c ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi 2012)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe**,** nikuombeni radhi sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba taarifa hii nilikuwa niitoe jana lakini kwa kuwa tulikuwa safarini tulipitikiwa ikawa taarifa hii hatukuwahi kuitia katika *order paper* ya jana. Kwa hivyo, nikuombeni radhi sana kwa hilo kwa sababu ya kucheleweshwa kwa siku moja taarifa hii hasa kiutaratibu ilikuwa itolewe jana.

Waheshijmiwa Wajumbe, taarifa hii tunaitoa kwa mujibu wa Kifungu cha 71(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 27 (1) (c) cha Kanuni hizo za Baraza la Wawakilishi za mwaka 2012.

Waheshimiwa Wajumbe, ninapenda kukupeni taarifa kuwa siku ya tarehe 3 Septemba, 2013 Ofisi yangu ilipokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ikinijuilisha maamuzi ya Chama hicho ya kumfukuza uanachama Ndugu Mansour Yussuf Himid, maamuzi ambayo yalifanyika tarehe 26/8/2013 kwa mujibu wa maamrisho ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe, katika kutekeleza wajibu wangu chini ya Kifungu cha 71 (2) cha Katiba ya Zanzibar 1984 Toleo la 2010 na chini ya Kanuni ya 27 (1) (c) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2012), napenda kutoa taarifa kuwa kutokana na maamuzi ya Chama, kiti cha Mjumbe Mwakilishi Mhe. Mansour Yussuf Himid wa Jimbo la Kiemba Samaki, kimekuwa kipo wazi kuanzia tarehe 26/8/2013 kwa mujibu wa Kifungu cha 71 (1) (a) na Kifungu cha 69 (1) (c) vya Katiba ya Zanzibar 1984 (Toleo la 2010).

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuwapa taarifa pia kwamba baada ya kupata barua hiyo na kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 71 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, mnamo tarehe 6 Septemba, 2013 nilipeleka taarifa rasmi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuwa kiti cha Uwakilishi cha Jimbo la Kiembe Samaki kipo wazi kwa mujibu wa Katiba.

Waheshimiwa Wajumbe ninapenda kutoa taarifa hiyo kwenu na ahsanteni kwa kupokea taarifa hiyo.

Naomba kuwasilisha.

Hiyo Waheshimiwa Wajumbe ndio taarifa ambayo Katiba ilikuwa inanitaka nitoe kwenu mara baada ya kuingia katika Mkutano wa kazi za Baraza la Wawakilishi jambo ambalo nimeomba radhi mapema kwamba jana hatukuwahi kutoa taarifa hiyo. Naomba muipokee hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hati ya Hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Mambo Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati wa Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Mambo Yanayohusiana nayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 10

Kufuatiliwa na Kutekelezwa Ahadi za Viongozi Wakuu

Mhe. Bikame Yussuf Hamad (Nafasi za Wanawake) -Aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali kazi yake moja ni kuendeleza, kuzikusanya na kufuatilia ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa kwa kushirikiana na Ofisi za Mikoa, Wilaya pamoja na taasisi nyengine.

(a) Je, ni ahadi ngapi ambazo Idara yako imefuatilia pamoja na kuzitekeleza na Mkoa gani na Wilaya gani kwa Pemba na Viongozi gani ambao waliweka ahadi hizo?

(b) Je, ahadi ngapi za viongozi wa awamu ya sita zimefuatiliwa na kutekelezwa mpaka sasa?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa raisi, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake nambari 10 nitangulize maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina jukumu la kuratibu ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kusiwasilisha kwenye Taasisi husika kwa utekelezaji na si jukumu la Idara kutekeleza ahadi hizo.

Mhe. Spika**,** baada ya ufafanuzi huo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake nambari 10 lenye vifungu a naba kama ifutavyo:-

a) Mhe. Spika**,** kwa upande wa Pemba katika kipindi cha Jaunari - Machi 2013, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imefuatilia jumla ya ahadi 17, kati ya hizo ahadi 12 zimeshatekelezwa na ahadi 5 zinaendelea kufuatiliwa. Viongozi waliotoa ahadi hizo ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Jumla ya ahadi zilzotolewa ni hizi zifuatazo:-

WILAYA	**MKOA**	**AHADI**
Wilaya ya Mkoani	Kusini Pemba	12
Wilaya ya Wete	Kaskazini Pemba	2
Wilaya ya Micheweni	Kaskazini Pemba	1
Wilaya ya Chake Chake	Kusini Pemba	2
JUMLA		**17**

b) Mhe. Spika, Wizara yangu mpaka sasa imefuatilia jumla ya ahadi 20 zilizotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa awamu ya sita, ahadi kumi na nne kati ya ahadi hizo tayari zimeshatekelezwa na ahadi sita zinaendelea kufuatiliwa kwa madhumuni ya kuzitekeleza.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, ninashukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana lakini naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Spika, miongoni mwa viongozi wakuu wa kitaifa wa awamu ya sita aliyekuwa Waziri Kiongozi Mhe. Shamsi Vuai Nahodha pia ninajua kama ni miongoni mwa viongozi wakuu kitaifa, kama itakuwa sivyo naomba nisahihishwe. Lakini mheshimiwa huyu tarehe 12/7/2008 alikwenda kwenye bonde la Mtunga la Ole kichwa. Bonde hilo linaitwa mwanzo mgumu. Katika bonde hilo akatoa ahadi ya kuwapelekea wananchi hao umeme, maji lakini kubwa zaidi ni kuwajengea bwawa katika bonde lao hilo. Sasa jee, Mhe. Waziri ahadi hii pia unaifahamu na kama huifahamu ni lini ahadi hii iliotolewa na kiongozi huyo itafuatiliwa na idara yako na pia kutekelezwa?

Pili, kwa kuwa viongozi wetu wamekuwa wakitoa ahadi ambazo nyengine hatimaye hazitekelezwi. Jee, Mhe. Waziri kufanya hivi si kwenda kinyume na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi?(Makofi).

Mhe. Spika: Waheshimiwa tunataka tusikilize majibu muafaka sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, ninapenda tumtambue rasmi kwamba Mhe. Shamsi Vuai Nahodha ni mmoja kati ya viongozi wa kitaifa kwa kuwa alikuwa ni Waziri Kiongozi wa Zanzibar na kwa kuwa hata unapostaafu nafasi hiyo bado heshima yako kwa mujibu wa sheria zetu inaendelea kuhifadhiwa na kulindwa. Kwa msingi huo ni mmoja kati ya viongozi wetu wa kitaifa.

Mhe. Spika, kuhusu ahadi ya Ole Kichwa aliyotoa Mhe. Shamsi kuhusu maji na umeme. Ninazo orodha zilizotolewa na Mhe. Shamsi lakini katika kabrasha langu hapa halioneshi ahadi hiyo. Kwa hivyo nitachukua jukumu Mhe. Spika, kufuatilia zaidi na wahusika hasa kuwasiliana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, niweze kupata taarifa zaidi juu ya jambo hili lakini pamoja na kuwasiliana na wasaidizi wake Mhe. Shamsi ili tuhakikishe kwamba ahadi hiyo kama ilitolewa iweze kutekelezwa. Hapana shaka yoyote Mhe. Bikame Yussuf Hamad anafuatilia kwa umakini mambo yake, nina hakika kabisa kuwa itakuwa ni ahadi lakini kama binadamu itakuwa pengine kwa upande wetu tumepitikiwa.
Lakini tutafanya kila jitihada kuwafuatilia wahusika ili tuweze kuona utekelezaji wake unatekelezwa.

b) Mhe. Spika, kwamba kutokutelezwa kwa ahadi hatuoni kwamba tumekwenda kinyume na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, kwanza ninataka nimuhakikishie kwamba ahadi zinazotolewa na viongozi wetu wa kitaifa zinaendelea kutekelezwa na zote zitakamilishwa awamu kwa awamu na ikumbukwe kwamba viongozi wetu wa kitaifa watakapotoa ahadi hata kama hakumalizia ahadi ile wakati wa awamu yake, basi viongozi wanaofuata wanatekeleza ahadi hizo. Ndio maana serikali imefuatilia ahadi nyingi za Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na tunayo *list* yao na zile ahadi zote zinaendelea kutekelezwa.

Kutokukamilika kwa ahadi hakusababishi kwenda kinyume na ilani ya Chama cha Mapinduzi bali ni utaratibu tu wa utekelezaji wa ahadi hizo. Na bado tuipongeze au tukipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kuweka ilani nzuri inayotekelezeka na ambayo kwa miaka yote imewezesha chama hiki kushinda uchaguzi kutokana na kukubalika vizuri na wananchi wake. Kwa hivyo, tuendelee kupongeza na tushukuru kwa kazi nzuri inayofanya Chama cha Mapinduzi, Mhe.Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kuna kauli ya kiongozi wa juu kuliko Rais katika nchi hii, leo miaka miwili wananchi wa Jimbo la Muyuni wamepewa ruhusa ya kuajiri daktari mpaka leo hapana kilichofanyika.

Mhe. Haji Omar Kheir kashasaini barua hiyo lakini imekwama Wizara ya Afya. Hebu unawaambia nini wananchi wa Jimbo la Muyuni ambao mimi ndio walioniajiri, walionipa kibarua hiki kuja kuwatetea, leo ni miaka miwili ni barua tu hiyo! Jee, inaandikwa hati moja moja mpaka leo haijesha kuandikwa barua hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mhe. Jaku Hashim Ayoub kutokana na umahiri, umakini wake wa kufuatilia shughuli mbali mbali za maendeleo ya wananchi na hususan katika sekta hii ya afya, na umahiri huo hapana shaka umempa umaarufu mkubwa kwenye jimbo lake. Ninataka nimuhakikishie tu kwamba jambo hili linashughulikiwa na kwa sababu serikali ina imani kubwa sana na wananchi wake na inapenda kuona afya za wananchi wake zinanawirika. Kwa hivyo itafanywa kila jitihada kuhakikisha kwamba daktari anapatikana katika Jimbo la Muyuni kama ilivyoahidiwa na viongozi mbali mbali katika utekelezaji huo.

Kwa hivyo ninamuhakikishia tutawasiliana na Wizara husika ili tuhakikishe kwamba daktari anapatikana na hali ya wananchi iendelee kuimarika katika Jimbo la Muyuni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri suali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, wakati Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Ali Moh'd Shein alipokuwa akiomba ridhaa za wananchi basi alikwenda Micheweni na akaweka ahadi pindi atakapofanikiwa Urais basi *inshallah* barabara za Micheweni ambazo ni Shumbamjini-Micheweni, Mjiniwingi-Micheweni, Maziwang'ombe-Micheweni, Kiuyu-Micheweni zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Sasa kwanza ninamuuliza Mhe. Waziri ahadi zile anapoziweka Mhe. Rais kama mgombea nani anaziratibu. Jee, kwanza unazo ahadi hizi kwanza.

La pili, kama anazo ni lini barabara zile zitajengwa kwa sababu haionekani hata dalili ya zitajengwa barabara hizo na kama hana, basi aendelee kutafuta kumbukumbu kwa sababu aliweka ahadi na wananchi kila leo wananikumbusha kama Rais wa Zanzibar aliweka ahadi kuzijenga barabara hizi kwa kiwango cha lami, basi ni lini zitajengwa barabara hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ninataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kila ahadi ambayo Mhe. Rais wetu alipokuwa mgombea ameitoa itatekelezwa kama alivyoahidi.

Ninataka nimuhakikishie kwamba Rais wetu anafuatilia kwa umakini ahadi zake zote zile ambazo amezitoa na ameanza kuzitekeleza awamu kwa awamu kutokana na hali halisi ya uchumi. Sina taarifa kamili kuhusu ahadi hizi ambazo Mhe. Mwakilishi anaeleza katika Wilaya ya Micheweni, lakini ninataka nimuhakikishie kwamba nitafuatilia kwa wasaidizi wa Mhe. Rais na kukukumbushia ili kujua kama kuna ahadi hizi ili kumueleza.

Ninaamini Mhe. Mwakilishi anapoleta taarifa hii inakuwa ni sahihi, kwa hivyo tunazipokea tuziwasilishe kunakohusika ili zifanyiwe kazi. Lakini nataka nimuhakikishie tu kwamba Rais wetu ahadi zake atazitekeleza hatua kwa hatua, nia ni hiyo na ninamuhakikishia Mwenyezi Mungu akituweka hai mambo yataonekana. Ahsante sana.

Nam. 44

Uwekaji TAA kwenye maeneo ya Makutano ya Barabara

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Jimbo la Mtambwe) - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa moja ya wajibu wa Wizara hii ni kuona kuwa kuna usalama wa kutosha katika usafiri wa barabarani kwa vile nchi hii hivi sasa na hasa mjini imezidiwa na vyombo vya moto na usafiri (magari, mapikipiki, vespa, wapanda baiskeli, magari ya punda nk). Kutokuweko kwa taa za kuongozea magari katika sehemu za makutano ya barabara ni sababu moja wapo inayosababisha ajali za barabarani.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokuwepo kwa taa hizo kwa muda mrefu hapa Zanzibar na kusababisha madereva kutumia akili zao tu katika maeneo hayo?

(b) Wizara haioni kuwa kutokuwepo kwa taa hizo kunahatarisha usalama barabarani na pia kushusha hadhi ya mji wetu?

(c) Ni sababu zipi hasa ikafika wakati madereva wanatumia akili yao tu jambo ambao haliendani na suala zima la usalama barabarani na sheria za usafiri za Kitaifa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Ni kweli moja ya jukumu la msingi la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kujenga na kutunza barabara ikiwa ni pamoja na matumizi salama ya barabara hizo.

Aidha, suala la uwekaji wa alama makhususi pamoja na usafishaji wa barabara hizo katika Mji wa Zanzibar muhusika mkuu ni Baraza la Manispaa. Hata hivyo, kwa kuona uzito wa jambo lenyewe na kwa kuzingatia gharama za miundombinu hiyo wizara yetu mwaka huu wa fedha katika bajeti yake tuna kiwango cha fedha tutakitumia kwa ajili ya uwekaji wa taa hizo.

Sambamba na hilo kwa kutambua ukuaji wa mji wetu tutaendelea kushirikiana na washirika wengine wa maendeleo pamoja na Baraza la Manispaa ili tuone maeneo yote muhimu tunayapatia ufumbuzi. Naomba ifahamike alama za barabarani ni nyingi na kila dereva analazimika kuzifufuata sambamba na miongozo ya kisheria ya usalama wa barabarani.
Si jambo la busara wala utaratibu unaoeleweka duniani kote kwa dereva kuacha kufuata utaratibu husika na kuongozwa na hisia zake au mitazamo yake binafsi. Tunaendelea kuwasihi

na kuwaelimisha madereva wetu watumie taratibu na miongozo ya kisheria katika shughuli zao za kila siku, kinyume chake hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

(a) Mhe. Spika, sababu za kutokuwepo kwa taa hizo ni baada ya mitambo ya awali iliyokuwepo maeneo kadhaa ya mji wa Zanzibar kuharibika na hivyo Serikali inajipanga kuweka mitambo mipya kama tulivyoeleza katika maelezo yetu ya awali.

(b) Sio kweli kwamba kutokuwepo kwa taa hizo kunahatarisha usalama kwa sababu bado alama zote za usalama wa barabarani zipo na zinaongoza mtiririko mzima wa shughuli za usalama barabarani.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nilisema swali langu lina vifungu (a), (b) na (c). Yeye kajibu vifungu viwili tu. Naomba na kifungu cha (c) kilichopo ukurasa wa 3 pia ajibu halafu tena nije na swali la nyongeza.

Mhe. Spika: Anasema majibu hayajakamilika. Jibu la (c) halikujibiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kifungu cha (c) tumekitolea majibu katika maelezo yetu ya awali.

Mhe. Spika: Naam.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nasema kifungu cha (c) tumekitolea majibu katika maelezo yetu ya awali.

Mhe. Spika: Mhe. Salim Abdalla Hamad kifungu cha (c) kimetolewa katika maelezo ya awali.
Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, sawa.

Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri Mhe. Naibu Waziri aliyoyatoa na ninampongeza kwa hilo. Lakini kwa sababu Mhe. Spika, serikali hii iliweka taa maalumu katika sehemu za mkusanyiko wa barabara, sisi tunaita *round about* kwa kuhakikisha kuwa utaratibu unafuatwa wa gari katika sehemu zote zinazotokea zinapita mule kwa kufuata taa zinavyowaka na rangi zake, na taa zile hazifanyi kazi kama alivyoeleza mwenyewe lakini kasema si kweli kuwa kutokana na alama zilizopo kuwa zinahatarisha amani.

Jee, kutokuwepo kwa taa hizi kufanya kazi na wakati taa hizi ziliekwa kwa makusudi zifanye kazi si kuhatarisha usalama barabarani. Na kwa nini ikiwa si kweli siku zote gari zinagongana na hata jana kulitokea athari kubwa sana pale Mwanakwerekwe kwa sababu ya hivi hivi ya kutokuwepo alama za barabarani. Hilo ni la mwanzo.

Halafu la pili Mhe. Spika, ninapenda kuuliza ni kuwa kuna zile *round about* muhimu, kama ile ya Maungani, Mwanakwerekwe hazina taa za barabarani lakini ni mahala ambapo kuna mkusanyiko wa gari nyingi sana tu na kila dereva anatumia akili yake, wengine wanakwenda kwa ustahamilivu kwa kujua kuwa wengine wanafanya wanavyotaka. Haoni kwa mule namo kwa kutokuwekwa hizo taa zikaongoza pia ni kuhatarisha amani kwa wanaoendesha vyombo hivyo vya moto?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya uwekaji wa taa za usalama wa barabarani ni kurahihisisha harakati na shughuli za usafiri barabarani. Lakini bado suala la muongozo, taratibu na sheria pamoja na alama za barabarani zipo nyingi na dereva analazimika kuzifuata zote.

Suala la taa nchini kwetu ni jambo ambalo limekuja mwisho lakini masuala ya sheria, taratibu za madereva zipo kwa muda mrefu. Kwa hivyo nimsihi tu Mhe. Mwakilishi kwamba suala la uwekaji wa taa tumelichukua na maelezo yetu ni kwamba tutahakikisha maeneo yote muhimu tunawawekea taa hizo lakini suala la kufuata sheria lipo pale pale, alama za barabarani zipo na kila dereva anatakiwa awe amehitimu kulingana na utambuaji wake wa alama na maelekezo yote muhimu kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani.

Suala lake la pili, maeneo haya ni miongoni mwa maeneo muhimu ambayo tumeyalenga ikiwa ni pamoja na *round about* ya Mwanakwerekwe, Kwamchina na maeneo mengine ambayo yanayosababisha msongamano usiokuwa na sababu za msingi.Tutaweka taa pale tu kadri ya hali ya fedha itakapokuwa inaruhusu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, Wizara hii huwa ina tabia ya kuchimba mitaro katika barabara zetu wakati barabara zimeshatengenezwa, na mitaro hiyo ni ya kupita maji machafu na wizara yako huwa inachukua muda mrefu kuitengeneza au kuijenga mitaro hiyo, jambo ambalo huwa linasababisha athari ya maji kutapakaa kutapakaa katika majumba. Mfano njia ya Kijichi. Kwa nini wizara yako ikiwa bado haijajipanga ili kuwa na mipango ya kuendeleza kujenga mitaro hiyo, huwa inazichimba njia hizo wakati wizara haijajipanga na kuziitengeneza mitaro hiyo.

b) Kwa kuwa mitaro ile inayochimbwa baadhi hupelekea kutuletea ajali. Je, Mhe. Waziri unatuambia nini kuhusu mitaro hiyo wizara yako inayochimba wakati haijawa tayari kuitengeneza?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, dhamira kubwa ya uchimbaji wa mitaro ni kutaka kuona ni kwa kiasi gani tunazinusuru barabara zetu, kama tunavyotambua kwamba maji ndio adui mkubwa wa barabara zetu. Kwa hivyo, maeneo yote ambayo tunachimba mitaro malengo yetu ni kukamilisha kwa wakati. Kuna baadhi ya maeneo tunashindwa kukamilisha mitaro hiyo kutokana na sababu nyingi, ikiwemo ukosefu wa fedha, mradi wa umekisiwa (umewekewa fedha kidogo), mahitaji kutokana na ardhi husika, pengine makisio yalikuwa madogo kulingana na ile ardhi husika tunalazimika kwamba tuongeze gharama kama lile suala la Kijichi, tulikuwa tuna malengo ambayo mradi ule ungekamilika kwa gharama za awali. Kwa bahati mbaya katika wakati wa utekelezaji wa mradi gharama zikaonekana kubwa kutokana na maumbile ya ardhi yenyewe, kwamba kuna maeneo ambayo mnaweza mkachimba mtaro mtupu, kuna maeneo ambayo mkichimba mtaro lazima mmalizie na *stone perch*. Kwa hivyo, kuna baadhi ya maeneo kama barabara ya Kijichi tutalazimika tuweke *stone pach*, jambo ambalo mwanzo hatukuwa tumelilenga.

Kwa hivyo, madhumuni ya wizara ni kwamba tunachimba mitaro kwa ajili ya malengo ya kunusuru barabara. Maeneo ambayo ardhi haikubali ni lazima tujenge, tutalazimika tusubiri ili tupate fedha za kuweza kujenga *stone pach* ili kunusuru ardhi isimong'onyoke kufikia yale malengo ambayo tumekusudia ya kunusuru barabara.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kumekuwa na usumbufu mkubwa kutoka barabara ya kutoka Mkoani Bandarini mpaka Chake Chake, barabara ile imekatwa vipande na kuchimbwa kwa ajili ya matengenezo, lakini imekuwa na muda mrefu sana. Wananchi wanaoendesha vyombo vyao vya moto ikiwemo gari, pikipiki na vespa na hata wapita njia wanapata usumbufu mkubwa sana. Sasa kama wizara haijawa tayari au watengeneza barabara ile kwa nini wanaichimba. Mhe. Spika, tunaomba kujua.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara ya kutoka Mkoani mpaka Chake Chake, kulikuwa kuna baadhi ya maeneo barabara ilikuwa imechoka, imepasuka na ilikuwa kuna mashimo. Wajibu wetu sisi kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kuhakikisha kwamba tunaziba mashimo yote. Katika uzibaji wa mashimo hayo kuna hatua, hatua ya awali ni kukata maeneo yale na kuweka kifusi kipya, kushindilia vizuri na wakati tunakamilisha kazi hiyo tulikuwa tuna upungufu wa lami, lakini kwa muda huu tunaongea tayari lami imekwishafika Pemba, tunaamini katika kipindi cha muda mfupi kazi hizi zitakuwa zimeshakamilika na huo usumbufu ambao wanaupata wananchi wetu utakuwa haupo tena.

Nam. 41

Mpango Mbadala wa Ukuzaji Uchumi

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Zanzibar uchumi wake mkubwa unategemea zao la Karafuu na Utalii;

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta mpango mwengine wa biashara au mradi mwengine wa kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi sali lake Nam. 41 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba hivi sasa Zanzíbar uchumi wake unategemea zao la karafuu na utalii kwa kiasi kikubwa, wakati hapo kabla uchumi wa Zanzíbar ulikuwa ukitegemea zao la karafuu peke yake. Sekta ya utalii Mhe. Spika, iliingia baada ya

juhudi za makusudi zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuifungua na kuikuza sekta hiyo ya utalii.

Hivyo, katika juhudi za Serikali za kutafuta mpango mwengine wa kibiashara ni pamoja na kuanzisha mradi wa kuifanya Zanzíbar kuwa eneo Tengefu la Kiuchumi (*Zanzíbar Special Economic Zone*) ambapo utafiti wake Mhe. Spika, tayari umekamilika na sasa hatua ya kwanza ya kutafuta wawekezaji imeshaanza. Katika mkakati huo imebainishwa miradi mingi ya uwendelezaji viwanda na usarifu wa bidhaa na zaidi bidhaa za kilimo. Sambamba na hatua hiyo ni pamoja na kuifanya Zanzíbar kuwa Kituo cha Biashara.

Mhe. Spika, mradi mwengine ni mkakati wa serikali wa kujenga uwanja wa Maonyesho wa Kimataifa wa Biashara kwa nia ya kutangaza mazao mengine katika masoko ya Kimataifa ili kuongeza mzunguko wa kibiashara na kuvutia utalii wa mikutano.

Pia Mhe. Spika, miradi mingine mikubwa inategemewa kuanzishwa katika sekta husika kama ya uendelezaji wa mifugo na uvuvi, kilimo na huduma kama za mawasiliano, huduma za fedha, elimu na afya.

Utekelezaji wa miradi hii utaweza kuongeza wigo na kupanua nyaja nyengine za biashara kwa ajili ya ukuzaji uchumi pamoja na tija kwa jamii.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kama alivyotueleza Mhe. Waziri kwamba nchi yetu inategemea sana biashara ya karafuu na utalii. Lakini bado nchi hii kutokana na biashara zote hizo zinazofanyika tuko mwisho kiuchimi.

Je, ni lini wizara yako kwa mpango huu uliotueleza utafanyika ili nchi yetu ipate kuendelea?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba arudie swali lake, maana yake nimeeleza mipango mingi, sijui ni mpango upi anaoukusudia yeye.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe rudia swali na ukielekee hicho kipaza sauti.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Naibu Waziri kama jawabu lake alivyotujibu kwamba nchi yetu imejikita katika karafuu na utalii. Swali ninalouliza ni kwamba bado katika biashara zote hizo tunazozifanya, karafuu na utalii tuko mwisho kiuchumi. Je, ni lini hiyo mipango aliyotueleza hivi sasa itafanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, nilieleza hapa kwamba mikakati ya kuinua uchumi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu kidogo ili Mhe. Naibu Waziri apate kujibu maswali na asikike vizuri, ahsante endelea Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimeeleza hapa wakati nikijibu swali kwamba mikakati ni mingi ambayo serikali yetu imekuwa inakusudia kuifanya katika azma nzima ya kuinua uchumi wa nchi. Sasa mikakati yote hii kila moja Mhe. Spika, itatekelezeka kwa wakati wake, haiwezi yote ikatekelezeka kwa wakati mmoja.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye ametuwezesha siku hii ya leo kuwepo hapa katika hali ya uzima na afya.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na ya ufafanuzi mkubwa, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii inaitwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Je, atakubaliana na mimi kwa wakati huu tulionao ili kukuza uchumi wetu kwamba wizara hii ishirikiane na wizara ambazo zinazohusika kwa mlango mmoja au mwengine, ili kuimarisha uchumi wetu, kuhakikisha tunaleta viwanda ambavyo vitazalisha na kukua uchumi wa nchi yetu, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kupokea kwa dhati kabisa pongezi alizonipa na namshukuru kwa kunipongeza.

Mhe. Spika, nikubaliane naye moja kwa moja kwamba ipo haja na ndivyo tunavyofanya katika serikali kushirikiana na sekta husika ndani ya wizara husika, ili kuhakikisha tunanyanyua uchumi wa nchi yetu. Nakubaliana sana na Mhe. Mjumbe kwamba tushirikiane na wizara kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Maliasili, ili kupata bidhaa ambazo zinapatikana hapa nchini tuweze kuanzisha na kuendeleza viwanda kwa lengo zima la kuinua uchumi wa nchi yetu. Nimuhakikishie Mhe. Asha Bakar Makame kwamba tunafanya hivyo na ndio maana hivi sasa tuko katika hatua za mwisho za uandaaji wa sera ya viwanda na mawazo yake yote haya tayari tunayafanyia kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri, katika swali la msingi alisema Zanzibar itakuwa ni kituo cha biashara. Swali langu ni dogo sana. Je, ni lini watakuwa tayari kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo cha biashara kutokana na wafanyabiashara wengi kuondoka nchi hii, kutokana na mateso na maudhi wanayopata katika kisiwa hiki?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mimi nataka nimtowe wasi wasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba wafanyabiashara hawapati maudhi wala serikali hii haitowafanyia maudhi wafanyabiashara kwa kuwa wizara tunafanyakazi nao vizuri sana. Ni kutokana na mashirikiano ya wafanyabiashara hawa ndio maana Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tumekuwa tukifanya kazi zetu kwa umakini mkubwa sana.

Lakini nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim kwamba Zanzibar kuifanya iwe ni kituo cha biashara sio suala la leo na kesho, kuna masuala mengi ya kuzingatia, sekta nyingi ambazo zitahusishwa kwenye hili na nimuhakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa, tunajidhatiti kwamba suala hili tutalifanikisha siku sio nyingi kuanzia leo au kuanzia sasa.

Kwa hivyo, nimuambie Mhe. Jaku Hashim kwamba kwa kuwa yeye ni mfanyabiashara ni mdau mkubwa wa suala hili, basi akae mkao wa kula.

Nam. 93

Adhabu ya Kuasiwa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-
Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu muhimu sana na nyeti kwa wananchi, hasa kwa jamii, naomba kufanya marekebisho katika swali (a) badala ya neno 'kuasiwa' liandikwe 'kuhasiwa'. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba swali langu nambari 93 lipate jawabu muafaka kabisa.

Vitendo vya ubakaji vimekuwa vikiongezeka Zanzibar ambapo kati ya mwezi wa Aprili – Julai, 2013 wanawake 480 wameripotiwa kubakwa na wanaume 54 kulawitiwa.

(a) Kwa nini Serikali isitunge Sheria ya kuasiwa wanaopatikana na hatia ya udhalilishaji wanawake na watoto Zanzibar?

(b) Serikali imefanya utafiti kujua sababu gani zimepelekea kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji Unguja na Pemba?

(c) Kwa nini Serikali imendelea kuachia biashara ya kuuza mitaani CD za video za ngono wakati zinalalamikiwa kueneza tatizo hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto) – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Vitendo vya ubakaji na udhalilishaji wa watoto na wanawake vimekuwa vikionekana kuongezeka kwa sababu hivi sasa vitendo hivyo vinaripotiwa katika vituo vyetu mbali mbali, baada ya kutoa taaluma na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuripoti vitendo vya aina hiyo. Hapo zamani vitendo hivi vilikuwepo, lakini vilikuwa haviripotiwi. Hivyo ukubwa wa tatizo sasa unajulikana kwa vile vitendo hivi vinaripotiwa rasmi.

(a) Mhe. Spika, serikali kwa upande wake bado haijaona haja ya kutunga sheria ya kuhasiwa kwa wanaopatikana na hatia ya udhalilishaji wanawake na watoto Zanzíbar. Suala la kuhasiwa linagusa suala la haki za binaadamu ambalo Zanzíbar inalipa umuhimu mkubwa. Lakini kwa mujibu wa Sheria zilizopo. Kwa mfano, Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Wari na Wajane ya mwaka 1984 na Sheria za mwenendo wa makosa ya jinai zinatosha kuwatia hatiani wanaotenda vitendo vya ubakaji na unyanyasaji wa watoto na wanawake. Kitu muhimu ni kwa sote kushikamana na kupambanana vitendo hivyo. Hasa vyombo vyetu vya dola kutimiza jukumu lake kwa wajibu wao.

(b) Mhe. Spika, serikali inafanya utafiti na inaendelea na juhudi zaidi za kufanya utafiti huo. Kilichogunduliwa kwa hatua za awali za utafiti huo, ni kwamba jamii ya Wazanzibari imeacha maadili ya kulea na kuhisi mtoto wa mwenzako ni mtoto wako. Aidha, ukosefu wa nidhamu na kutokuwepo kwa hatua madhubuti zinazochukuliwa kwa wanaofanya vitendo vya udhalilishaji na ubakaji, nayo pia imechangia kuongezeka kwa vitendo hivyo.

(c) Mhe. Spika, serikali kamwe haikuwachia hata kidogo biashara ya kuuza mitaani CD za Video za Ngono, bado suala hilo ni kosa kwa mujibu wa Sheria za nchi, na atakaepatikana nazo atachukuliwa hatua za kisheria na vyombo vya Dola.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Haki za binadamu zinastahiki kulindwa kwa pande zote mbili kwa anayebaka na anayebakwa. Kwa nini watu hawa wakifikishwa kwenye vyombo vya sheria baada ya muda huonekana wamo mitaani na hupata shida muathirika?

Mhe. Spika, katika majibu aliyojibu Mhe. Waziri anasema serikali haijaachia uuzaji wa kaseti na CD za ngono. Je, utakuwa tayari Mhe. Waziri kwa hili mguu kwa mguu mimi na wewe kwenda kuweka mtego ili kufanikisha suala hili, kwenye duka linalouza kaseti hizi na CD ili tupate uhakika wa suala hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kama nilivyosema suala la haki za binadamu zina pembe nyingi na sehemu nyingi. Sasa kwa wanyama sawa Paka amehasiwa kwa kupunguzwa uzazi. Nadhani sijui kama na mbwa na wao au vipi. Lakini kwa binadamu bado Mhe. Spika, serikali haijafikia uamuzi huo. Serikali kwa kuliona hili iliunda kamati ya mawaziri ili kulifuatilia suala zima la unyanyasaji wa watoto na mambo yanayohusiana na hayo na ripoti hiyo imeshapatikana. Kwa hivyo, tuipe muda serikali iliangalie suala hili ili kujua ni hatua gani za kinidhamu zitachukuliwa.

Mhe. Spika, jana nilihudhuria kwenye sherehe za nyumba salama, ambapo sherehe hizi zilifanyika pale *Ocean View* na Mhe. Makamu wa Kwanza alikuwa ni mgeni rasmi, yaani ni nyumba ambazo zimejengwa kwa ajili ya kuwahifadhi kina mama ambao wanafanyiwa ukatili na waume zao, yakiwemo mambo haya ambayo tumeyataja. Yote haya ni kutaka kuwapa elimu au tunasema *counselling* ili kuondokana na tatizo hili. Mhe. Spika, taaluma inahitajika sana. Ni kweli vitendo hivi vimeongezeka na lazima serikali ijidhatiti katika suala hili.

Mimi napenda kuahidi kwa kupitia wizara yetu hii ya Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kwamba suala hili bado tutalifanyia kazi kiasi ambacho hatua zote ambazo tunahisi zichukuliwe kwa watu hawa ili liwe ni funzo, basi lichukuliwe. Jana kulikuwa na mama mmoja anahojiwa, anasema mtu mmoja aliyefanya vitendo hivi alifungwa miaka 15, miaka hii siingefaa akafungwa miaka 30. Lakini huko mbele pengine serikali ikaamua kuwafunga maisha vile vile, kwa sababu wakibakia mitaani hawa wana madhara. Wengine wana kesi moja au mbili au tatu ni kesi nyingi. Kwa hivyo, *Inshaallah* serikali itafanya juhudi.

Suala la kwenda mguu kwa mguu, kama sio mbali tutakwenda, kama ni mbali tutakwenda kwa gari tutafuatana mheshimiwa ili tulifuatilie mimi na watu wangu wanaohusika na masuala haya wizara hii. Atakayepatikana anauza kanda hizi, madamu sasa hivi tunasema hivi basi huko zitaondoshwa kwa sababu wanasikiliza, lakini kama bado watakuwa wameziweka basi watakuwa wanazidi kuonesha jeuri na kiburi, huyo atachukuliwa hatua hapo hapo na tutakwenda na vyombo vyetu vya usalama ili kumshughulikia ipasavyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametukumbusha kwamba mwaka 2011 Baraza hili lilipitisha sheria nambari 6 ya kumlinda mtoto, sheria ile ilikuwa na madhumuni ya kumlinda mtoto bila ya kubagua kama ni mtoto wa kike au wa kiume, sheria ilitafsiri mtoto kwamba ni kuanzia siku moja mpaka chini ya miaka 16. Sasa Mahakama zetu hapa Zanzibar zimekuwa zikitoa adhabu baada ya mtoto kudhalilishwa.

Mhe. Spika, hivi karibuni kuna mtoto wa kike ambaye alidhalilishwa na mdhalilishwaji alifungwa miaka 28, lakini mtoto wa kiume ambaye alilawitiwa mdhalilishaji alifungwa miezi 10. Je, hatuoni kwamba mtoto wa kike anapewa hadhi zaidi kulindwa na sheria hii, kuliko mtoto mwanamme. Kama hivyo ndivyo, kwa nini sheria haisemi wazi kwamba hakuna ubaguzi baina ya mtoto wa kike na wa kiume. Kwa nini mtoto wa kiume mdhalilishaji afungwe miezi 10, lakini mtoto wa kike aliyedhalilishwa mdhalilishwaji afungwe miaka 28?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, aliyehukumu ni Jaji na yeye atakuwa na uthibitisho gani kwamba huyu akamuhukumu miaka 28 na huyu mwengine miezi 10, inatokana na vielelezo na ushahidi uliotolewa. Sasa kwa mimi hapa sasa hivi siwezi kutoa maelezo, lakini nadhani kama sheria haiko wazi kiasi hicho, basi ni vizuri tukaiangalia ili haki ikatendeka kwa watoto wote, awe mwanamke au mwanamme. Kudhalilishwa ni kudhalilishwa tu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kuongezea pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri amezungumzia. Katika utoaji wa adhabu kwenye kesi yoyote ile, kuna kitu ambacho kinaitwa *Incubating Factors*, yaani ni mambo ambayo yanaweza yakasababisha Mahakamani pale ama adhabu ikawa kubwa au adhabu ikawa ndogo. Mambo hayo anayeyajua ni Hakimu au Jaji aliyepo pale, huwezi tu ukasema kwamba kosa hili mtu apewe adhabu kiasi hiki na kosa hili mtu apewe adhabu kiasi hiki, uamuzi huo anao Hakimu kutokana na mambo ambayo yameelezewa Mahakamani pale.

Sasa kutokana na hayo Mhe. Spika, pengine ndio sababu yule wa mwanzo akafungwa miaka 28 kutokana na mambo mbali mbali ambayo yanaweza yakajitokeza na yule mwengine akafungwa miezi 10 kutokana na mambo mbali mbali pamoja na hizo *Incubating Factors* ambazo zimetolewa. Lakini hata hivyo, ikiwa kuna mambo ambayo yamekosewa kisheria, basi waendesha mashtaka wanayo haki ya kukata rufaa ili adhabu ile iweze kuongezewa huo ndio utaratibu Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake ya msingi amekiri kwamba sheria zipo na zilizopo zinatosha kuwatia hatiani wahalifu hawa bila ya kuhasi. Je, ni kwa nini kesi zinazoripotiwa ni nyingi sana kuliko ambazo zinazotolewa hukumu?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nikijibu nilivitaja hasa vyombo vya dola kutimiza jukumu lake na wajibu wao na hapa ndipo tunapopata malalamiko ya kwamba kweli vyombo vyetu vya sheria vikiwemo vyombo vya dola, suala hili kwa kweli linawavunja moyo wananchi mara nyingi sana, kwa sababu ushahidi unakuwepo, kila kitu kinapatikana, yaani hakuna kitu ambacho kimejificha mambo yote yako wazi na matokeo yake utaona kwamba hatua hazichukuliwi. Sasa hapa ni vyombo vya sheria kujitahidi kufuata maelekezo na sheria, kwa sababu sheria zimeweka anayepatikana na kosa hili anahukumiwa hivi, akipatikana na jambo hili atahukumiwa hivi.

Kwa hivyo, inapotokezea ushahidi umepatikana kila siku na bado unaambiwa kwamba hakuna ushahidi, ni kitu ambacho wananchi kinawavunja moyo sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria yupo, nadhani atachukua ujumbe huu na kuupeleka kwenye vyombo vinavyohusika ili tusaidiane kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake.

Nam. 5

Tatizo la ZBC – TV Kushindwa Kurusha Matangazo - Dar es Salaam

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Televisheni ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) imeshindwa kurusha matangazo yake kufikia jijini Dar-es-salaam na sehemu nyengine za Tanzania Bara na kupelekea kutofahamika na wananchi wa huko na hatimae kukosa matangazo ambayo yangesaidia kupata fedha za kugharamia shughuli ndogo ndogo za *ZBC*.

(a) Je, Wizara inalijuwa hili na kama inalijuwa ni hatua gani zilizochukuliwa hadi sasa katika kutatua tatizo hili?

(b) Ni njia gani inayotumika kurushia matangazo kutoka kituo cha ZBC Dar- es-salaam kuja studio ya Rahaleo?

(c) Je, njia hiyo ni mwafaka kwa ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia na inaweza kuliwekea mazingira mazuri shirika kuingia katika mfumo wa Digitali kikamilifu?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.
5 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nchi za Afrika Mashariki zilikubaliana kuanza rasmi matangazo ya Digitali tokea Januari mwaka huu. Nchi ya Tanzania Bara ilizima matangazo yake ya Analojia kwa Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Mikoa na kuanza matangazo ya Digitali. Kwa kuzima mitambo ya matangazo ya Analojia ilipofika Januari mwaka huu wananchi wote walikuwa wakipata matangazo ya Analojia Kwa Dar es Salaam na Zanzíbar matangazo hayo yalikatika. Ndio maana kuanzia mwezi wa Januari wananchi wa Zanzíbar waliokuwa wakipata matangazo ya ITV, Star TV, TBC na Channel Ten kwa kutumia antena ya kawaida wamekosa matangazo hayo.

Mhe. Spika, kwa nchi ya Zanzíbar tulianza kufunga mitambo ya Digital kuanzia mwezi wa Novemba 2012 na tulipofika Februari 2013 tulianza majaribio ya matangazo ya Digitali. Katika kuanza majaribio hayo tulilazimika kwenda kwa wakati mmoja matangazo ya Digitali na Analojia. Na ili matangazo ya digitali ya ZBC yaweze kufika Mkoa wa Dar es Salaam na kwengineko wanafanyia kazi hatua mbili.

a) Mhe. Spika, wizara yangu inalielewa hilo na ili matangazo ya digitali ya ZBC yaweze kufika Mkoa wa Dar es Salaam na kwengineko, ZBC wanafanyakazi hatua mbili;

   i) Kufikisha matangazo ya ZBC kwenye vituo vyenye mitambo ya Digitali vilivyosajiliwa Dar es Salaam ama kupitia moja kwa moja, na mazungumzo yanaendelea na uongozi unaomiliki mitambo ya digital ya AZAM TV ambayo itazinduliwa wakati wowote.

   ii) Au matangazo ya ZBC kuunganishwa kwenye *satelite* jambo ambalo linafanyiwa kazi ndani ya Uongozi wa Shirika na hili ndio miongoni mwa majukumu mapya ya bodi mpya ya ZBC iliyozinduliwa wiki iliyopita.

(b) Njia inayotumika kurushia matangazo ya redio kutoka kituo cha ZBC Dar es Salaam kuja Studio ya Rahaleo ni kwa njia ya simu.

(c) Njia ya kutumia simu ni muafaka, na ni miongoni mwa njia ya teknolojia ingawa kila siku njia bora na nzuri zaidi huwa zinavumbuliwa na kutumiwa ambapo mtumiaji atawajibika kuwa na uwezo wa kumudu ununuzi wa miundombinu husika.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa anajibu alisema ya kwamba kuna vituo vitafunguliwa huko jijini Dar-es-Salaam, je vitafunguliwa katika maeneo gani?

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Mwakilishi na kama amenielewa vizuri basi nimemwambia kwamba *ZBC* pamoja na Wizara inazungumza na wamiliki wa Mitambo ya *Azam Television* ambao wao watakuwa wanarusha matangazo haya kwa njia ya *satellite*. Kwa hivyo, mitambo yao iko maeneo ya Temeke nimeambiwa na watakuwa wanarusha moja moja katika *satellite* ambazo *ZBC Television* kwa njia hii itaweza kufika Dar-es-Salaam pamoja na nchi jirani mbali mbali.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba na mimi nimuulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na kukua kwa *ZBC Television* kwa kurusha matangazo yetu na kuweza kupatikana sehemu tofauti. Lakini kulikuwa na tatizo kubwa kisiwani Pemba kwa kuyakosa matangazo ya *ZBC Television*, je tatizo hilo kwa sasa limeondoka? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli bado suala la matangazo ya *ZBC Television* Pemba hayajakaa vizuri, isipokuwa matangazo ya *ZBC Radio* yameshakaa vizuri. Kwa hivyo, kuhusu hili la *ZBC Television* linafanyiwa kazi na nimeambiwa na wahandisi kwamba nadhani mwisho wa mwezi huu wa Oktoba mambo yatakuwa mazuri, lakini hayo ni mambo ya kiufundi na yanahitaji kufuatiliwa vizuri na kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri na tunajitahidi katika hili.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Katika Kikao cha Bajeti nilimuomba Mhe. Waziri kufanya *Promotion* ya Ving'amuzi jambo ambalo alilikubali, vile vile ninashukuru kwamba aliwaarifu wananchi kwamba *promotion* hiyo imeakhirika.

(a) Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako, kwamba anifahamishe ni sababu zipi za msingi zilizofanya *promotion* hiyo kuakhirika?

(b) Vile vile naomba nijue kwamba *promotion* hiyo imepangwa kufanyika lini tena?

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli nakumbuka wakati wa Kikao cha Bajeti Mhe. Mjumbe alipokuwa akichangia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, alichangia umuhimu wa wizara kufanya *Promotion* ya King'amuzi cha *Z Movies*, jambo ambalo kwa nia njema kabisa nililikubali na kulipokea na kuliwekea ahadi ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba kufafanua kwamba wakati nilipokuwa nikitoa ahadi hiyo tulikuwa tumejiridhisha kwamba kifaa kilichowekwa pale Nungwi ambacho kilikuwa kinasababisha kukatikakatika kwa matangazo Pemba ambapo kilikuwa kinafanyakazi vizuri. Lakini bahati mbaya wakati tunapanga *promotion* yenyewe basi kifaa chewenye kilipata hitilafu ya kiufundi na kwa sababu kimo kwenye *guarantee* ikabidi kurejeshwa kwao Afrika ya Kusini kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na ikiwezekana kupewa chengine kipya.

Lengo la *promotion* ile ni kutoa taaluma katika maeneo yote ya Unguja na Pemba na wala haikuwa busara wakati kifaa kile kimeharibika tukafanya *promotion* kwa Kisiwa kimoja cha Unguja tu. Kwa hivyo, sababu kubwa iliyofanya tuzuie ni kwamba ilikuwa hatujafikia wakati wa kwamba shehia pamoja na vijiji vyote sasa *signal* yetu inafika vizuri sana.

Kwa hivyo, kama nilivyosema katika jibu lililopita ni kwamba nimeambiwa na mafundi kwamba mwishoni mwa mwezi huu tunatarajia kuwa kifaa kitafika na hali ya kupatikana *ZBC Television* Pemba itakuwa imeimarika vizuri.

Sasa ninachokiahidi kwa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, ni kwamba mara baada ya *signal* kufika katika shehia pamoja na vijiji vyote vya Unguja na Pemba, basi *promotion* hiyo tutaifanya kama ambavyo tumeahidi.

Nam. 66

Kusuasua kwa Kesi za Wizi wa Mifugo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Zaidi ya asilimia thelathini ya wakaazi wa Jimbo la Wawi katika vijiji vya Furaha, Wawi, Mvumoni, Mfikawa Uwandani, Ngambwa pamoja na Vitongoji wameekeza maisha yao katika mifugo ya Ng'ombe, Mbuzi na Kuku. Kwa kuwa wizi wa mifugo pamoja na mifugo kuliwa na mbwa hususan mbuzi na kuku limeshamiri katika maeneo hayo na kwa kuwa wizi hukamatwa na kufikishwa polisi lakini baada ya muda mfupi wizi hao huonekana mitaani wakitembea kama kawaida.

Je, ni tatizo gani linasababisha kesi za wizi wa ngo'mbe kusuasua mahakamani
na hatimae wezi hao kuachiwa huru?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 66 kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake hilo napenda kumjuilisha kwamba, kwa mujibu wa taratibuu tulizojiwekea kazi ya Mahakama ni kusikiliza kesi zinazopelekwa mahakamani na kutoa uaamuzi. Uamuzi unaotolewa una sura mbili ambazo ni ama kumuona mshtakiwa ana hatia na kumpa adhabu inayostahiki kulingana na sheria au kumwachilia huru iwapo itaonekana hana kosa.

Kwa hivyo, si jukumu la Mahkama kujua sababu zipi ambazo polisi huwaachia watuhumiwa wanofikishwa vituoni mwao wakituhumiwa kwa makosa mbali mbali. Hata hivyo, sheria imetoa uwezo kwa mahkama kutoa dhamana kwa mtu yeyote anayefikishwa mbele yake, iwapo shtaka linalomhusu linastahiki kupatiwa dhamana kwa mujibu wa sheria inayohusu shtaka hilo.

Kisheria, mtuhumiwa wa kosa la wizi wa ng'ombe anaweza kupewa dhamana na pengine ndio maana washtakiwa wa wizi huo baadhi huonekana wakitembea mitaani muda mfupi tu baada ya kufikishwa mahakamani, kwani kukamatwa na kufikishwa mahkamani kwao haina maana kwamba tuhuma zao ndio zimethibiti kiasi cha kutopewa dhamana.

Baada ya maelezo hayo, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba takwimu za makosa ya wizi wa ngombe yalifikishwa mbele ya Mahkama ya Wilaya ya Chake Chake Pemba kwa mwaka 2012 yalikuwa ni manne (4), ambapo kati ya kesi hizo moja(1) ilitokezea katika eneo la Jimbo la Wawi. Kwa mwaka 2013 hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2013 makosa yaliyofunguliwa mahkamani hapo ni manane (8) ambapo makosa (5) yametokezea katika jimbo hilo hilo. Hivyo, kuanzia mwaka 2012 hadi mwishoni mwa mwezi Septemba, 2013 kesi ambazo zilitokezea Jimbo la Wawi ni sita (6). Kesi hizo zilifikishwa mahakamani tarehe 12 Juni, 2013 na hivi sasa bado zinaendelea.
Kutokana na takwimu hizo Wizara ya Katiba na Sheria haioni kama kuna kusuasua kwa kesi hizo za wizi wa ngombe zinazotokezea katika Jimbo la Mhe. Mjumbe au jimbo jengine lolote lile.

Mhe. Spika, Katika kujibu kifungu (b) cha swali la Mhe. Mwakilishi, naomba kumjulisha kuwa Wizara ya Katiba na Sheria haina jukumu la kuangamiza mbwa wanaoranda ovyo mitaani na kula mifugo kama vile kuku, ndama na kadhalika. Kutokana na hali hiyo, ninamshauri Mhe. Mwakilishi alipeleke tatizo hili wizara husika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ya Katiba na Sheria, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama utaangalia Dira ya 2020 pamoja na MKUZA I na II, yaani lengo la MKUZA ni kupunguza umasikini na kuongeza kipato kwa wananchi. Kwa kweli wananchi wa Jimbo la Wawi katika maeneo ya Uwandani, Vitongoji, Mikunguni na kadhalika wanapunguza umasikini na kujiongezea kipato kuputia mifugo ikiwemo ng'ombe na kuku.

Vile vile kwa kuwa wizi huu umeshamiri sana na hizo kesi ambazo amezitaja Mhe. Waziri ni kidogo sana ambazo zimefika hapo mahakamani. Sasa Mhe. Spika, nadhani ameniambia nilipeleke kwenye wizara husika lakini serikali ni serikali tu na wizara yake ni serikali.

(a) Je, kuendelea kuwaachia hawa jamaa kutuibia ng'ombe wetu pale Wawi, Vitongoji na Uwandani si kurudisha nyuma lengo la SMZ la kupunguza umasikini na kuongeza kipato kwa wananchi wake?

(b) Mhe. Spika, kuku pamoja na mbuzi wanaliwa sana na mbwa na sisi tumekwenda kwa mzee mmoja anaitwa Adili Khamis Abdalla mkaazi wa Vumba huyo alikuwa akitusaidia sana kuwapiga magobole mbwa pamoja nakunguru wanaoathiri mifugo yetu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba huu ni karibu mwaka wa pili alikuwa akikodishwa gobole pale Polisi, lakini magobole ya Polisi yote yameshaharibika hivi sasa.

Je, lini watatunga sheria ya kuweza kuwamilikisha watu magobole, kwa ajili ya kupambana na hawa mbwa wanaotuharibia mifugo yetu na kuweza kufuata yale malengo ya MKUZA ya kupunguza umasikini na kujiongezea kipato na kuweza kuwasomesha watoto wetu wakaondokana na kuvuta mambo ya unga na mambo mengine?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza napenda ajue na aelewe kwamba katika serikali kuna mgawanyo wa madaraka kwamba wizara fulani inashughulikia vitu kadha na wizara nyengine inashughulikia vitu kadha. Kwa hivyo, Wizara ya Katiba na Sheria haishughulikii kuua mbwa anayekula kuku wachanga au mifugo, isipokuwa hiyo ni Wizara ya Kilimo.

Kutokana na hali hiyo, naomba kumshauri Mhe. Mwakilishi kwamba kwa masuala kama hayo wizara inayohusika na mambo hayo ya ufugaji ni Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nafikiri ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusika na suala la kutunga sheria kama mifugo ina matatizo na hiyo kama nilivyosema jana inaanzwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kama kuna matatizo, basi Wizara ya Mifugo na Uvuvi ndio inayoanzisha ule utaratibu wa kusema sasa tubadilisheni sheria, ili wenye wanyama kama mbwa na vitu vyengine kama hivyo wapate adhabu kubwa au kali ikiwa mifugo yao italiwa na huo ndio utaratibu kama tulivyoeleza jana.

Jambo la pili Mhe. Spika, ni kwamba katika utaratibu huo Wizara ya Katiba na Sheria wao wanahusika na kesi ambazo zinakuja katika mahakama na kabla hazijafika katika mahakama kuna vyombo vyengine kama vile Jeshi la Polisi. Sasa Polisi wanapopelekewa watu wa aina hiyo wao wana jukumu la kufanya uchunguzi na kutafuta ushahidi wowote ambao upo katika suala lile, wao wanaweza kumuweka mtu ndani kwa kipindi ambacho kinakubalika kisheria pia na wao wanaweza kumtoa mtu huyo kulingana na utaratibu uliopo.

Mhe. Spika, ikiwa watu watakamatwa na kupelekwa polisi na halafu wakaachiliwa, basi hapo vile vile Wizara ya Katiba na Sheria bado haijawa na dhamana ya shughuli hiyo, isipokuwa sisi tunaanza pale inapopelekwa kesi mahakamani ndipo pale Wizara ya Katiba na Sheria inahusika na kama nilivyoelezea hapa kesi zinapokuja zina utaratibu wake zinakwenda na baadaye kama kuna ushahidi basi mtu yule anahukumiwa na kama hakuna basi mtu yule anaachiliwa huru. Vile vile mtu anapoachiliwa huru basi bado anayo haki ya kukata rufaa katika mahakama za juu zinazohusika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya nyongeza yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria naomba kuongezea nyongeza ndogo kuhusu yale matatizo ya mbwa wanaoharibu vipando katika mashamba.

Mhe. Spika, upo utaratibu kwa wanyama waharibifu uliowekwa rasmi na serikali kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa pamoja na wizara husika ya Mifugo na Uvuvi inapotokea tatizo.

Kwa hivyo, wanapaswa shehia husika kuitaarifu Serikali ya Wilaya, kwa ajili ya kuwajuulisha uharibifu huo unaotokea na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wanakuwa na *operation* maalumu ya kupambana na wanyama hao waharibifu, ikiwa mbwa au wanyama wengine wowote na hutolewa ruhusa maalumu ya kutumia magobole na kadhalika, ili kulinda mashamba au vipando vyetu pamoja na mifugo yote kwa ajili ya kujihadhari na wanyama waharibifu.

Mhe. Spika, utaratibu upo kwa maana hiyo ninamshauri Mhe. Mwakilishi kwamba awasiliane na sheha wake, Mkuu wa Wilaya, ili hatua zichukuliwe na utaratibu ufanyekazi na wale wanyama waharibifu washughulikiwe ipasavyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani majibu hayo yatoshe na kutokana na muda unavyokwenda, basi tunakushukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tunaendelea

Nam. 110

Tatizo la Ajira kwa Vijana Waliohitimu Mafunzo

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Serikali inajua idadi ya vijana waliohitimu vyuoni wasio na ajira kwa ngazi ya stashahada, shahada na shahada za juu.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira vijana hao?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 110 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la msingi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Wizara ya Nchi, (OR) Kazi na Utumishi wa Umma imeanza Kituo cha Kukusanya Taarifa za Soko la Ajira ambacho kwa sasa kimo katika hatua za mwisho za kuweka mtandao (*Website*). Kituo hichi kimelenga kukusanya taarifa mbali mbali zinazohusu soko la ajira nchini. Taarifa hizi zitajumuisha nafasi za ajira zilizopo, idadi ya waomba kazi na fani zao na taarifa nyengine muhimu kwa waajiri na watafuta kazi.

Taarifa hizi hutumika kwa lengo la kuwaunganisha vijana na fursa za ajira zinazojitokeza kupitia ngazi mbali mbali za umma na binafsi. Aidha, taarifa hutumika pia katika kuwapa fursa za mafunzo yanayohusiana na kujiajiri kila yanapotokea

Mhe. Spika, hadi kufikia Septemba mwaka huu, jumla ya vijana waliosajiliwa katika kituo chetu kwa ngazi mbali mbali ni kama ifuatavyo:-

a) Shahada ya Kwanza 42,
b) Stashahada 92 na
c) Cheti 54
   Jumla ni vijana 188.

Kwa kweli idadi hii kwa wale tu ambao wamekuja kujisajili na jua wako wengi ambao bado hawajajisajili. Kwa hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuwahimiza vijana kujisajili katika kituo chetu hichi, ili tuweze kuwaunganisha na waajiri pale fursa zinapopatikana.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi imekuwa ikichukua hatua mbali mbali katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira, ili kuwapunguzia ukali wa maisha. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ilianzisha mpango maalumu wa Kazi Nje Nje (KNN) kwa lengo la kuwajengea uwezo vijana wetu juu ya ujasiriamali, ili nawao waweze kuwapatia mafunzo hayo vijana wenzao. Kupitia mpango huu, jumla ya vijana 32 walipatiwa mafunzo hayo ya ujasiriamali na serikali ililenga kuzalisha ajira 6,400 Unguja na Pemba kupitia mpango huo.

Vile vile serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilianzisha Mpango wa Ajira kwa Vijana, ambao unatekelezwa kupitia taasisi mbali mbali na kuratibiwa na wizara yangu. Kupitia Mpango huu wa kitaifa jumla ya ajira 950 zinategemewa na kupatikana ifikapo mwaka 2016.

Aidha, Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imelenga kutoa ajira 2,464 kupitia Sekta za Umma. Hatua zote hizi zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaohitimu katika viwango mbali mbali vya elimu wanapata fursa za ajira na kuweza kupata kipato halali.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa vijana kubadili tabia na kupenda kufanya kazi za kujiajiri zaidi kuliko kukaa na kusubiri ajira za serikali, kwani kwa sasa uwezo wa serikali kuwaajiri vijana wote ni mdogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, taarifa za serikali zimetuonesha wazi kwamba zaidi ya asilimia 17 ya vijana wa Zanzibar hawana ajira na serikali imekiri kwamba wao ndio wenye jukumu la kutafuta ajira kwa ajili ya vijana wetu.

Kwa hivyo naomba kujua kwa mwaka 2013/2014 kwa bajeti hii ya serikali tuliyoipitisha wizara yake imepanga kuwapatia ajira vijana wangapi, ili kupunguza ile asilimia 17 ya vijana ambao hawana ajira.

(b) Mhe. Spika, pamoja na serikali kuunda Tume ya Utumishi Serikalini na madhumuni yake makubwa ni kuondosha aina yoyote ya upendeleo wa ajira, lakini kadri tunavyokwenda kumekuwa na malalamiko ya upendeleo wa ajira katika kada mbali mbali.

Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ni lini wizara yake itaondosha udhaifu huu wa kupendelea ajira kwa vijana wetu, ili kuweka sawa ile misingi ya uwajibikaji wa serikali?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, katika jibu langu la swali mama nilisema ajira za serikali zilizotengwa safari hii ni 2464. Vile vile alisema Mhe. Mjumbe kwamba kuna upendeleo. Mimi nimekabidhiwa wizara hii na wala siwezi kusema

kwamba limefanyika au halikufanyika, lakini nasema kwa asilimia 99 kwamba suala la upendeleo halipo.

Kwa kweli ajira za siku hizi zinakuja kisheria na Mhe. Waziri aliyetangulia alilitolea ufanuzi hapa kwamba zinatangaziwa, watu wanaomba, wanafanyiwa interview na baadaye kwa wale ambao wamefanikiwa basi wanachukuliwa na kujuilishwa. Sasa kama kuna upendeleo inaweza kuwa ni dhana, lakini kama kuna chembe ya jambo kama hilo na kama kuna ushahidi basi namuomba Mhe. Mjumbe tushirikiane, ili tuweze kujua kama kuna matendo kama hayo yanafanyika na binadamu hakuna aliyekamilika na udhaifu unaweza ukapatikana.

Kwa hivyo, *inshallah* Mhe. Mjumbe ninamuomba sana aje tuonane mimi na yeye na anidokeze tu kwamba mahala fulani kumefanyika hivi, basi *inshaallah* tutachukua hatua za kufaa, ili kunusuru hali hiyo isiendelee. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, na majibu hayo yatoshe kwamba swali hili limejibika. *(Makofi)*

Nam. 22

Matumizi ya Dawa za Uzazi wa Mpango

Mhe. Salma Mohammed Ali (Kny: Mhe. Farida Amour Mohamed) – Aliuliza:-

Nchi nyingi duniani ikiwemo Zanzibar hudhibiti ongezeko la watu katika nchi zao kwa kuwahamasisha akinamama kutumia Dawa za Uzazi wa Mpango. Kwa kuwa kabla ya matumizi ya dawa hizo kina mama hulazimika kufanyiwa vipimo vya kiafya "*medical check up*", ili kuona kuwa hazitasababisha madhara kwa afya zao na ndipo huruhusiwa kuanza matumizi ya dawa hizo.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea akinamama kutopimwa na hatimaye kusafishwa njia za uzazi "*reproductive system*" pale watakapoamua kuacha dawa hizo na kuzaa tena?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kinamama kupimwa wakati anapotaka kuanza kutumia uzazi wa mpango, kufanyiwa vipimo vya kiafya ni lazima kwa sababu aina na njia za uzazi wa mpango ziko nyingi na tofauti.

Ili ipi itumike ni muhimu kufanya vipimo kwa usalama wa mama pia kumuongoza mtoa huduma hizo kumshauri mama njia ipi kati ya alizonazo zinazoweza kumfaa na kumsaidia kuchagua. Kwa hiyo kupima presha, upungufu wa damu, mkojo, kupimwa matiti, uvimbe wa tumbo, ini wengu, tezi ya shingo ya uzazi, uvimbe wa miguu, uzito na kuanzalia sehemu zake za siri ni muhimu kabla mama hajaanza kutumia njia yoyote ile ya uzazi wa mpango.

Mama anapoamua kuacha matumizi ya uzazi wa mpango halazimiki kusafishwa, kwa sababu hakuna ushuhuda wa kitaalamu unaoonesha ulazima wa kufanya hivyo.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa akinamama wengi wamejenga hofu juu ya utumiaji wa dawa hizi kwa ile dhana ya kuwa dawa hizi zinasababisha ugonjwa wa kensa na mara nyengine pale wanapoamua kuacha kutumia dawa hukosa kizazi kabisa.

(a) Je, Wizara ya Afya inawaambia nini wananchi juu ya suala hili?

(b) Je, Mhe. Waziri haoni umuhimu wa kutayarisha vipindi na kuwapa elimu akinamama hao juu ya suala hilo?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, masuala ya kujenga hofu ni masuala yanayoenezwa katika njia za kawaida ya akinamama wenyewe, lakini hakuna uhakika wala ushahidi huo na ndio maana kabla hujafanyiwa lolote inabidi ufanyiwe vipimo.

Kwa hivyo, ninachowaomba akinamama wasitiane hofu kwa hilo ni kwa faida yao ndio maana vikaja vipima kabla ya kutumia uzazi wa mpango, kwa ajili ya kuwasaidia kwa afya pamoja na kuwasaidia kuzeeka kwa kuzaa sana na wala hakuna sababu ya kuogopa.

Hofu ya kwamba wanakosa kizazi kabisa vile vile si kweli, kwa sababu ninavyosikia wengine ndio huzaa zaidi yaani watoto wengi wanapoacha kutumia dawa za uzazi wa mpango. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la vipindi ni kwamba tunavyo vipindi katika Idara yetu ya Kinga. Kwa kutokana na ushauri wa Mhe. Mjumbe, basi tutaendelea kuongeza na hiki kinachohusu mambo haya tutaendelea kukishajihisha zaidi, kwa ajili ya kuwasaidia akinamama.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, tunashukuru naona muda wa maswali karibu umekwisha na kwa saa yangu kuna dakika tano nafikiri hii iko mbele kidogo. Kwa hiyo, hebu twende kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Nam. 33

Mzigo wa Masomo kwa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman – Aliuliza:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inastahili pongezi kwa msimamo wake wa kutaka kila mwananchi apate haki yake ya msingi ya kupata elimu, kama ilivyo dhamira ya Mapinduzi Matukufu ya 1964. Hata hivyo, kuna tatizo kubwa kwa watoto wetu wanaoanza darasa la kwanza kwa kupangiwa masomo 8.

Je, serikali haioni hili ni tatizo kwa watoto hao kubebeshwa idadi hiyo ya masomo katika hatua ya mwanzo?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 33 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba, wadau au wananchi ama wahusika wengi wanalilalamikia suala hili la kwamba masomo manane kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza ni mengi.

Lakini nataka nimuelezee kwamba mwezi wa Novemba mwaka 2008 wizara yangu ilizingatia masuala ya aina hiyo hiyo kwamba vipindi vilivyokuwa vinatolewa wakati ule vipindi vitano ni kidogo sana. Kwa hivyo, wizara ikakaa chini na kulizingatia suala hilo ndipo vipindi vikaongwezwa badala ya vitano vikawa vinane.

Mhe. Spika, utaratibu huu wa vipindi vinane vinakubalika kwa nchi mbali mbali kwa mfano, nchi ya Japan vina vipindi vinane (8), Malaysia vipindi tisa (9), nchi nyengine Jamuhuri ya Korea ina vipindi kumi na tatu (13) kwa darasa hilo la kwanza.
Kwa hivyo, malalamiko na manung'uniko tumeyasikia na utengenezaji wa mitaala si jambo dogo, yaani ni jambo refu kidogo. Kwa hivyo, tulikusudia tulizingatie suala hili na tulibadilishe mwaka 2016 ndio kipindi ambacho mitaala iliopo sasa itakuwa imeshamalizika. Lakini kutokana na malalamiko na hoja nyingi zinazojengwa na wananchi tumeamua tuanze kulifanyia kazi suala hilo. Kwa hivyo kwa ufupi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali, kwamba ni kweli wananchi wanalalamika na wanasema na sisi tumeanza kulifikiria suala hilo na tunaanza mchakato wa hiyo mitaala ili sasa turudi kuangalia uwezekano wa kurudi katika masomo matano au manane kama wananchi wanavyosema. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara Zanzibar

Mhe. Waziri wa Afya Kny/ Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara Zanzibar.

Mhe. Spika, kuweka msingi na masharti ya jumla ya kuanzisha na kuendesha biashara ni moja wapo ya hatua muhimu katika kujenga mazingira rafiki ya ukuzaji biashara na uwekezaji hapa Zanzibar. Hatua nyengine yenye uzito mkubwa pia ni kuweka mfumo bora wa kusimamia utoaji wa leseni za biashara, kama ilivyokuwa kwa sheria ya biashara mfumo wa utoaji leseni za biashara na usimamizi wake uliathirika na mabadiliko ya kisera yaliyojitokeza katika mwaka 1980 na ambayo kwa ujumla wake yalijielekeza zaidi katika kujenga uchumi kwa misingi ya nguvu za soko. Hivyo kuibuka kwa mazingira hayo mapya kulisababisha mfumo na sheria ya utoaji leseni za biashara kupungukiwa nguvu za usimamizi.

Mhe. Spika, hivi sasa utoaji wa leseni za biashara hapa Zanzibar unasimamiwa na Sheria ya Leseni ya Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983. Sheria hii ndio sheria kuu inayosimamia utoaji leseni za biashara hapa Zanzibar. Hata hivyo zipo sheria nyengine 68 ambazo zinasimamia kwa namna moja au nyengine mwenendo wa biashara na utoaji wa leseni hapa Zanzibar.
Kadhalika zipo sheria nyengine zinazosimamia biashara katika maeneo yanayoendeshwa kimuungano kama vile sheria za mawasiliano ya simu *TCRA*, sheria ya Mabenki (Benki Kuu), Usafiri wa Unga (*TAA*) na nyenginezo.

Athari Zitokanazo na Mfumo Uliopo

Mhe. Spika, athari zitokanazo na mfumo uliopo wa utoaji wa leseni kwa biashara na uchumi na hasa wingi wa leseni na wingi wa vyombo vya utoaji leseni zilibainika kipindi kirefu. Utafiti uliofanywa ulibaini kuwepo kwa aina 243 za leseni za kuendesha biashara ambazo zinatolewa kwa mujibu wa sheria zilizoelezwa hapa juu.

Mhe. Spika, huko nyuma serikali ilifikiria wazo ya kuwa na chombo cha kutoa leseni kama moja wapo ya suluhisho la tatizo la wingi wa vyombo vya utoaji leseni na leseni zenyewe. Wazo hilo lilifunganishwa na matamko ya sera za kitaifa kuhusu biashara kama vile Sera ya Biashara 2006, Sera ya Uendeshaji wa Ujasiri Amali 2006, Mkakati wa Kitaifa wa kuimarisha usafirishaji biashara nje ya mwaka 2009 -2015. Hata hivyo hatua ya kuwa na chombo kimoja imeonekana kuwa na ugumu kiutekeleza kutokana na ukweli kuwa msingi mkuu wa kutoa leseni kuwezesha chombo kinachotoa leseni hiyo kuwa na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni husika. Chombo kimoja kisingeweza kuwa na utaalamu na weledi wa masuala yanayosimamiwa na vyombo mbali mbali vinavyotoa leseni kwa ajili ya ufatiliaji.

Mhe. Spika, utafiti uliofanywa kuhusu hali na biashara ndogo ndogo hapa Zanzibar mwaka 2007, kulibaini kuwa karibu asilimia 1997 ya biashara zinaendeshwa nje ya mfumo wa kisheria kutokana na sababu zifuatazo:

1. Urasimu na taratibu ngumu za usajili wa biashara na upatikanaji leseni.
2. Muda mrefu wa kusajili biashara au kampuni ambapo huchukua siku 86 na ngazi 28 za kiutawala.
3. Ugumu wa kupinga tathmini ya malipo ya kodi ambapo imebainika kuchukua zaidi ya siku 300 na kupitia ngazi 76 za kiutawala.
4. Ugumu kwa mabenki kuchukua mali zilizowekwa dhamana na wadeni wao wanaposhindwa kulipwa mikopo waliyochukua.

   Hivyo kwa ujumla utafiti huo ulibaini mambo matatu makubwa kama ifuatavyo:-

1. Kuwepo kwa mfumo wa kisheria usiorafiki kwa ukuwaji biashara na uwekezaji ambao pia husababisha kuwepo kwa gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara. Urasimu na kutovutia au kusaidia urasimishaji biashara hizo.
2. Kuisukuma sehemu kubwa ya biashara kuendeshwa nje ya mfumo wa kisheria na kusababishwa kuanzishwa kwa mfumo mbadala uliouwezesha sekta hiyo kufanya biashra kwa urahisi.
3. Kusababisha ugumu wa kusimamia mwenendo wa biashara.

Mhe. Spika, kwa kutambua udhaifu wa mfumo wa sasa serikali ilifanya utafiti wa kutathmini mfumo huo kubainisha upungufu na kuandaa mfumo mbadala wa sheria na usimamizi utakaowezesha kukabiliana na matatizo yaliyopo. Kwa muhtasari Mhe. Spika, utafiti huo ulibainisha mambo makubwa yafuatayo:

1. Mfumo uliopo wa kisheria na usimamizi umepitwa na wakati.
2. Mfumo huo hata kama ungewiana na wakati hautekelezeki.
3. Mfumo huo haujawahi kutekelezwa.
4. Kwa sasa mfumo huo haukidhi mazingira na mahitaji ya utoaji leseni, usajili na ufanyaji biashara.

Chimbuko la Mswada

Mhe. Spika, chimbuko la Mswada wa sheria kama nilivyoeleza katika utangulizi hapo juu kuwa mfumo wa utoaji leseni za biashara uliyopo hivi sasa haukidhi dhamira na malengo ya Sera ya Kukuza Biashara, imebainika kuwa mfumo uliopo ni moja ya vyanzo vya urasimu unaoathiri ukuaji wa biashara, kukwaza uwekezaji na kuathiri ufanisi wa kiuchumi, kudhoofisha motisha kwa wafanyabiashara kubadilika kulingana na mabadiliko ya soko la ndani na nje ya nchi. Kupunguza ari ya ubunifu na ukuaji wa ujasiri amali.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Biashara ya mwaka 2013 unaweza misingi na masharti ya kisheria inayotoa haki kwa wananchi kuanzisha na kuendesha biashara hapa nchini kwa kiasi, misingi hiyo pia inajitokeza katika sheria ya sasa ya leseni. Hata hivyo sheria iliyopo imeonekana kuwa na upungufu katika maeneo mbali mbali muhimu.

1. Kwanza sheria hiyo haikuweka umuhimu wa kutosha kwa kutumia leseni kusimamia biashara.
2. Haikuzingatia mambo mengine muhimu ya kibiashara kama vile usalama wa bidhaa, afya na mazingira. Ingawa zipo sheria nyengine zinazohusika na masuala hayo.
3. Kwa ujumla sheria iliyopo haikuweka mkazo katika suala la ukaguzi ambapo leseni ingetumika kama chombo muhimu cha usimamizi kwa biashara.

Mhe. Spika, eneo jengine lililobainika kuwa na udhaifu katika utekelezaji wa sheria hiyo ni ugumu wa utaratibu wa kuomba leseni kulingana na masharti ya sheria hiyo, maombi yote ya leseni yalipaswa kufuata utaratibu ufuatao.

1. Maombi yote ya leseni yawasilishwe kwanza katika mamlaka za mji au Wilaya inapofanyika biashara husika,
2. Baada ya maombi hayo kupokewa katika ngazi ya Mji au Wilaya yawasilishwe na kuzingatiwa na kamati za mapinduzi za Wilaya.
3. Maombi yatakayokubalika katika ngazi ya Wilaya yawasilishwe na kuzingatiwa na Kamati za Mapinduzi za Mkoa.
4. Maombi yaliyoidhinishwa na Kamati za Mapinduzi za Mkoa ndio huwasilishwa katika Bodi ya Leseni kwa kuzingatiwa zaidi na yakikubalika ndipo leseni hutolewa na Afisa wa leseni.

Mhe. Spika, utaratibu huo haukuwahi kutumika katika kipindi chote tangu kutungwa kwa sheria hiyo. Kutotumika kwa utaratibu huo huenda kulisababishwa na mambo makubwa yafuatayo:

1. Kutoanzishwa kwa bodi ya leseni za biashara kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 6(1) cha sheria hiyo.
2. Kutoteuliwa kwa maofisa wa leseni wa Miji na Wilaya kama inavyoelekezwa katika kifungu cha Nam 8 cha Sheria ya Leseni.
3. Mabadiliko ya Kisera katika uendesheja uchumi na biashara.

Hivyo kutokuwepo na mambo ya msingi bila ya shaka kulichangia kudhoofisha uwezo wa kiusimamizi wa sheria hiyo ingawa iliendelea na inaendelea kutumika kama sheria mama ya kusimamia utoaji wa leseni za biashara nchini.

Mhe. Spika, licha ya kutokuwepo kwa mfumo wa kitaasisi wa kutekeleza sheria hiyo ilibainika vile vile kuwa kifungu cha 11 cha sheria hiyo hakiendani na dhamira ya msingi ya kuwawezesha wananchi kuanzisha na kuendesha biashara kwa kuweka masharti ya upendeleo wa aina ya wafanyabiashara watakaopewa umbele wa kupatiwa leseni.Vyama vya Ushirika ndiyo vilivyotakiwa kupewa umbele huo ingawa watu mmoja mmoja waliruhusiwa kupata leseni hiyo pale tu watakapopata ruhusa ya Waziri anayeshughulikia biashara ya kutolewa kwa leseni hiyo.

Madhumuni ya Mswada

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria ya Kusimamia utekelezaji wa mageuzi ya mfumo wa utoaji leseni za biashara yenye malengo yafuatayo:

1. Kuanzisha mfumo wa kitaasisi na kisheria utakaosimamia mageuzi ya utoaji leseni za biashara, vibali na ruhusa nyengine za kufaya biashara
2. Kusimamia utekelezaji wa magaeuzi yanayohitajika na kuhakikisha kuwa yanakuwa endelevu kwa kufanya mapitio ya mara kwa mara.
3. Kuratibu na kuelekeza mageuzi yanayohitajika kwa lengo la kuondosha aina zote za leseni, vibali au ruhusa maalumu za biashara zinazoathiri ustawi wa biashara.
4. Kusimamia na kuhakikisha kuwa leseni zote zitakazotolewa zitachunguzwa na kuidhinishwa kwanza na Baraza la kusimamia mageuzi hayo linalopendekezwa kuanzishwa katika Mswada wa Sheria hii.

5. Kuweka utaratibu na misingi ya wazi ya kutoa leseni, vibali au ruhusa maalumu ya kuendesha biashara.
6. Kusimamia utendaji na taratibu za mamlaka za utoaji leseni katika utekelezaji wa majukumu yao.

Muundo wa Mswada

Mhe. Spika, muundo wa Mswada wa sheria hii, umegawika katika sehemu kuu saba na vifungu 56. Sehemu hizo 7 pamoja na vifungu vyake zimejielekeza katika dhamira ya kuanzisha mageuzi ya mfumo wa utoaji leseni za biashara kwa kuweka chombo cha kusimamia mageuzi hayo ili kufikia malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mazingira ya biashara yatakayowavuta wafanyabiashara kuendesha biashara zao ndani ya mfumo wa kisheria na hivyo kuondoa sehemu kubwa ya wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao hivi sasa nje ya taratibu za kisheria.
2. Kupunguza gharama za usimamizi kwa wafanyabiashara na hivyo kuongeza tija ya biashara zao.
3. Kuiwezesha serikali kusimamia mwenendo wa biashara kwa gharama nafuu na pale ambapo ni muhimu kusimamia.
4. Kuiwezesha serikali kupanua wigo wa kodi na hivyo kuongeza mapato yake ya kuingiza sehemu kubwa ya wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao nje ya mfumo wa sheria.
5. Kuzingatia misingi ya usimamizi bora katika utoaji wa leseni za biashara.

Mhe. Spika, utayarishaji wa Mswada huu umezingatia pia maoni ya wahusika wengine pamoja na Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo. Maoni ya wadau hao pamoja na Kamati yamezingatiwa katika Mswada unaopendekezwa.

Muhtasari na Maudhui

Mhe. Spika, muhtasari na maudhui ya Mswada na uchambuzi wa ujumla kila sehemu ya Mswada unapendekezwa kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza
Sehemu hii inatoa tafsiri ya maneno mbali mbali yanayotumika katika rasimu hii.

Sehemu ya Pili
Sehemu hii inapendekeza kuanzishwa chombo, Baraza la kusimamia utekelezaji wa mageuzi ya mfumo wa utoaji leseni za biashara Zanzibar. Kubainisha kazi, mamlaka yake na uteuzi wa Wajumbe wa Baraza hili,

Sehemu ya Tatu
Sehemu hii inapendekeza kuanzishwa kwa chombo cha Utendaji kwa Baraza linalopendekezwa kufafanua kazi zake na wafanyakazi wake.

Sehemu na Nne
Sehemu hii inaweka misingi ya kusimamia Biashara na Utoaji leseni, kubainisha wajibu wa mamlaka za utoaji leseni na mamlaka ya serikali za mitaa kuhusu usimamizi wa biashara na utoaji leseni. Sehemu hii inaweka masharti ya kisheria kuhusu utaratibu wa kuzingatia maombi

utoaji na usitishaji wa leseni. Kadhalika sehemu hii inabainisha adhabu kwa makosa yatakayofanywa chini ya sheria hii.

Sehemu ya Sita
Sehemu hii inatoa maelezo ya vianzio vya fedha za Baraza, utayarishaji wa bajeti, uhasibu na ukaguzi wake.

Sehemu ya Saba
Mhe. Spika, inapendekeza kuwekwa masharti ya kisheria yatakayosimamia utoaji na utekelezaji wa maelekezo ya Waziri. Makosa yatakayofanywa na Makampuni chini ya sheria hii na uwezo wa Waziri kutunga kanuni kuhusu utekelezaji wa sheria hii.

Hitimisho

Kabla ya kuhitimisha maelezo ya hoja yangu hii naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa kuchambua mapendekezo ya awali ya Mswada huu kifungu kwa kifungu na kushauri maeneo muhimu ya kuimarisha Mswada huu. Kazi iliyofanywa na Kamati ilikuwa kubwa Mhe. Spika, na kuchukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa. Hii ilitokana na haja ya kuhakikisha kuwa Mswada unaowasilishwa unakidhi viwango vya ubora unaohitajika.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupokee Mswada unaopendekezwa, kuujadili na hatimaye kutungwa kwa sheria ya kusimamia mageuzi ya mfumo wa utoaji leseni za biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu kabisa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima, siha na nguvu zilizotufikisha hapa Barazani hadi tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga, hatuna budi kusema *Alhamdulilah*!

Mhe. Spika, shukurani zangu za dhati zije kwako kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako kutoa muhutasari wa maoni ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Mswada wa sheria ya kuanzisha sheria ya marekebisho ya usimamizi wa utoaji wa leseni za biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Kaimu Waziri wa biashara Viwanda na Masoko Mhe. Juma Duni Haji pamoja na Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko Mhe. Thuwaibah Kisasi na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao na Kamati wakati wote tulipokuwa tukichambuwa na kujadili mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, kuishirikisha jamii katika nia ya kufanikisha jambo lolote nchini ni jambo muhimu sana,tunawashukuru wadau wa sekta za biashara na sekta nyengine kwa kushirikiana nasi katika

kuuchambua na kuujadili mswada huu wa sheria. Maoni na mapendekezo yao yameweza kusaidia sana katika kuufanya mswada wa sheria kuwa bora.

Mhe. Spika, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa wajumbe wa kamati hii ya Fedha Biashara na Kilimo ya baraza la Wawakilishi, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuupitia na kuuchambua mswada huo.

Mhe. Spika, pamoja na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye kamati hii hadi kufanikisha kazi hii, naomba sasa niwataje kwa majina wajumbe hao wa Kamati kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Masoud Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed - Katibu

Mhe. Spika, Kamati yako ya Fedha Biashara na Kilimo ilipata wakati mgumu sana pale ilipokuwa tukiuujadili na kuupitia mswada huu kwa hatua ya awali, makosa mengi ya kimaandishi, tafsri isiyolingana na maana iliyokusudiwa ni baadhi ya mambo yaliyojitokeza sana katika rasimu ya mswada huu, jambo ambalo ilitulazimisha kuitaka Serikali iuchapishe upya mswada huu .

Mhe. Spika, tunaishauri Serikali kuwa makini wakati wanapoandaa rasimu ya sheria ili rasimu hiyo isiwe na kasoro nyingi sana kama zilivyoonekana katika rasimu hii, kufanya hivyo kutasaidia kupunguza muda wa kuchambua na kupitia mswada lakini vile vile kupunguza gharama za fedha zisizo za lazima.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwa muda mrefu sana Zanzibar imekuwa ni kitovu cha biashara katika Afrika ya Mashariki ambapo biashara za aina mbali mbali zimekuwa zinafanyika. Hata hivyo changamoto kubwa tuliyonayo ni kuwa kumekuwa hakuna mfumo mmoja uliomadhubuti na ambao unanguvu za kisheria wa utoaji wa leseni, vibali au ruhusa pamoja na usajili ya maeneno ya biashara.

Mhe. Spika, idadi halisi ya maduka yaliyopo hapa Zanzibar bado haijulikani jambo ambalo linatupa mashaka kuona kama kweli kodi za ada mbali mbali zinazopaswa kutolewa na wafanyabiashara hao zinapatikana ipasavyo. Maduka bubu ambayo yanaendeleza biashara zake tena kwa faida katika majumba mbali mbali mitaani pamoja na maeneo ya kufanya biashara ya wazi yanaendelea kufanya biashara hizo bila ya vibali au ruhusa. Haya yote yamekuwa yakifanyika kutokana na kukosekana kwa misingi na masharti ya jumla ya kisheria ya kuanzisha na kuendesha biashara.

Mhe. Spika, Sheria Nam 3 ya mwaka 1983 ndio inayosimamia utoaji wa leseni hata hivyo kuna sheria nyengine 68 ambazo pia zinasimamia kwa namna moja au nyengine mwenendo wa utoaji wa leseni za biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mfumo uliopo hivi sasa wa utoaji leseni umekuwa na athari kubwa katika biashara na uchumi kutokana na utitiri wa leseni na wingi wa vyombo vya utoaji wa leseni kama utafiti ulivyobainisha kuwepo kwa aina 243 za leseni za kuendeshea biashara ambazo zinatolewa kwa mujibu wa sheria zilizopo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, utafiti uliofanywa mwaka 2007 kuhusiana na mali na biashara ndogo ndogo hapa Zanzibar umeonesha kuwa karibu asilimia 97 ya biashara zinaendeshwa nje ya mfumo wa kisheria, kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo urasimu na taratibu ngumu za usajili wa biashara na upatikanaji wa leseni.

Mhe. Spika, vile vile utafiti huu umebaini kuwa kusajili biashara au kampuni huchukua muda mrefu ambapo ni siku 86 na ngazi 28 za kiutawala. Aidha ugumu wa kupiga tathmini ya malipo ya kodi ambapo imebainika kuchukua zaidi ya siku 300 na kupitia ngazi 76 za kiutawala na ugumu wa benki kuchukua mali zilizowekwa dhamana na wadeni wao wanaposhindwa kulipa mikopo waliochukua.
Mhe. Spika, kwa ujumla hali hii haikuweka mazingira rafiki kwa biashara pia imesababisha kuwepo kwa gharama kubwa za kuanzisha biashara na kuendeleza urasimu na kutovutia au kusaidia urasimishaji wa biashara.

Mhe. Spika, kutokana na udhaifu tuliokwisha kuueleza Serikali ilifanya utafiti ambapo ilibainika kuwa mfumo uliopo wa kisheria na usimamizi umepitwa na wakati kwa vile sheria hiyo haikuweka masharti ya kutosha ya kutumia leseni na kusimamia biashara. Aidha mfumo huo haukuzingatia mambo mengine muhimu ya kibiashara kama vile usalama wa bidhaa, afya na mazingira, kwa ujumla sheria iliyopo haikuweka mkazo katika suala la ukaguzi ambapo leseni ungetumika kama chombo muhimu cha usimamizi wa biashara.

Mhe. Spika, mfumo wa utoaji wa leseni uliopo hivi sasa umeshapitwa na wakati na hata kama mfumo huo ungeliwiyana na wakati usingeweza kutekelezeka kwa vile mfumo huo haujawahi kutekelezwa na kwa upande mwengine mfumo huo wa utoaji leseni, vibali na ruhusa haukidhi mazingira na mahitaji ya utoaji leseni, usajili na ufanyaji biashara hivyo sasa upo umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa sekta hii.

Mhe. Spika, sababu nyengine ni kuwa mfumo wa utoaji wa leseni za biashara na usimamizi wake uliathirika kutokana na mbadiliko ya kisera yaliyojitokeza katika miaka ya thamanini na ambayo kwa ujumla wake yalijielekeza zaidi katika kujenga uchumi kwa misingi ya nguvu za soko. Hivyo kutokana na kubadilika kwa mazingira hayo mapya kumesababisha kubadilika kwa mfumo na sheria za utoaji wa leseni za biashara.

Mhe. Spika, kamati yetu imeupitia mswada huu na kuujadili kwa kadiri ya uwezo wetu na kufanya marekebisho ya makosa ya kiuandishi pamoja na mabadiliko mengine madogo madogo. Katika Mswada huu wa leseni kunaanzishwa mfumo wa kitaasisi na kisheria utakaosimamia mageuzi ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara, vibali na ruhusa nyengine za kufanya

biashara, mfumo ambao utatoa haki ya kisheria kwa watu wote kuanzisha na kuendeleza biashara hapa nchini. Aidha kusimamia utekelezaji wa mageuzi yanayohitajika na kuhakikisha kuwa mageuzi hayo ya mfumo ni endelevu kwa kuyafanyia mapitio ya mara kwa mara.

Mhe. Spika, Mswada unatoa fursa ya kuhakikisha kuwa leseni zote zitakazotolewa zinachunguzwa na kuidhinishwa kwanza na Baraza la kusimamia mageuzi ya mfumo wa leseni kwa lengo la kuondosha kutofanana kwa masharti ya utoaji wa leseni. Aidha leseni vibali au ruhusa zitazingatia masuala muhimu ya afya, usafi, usalama, ubora wa bidhaa na mazingira na mambo mengine yanahusiana na uendeshaji mzuri wa biashara.

Mhe. Spika, mswada huu unalengo la kuondosha vipingamizi, urasimu na utaratibu mgumu wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni, vibali na ruhusa ambapo hapo awali ulichukua muda mrefu kusajili biashara au kampuni ambapo huchukua siku nyingi, hivyo mswada huu umekuja na suluhisho la tatizo hilo kwa kuweka kifungu kinachotaka ushughulikiwaji wa maombi usiozidi siku 30.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya mswada inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Baraza la utoaji wa leseni za biashara ambalo litakuwa na mamlaka kwa mujibu wa sheria kuweka masharti bora yanayohusu upatikanaji wa leseni, vibali au ruhusa. Aidha Baraza hili litajumuisha na Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima kuwa ni wajumbe wa Baraza. Jambo hili ni la kupongezwa sana kwani litaleta mashirikianao baina ya Serikali na sekta binafsi. Kamati imependekeza kuongezwa kwa idadi ya wajumbe kutoka jumuia ya wafanyabiashara, wenye viwanda na wakulima kufikia watatu ili kuwe na uwakilishi mpana kutoka sekta binafsi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 9 kinachozungumzia suala la muda wa uongozi kamati imependekeza kuongezwa maneno “kipindi kingine kimoja” ambapo kutakuwa na ukomo kuwa mjumbe wa Baraza. Jambo hili litaondosha ile tabia iliokuwepo hivi sasa ya mjumbe wa Bodi au mabaraza wa kuwepo kwa muda mrefu sana.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 10 ambacho kinaelezea vikao vya Baraza Kamati imependekeza kuwepo kwa Makamo mwenyekiti ili aweze kuendesha vikao vya Baraza pale inapotokea Mwenyekiti kuwa hayupo.

Mhe. Spika, katika sehemu ya nne ya mswada inayoelezea kanuni zinazosimamia utoaji wa leseni za biashara katika kifungu cha 24 (2) ambacho kinahusu ushughulikiwaji wa maombi na madai ambayo yamewasilishwa, Kamati imependekeza yashughulikiwe na yajibiwe ndani ya siku saba (7) badala ya siku thalathini (30) zilizopendekezwa katika mswada huu. Aidha kifungu cha 24(3) na 24 (4), 26 (2) vimefutwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yangu ya hapo juu nadhani nyote mtakubaliana na mimi kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuujadili na kuupitisha mswada huu bila ya pingamizi yeyote kwani ni mswada ambao tulikuwa tunauhitaji sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati yetu imerekebisha makosa mengi ya kiuadishi na imekubaliana na mapendekezo ya maswada huu na imeunga mkono mswada huu na tunawaomba Wajumbe wenzetu waujadili na wauchangie hatimae waukubali ili iwe ni sheria.

Hata hivyo, tunapenda kutoa indhari kwa wizara kuwa baada ya kutiwa saini kwa mswada huu tunawaomba waharakishe utungaji wa kanuni ili makusudio ya mswada huu yaweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja na niwaombe wenzangu waheshimiwa wajumbe waujadili kwa kina na baadae waukubali na waupitishe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Baada ya maoni ya Kamati ningekuomba kutumia Kanuni zetu basi nipate kidogo dakika mbili ili niweze kutoa mchango wangu katika mswada huu kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magomeni kuhusu Mswada huu, ni mswada muhimu kwa biashara, kama tunavyojua kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar ni wafanyabiashara iwe ni wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wale wadogo wadogo, ambao asilimia kubwa ya wafanyabiashara wadogo wadogo ni wale waliopo katika Jimbo langu la Magomeni. Kwanza Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwanza kwa kuona umuhimu wa kuandika mswada huu wa sheria unaosimamia masuala ya biashara.

Suala la biashara ni suala kubwa ambalo kwa ujumla ni sehemu ya uchumi ya watu hasa wale wafanyabiashara wadogo wadogo. Lakini pia hata kwa wafanyabiashara wakubwa ambao karibu asilimia yote mapato yanayotokana na mapato ya nchi yetu ambayo yanakusanywa na taasisi zetu hizi za kukusanya kodi yanatokana na wafanyabiashara. Na bila ya kuwa na wafanyabiashara mahiri wanaoweza kufanya biashara basi nchi yetu ingekuwa na ukosefu mkubwa sana wa mapato. Kwa hivyo, ni vyema kuanzisha sheria ambayo itaweza kutatua matatizo mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa ametueleza madhumuni na malengo ya mswada huu na naomba kidogo kunukuu Mhe. Waziri anasema "Mswada huu wa sheria umelenga kuanzisha chombo cha kusimamia utekelezaji wa mabadiliko ya mfumo wa utoajiwa leseni za biashara Zanzibar, ambacho chombo hiki kitaweka misingi imara ya kuendesha biashara na utaratibu thabiti wa utoaji wa leseni za biashara, jambo ambalo litasaidia kujenga uchumi kwa misingi ya nguvu za soko’’.

Mhe. Spika, madhumuni haya ni mazuri au malengo haya ya mswada huu ni mazuri. Lakini tumekuwa na tabia ya kutunga sheria, chombo chako hiki kimekuwa kikitungia sheria nyingi, masharti mazuri bora, lakini tatizo letu linakuwa katika utekelezaji wa sheria zenyewe hapo ndipo penye matatizo. Suala la chombo kimoja kusimamia utekelezaji wa masuala ya biashara ni muhimu na kwa sababu sasa hivi kinachoonekana kwamba kumekuwa na mamlaka nyingi za utoaji wa leseni, kila mmoja anaanzisha mamlaka, sheria zinakuja hapa tunapitisha sheria za kusimamia lakini imekuwa kama vile ni vurugu *match*, hakuna chombo kimoja kinachowasimamia. Haidhuru Wizara hii ya Biashara ndio inayosimamia masuala mazima ya biashara haya nchini kwa hivyo kila chombo kimekuwa kikitoa leseni, kila chombo kimekuwa kikitoa vibali. Imekuwa sasa leseni, vibali, ruhusa, ada, kila chombo kina-*create* namna ya kupata fedha wakati suala la leseni ni suala la kuratibu tu juu ya jambo lenyewe. Lakini hapa sisi imekuwa leseni ni kianzio cha mapato jambo ambalo kwa kweli si utaratibu mzuri.

Ruhusa, tunaweza tuka-*create* kwamba mtu hawezi kufanya hivi mpaka apewe ruhusa na wakati anapopewa ruhusa sio bure anatakiwa mtu yule alipe, atoe fedha ili apewe ile ruhusa. Mambo haya yamekuwa yakisababisha ugumu wa biashara hapa kwetu Zanzibar na kwa sababu kumekuwa na utitiri wa malipo, ulipe hapa, ulipe hapa hasa katika sekta ya utalii, unakwenda katika mfanyabiashara wa utalii anakata leseni yake ile ya gari lile la *private hire* kwa ajili ya kuchukua watalii, matokeo yake anapofanya kazi ile ya kuchukua watalii analazimika kila mtalii amkatie *permit*. Sasa mambo haya yanaongeza ugumu wa maisha ya watu wetu na biashara, hivyo Mhe. Spika, mimi naamini kuwepo kwa chombo hiki cha usimamizi wa utoaji wa leseni chombo kimoja kitaweza ku-*control* mambo haya na kuona kwamba wafanyabiashara wetu sasa hawapati usumbufu.

Kwanza suala la ruhusa ya kufanya jambo hili halitakiwi kutolewa fedha, kuwa na mabadiliko ya bei ya leseni kila wakati hili si jambo zuri kwa sababu si kianzio cha biashara, si kianzio cha kodi. Lakini ZRB kama Taasisi ya Kukusanya Kodi isiruhusiwe kutoa leseni, leo utashangaa kwamba ZRB nayo inatoa leseni wakati ZRB kazi yake ni kukusanya kodi. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naamini kuanzishwa kwa chombo hiki cha kusimamia leseni pamoja na masharti mblai mbali ambayo yapo kwa mujibu wa sheria hizi na kama uadilifu na usimamizi mzuri utakuwepo naamini mambo haya yanaweza yakatusaidia katika kuona kwamba biashara zetu zinakwenda vizuri, wananchi wetu, wafanyabiashara wetu wanaondosha malalamiko ya hapa na pale, lakini zile fedha au kodi zile zinazohitajika zitalipwa na uchumi unaotokana na biashara basi utaweza kukua.

Kwa hivyo Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mimi niunge mkono tena kwa mara nyengine kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni kwamba mwada huu na wenzangu tuujadili hatimae uweze kuwa sheria.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ninashukuru sana na mimi kupata nafasi hii asubuhi ya leo lakini Mheshimiwa katika mchango wangu tofauti na wenzangu kwa sababu kila mtu huwa na fikra zake na mawazo yake.

Mhe. Spika, mimi naanza kusema kuwa mswada huu mimi siuungi mkono kabisa na sababu ninazo za kusema kuwa siiungi mkono. Mhe. Spika, mswada huu umekuja wakati wananchi washaumia kwa asilimia kubwa sana na mswada mzuri sana una mantiki nzuri lakini *time* siyo Mhe. Spika, tumechelewa sana. Tunaleta mswada huu wananchi wetu wameshapoteza nguvu zao, wameshapoteza haki zao. Sasa tunauleta leo Mheshimiwa faida yake siioni mimi niseme niunge mkono na nikisema nikiunga mkono Mhe. Spika, nitawasaliti wananchi na mimi wananchi wananipenda sana Mhe. Spika, kwa kuwatetea haki zao halafu leo niseme niunge mkono. Mheshimiwa hili suala hapo linanitia majonzi makubwa sana.

Mhe. Spika, tuna mambo mengi wenzetu wanatembea Mhe. Hamza ametembea nchi mbali mbali, lakini nchi ya Zanzibar ni mfano ambao mimi sijapata kuuona katika ulimwengu huu, unakodi mpaka vichochoroni, maana yake ina kodi nyingi sana. Kwa kweli hata wafanyabiashara wetu wameshindwa kukaa hapa Zanzibar wamekwenda kutafuta biashara nyengine kwa ndugu zetu, kutokana na kodi zilivyokuwa nyingi, kutokana na leseni Mheshimiwa kuwa nyingi sana.

Sasa ndio maana nikasema kuwa mswada huu umekuja wakati sio, wafanyabiashara wameshatukimbia sasa hivi tunamuundia nani Mhe. Spika, wafanyabiashara waliobakia ni wachache tunawaona kila leo hao hao tu. Sasa mimi naomba Mheshimiwa ningemuomba sana si vibaya hata tukarudi nao mswada huu.

Leo Mheshimiwa nitoe mfano, tuna wafanyabiashara waliokuwa wanafanya biashara nzuri sana ya gari kupeleka Tanzania Bara lakini kwa kuwa hakuna usimamizi mzuri, mimi nilifikiria mswada huu utakuja tusimamie masuala ya biashara mimi ningeunga mkono asilimia lakini bado tunauleta mswada huu kwa kusimamia leseni hatutafuti mbinu za kusimamia biashara zetu, zimeanguka kabisa, hapa mimi ndipo ninapopata mashaka Mshika Spika. Biashara zimeshatutoka Zanzibar na tulikuwa na soko kubwa sana hapa Zanzibar hakuna asiyejua, kila mtu akifanya kazi mahoteli, vijana wakifunga mizigo kwa mizigo pale, wabeba rikwama, halikadhalika na watu wengine, vyombo vyetu hivyo vya baharini na mambo mengine Mheshimiwa.

Lakini leo tumepoteza Mheshimiwa, tumepoteza kwa kuwa labda tulikuwa hatuna chombo hicho na ndio sababu yenyewe ya kuona jinsi gani wenzetu wafanyabiashara wanaondoka hatujajiuliza suala hilo, sababu gani wafanyabiashara sasa hivi wanaondoka wanakwenda katika sehemu kufanya biashara zao tena wanatajirika kabisa hatujakaa tukajiuliza. Lakini sasa ndio tunajiuliza kumbe tumejiuliza suala ambalo kuwa tuna leseni nyingi sana hakukuwa na chombo cha usimamizi, sasa uone kasoro hizo Mhe. Spika, kwa kweli suala linasikitisha sana. Tumejifanyia *correction* kwa kweli kulikuwa na tatizo na kutokusimamia, Mhe. Spika, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana, mimi ninasikitika sana. Mheshimiwa sasa hivi biashara ambazo zile za kufanywa na mzawa hapa lakini kwa kuwa hakuna chombo cha kusimamia anafanya mtu wa kigeni. Mheshimiwa utakuta mzungu anauza tungule leo! Wakati mzawa ana uwezo wa kuuza tungule, ni suala la kuchekesha.

Mheshimiwa sasa wazungu wanafanya hizi *restaurant* za chakula *local food* wakati mwananchi mzaa anaweza kufanya biashara ile. Lakini utakuta leo biashara ile hapewi mswahili anapewa mzungu na hakuna chombo cha kudhibiti mambo hayo. Mhe. Spika, kuna jambo alisema Mwenyekiti wangu hapa kidogo nitamuunga mkono suala la wenzetu wa *private hire.* Sasa hivi hawa biashara inawashinda kutokana na mambo ya kodi nyingi sana wanaekewa leseni nyingi, ni suala ambalo la kusikitisha mpaka siku hizi unaambiwa kuna sheria nyengine zimetungwa za maajabu ajabu, wawe na *fire extinguisher,* waweze kuwalipia wageni afya, wawe na viboksi vya tools, Mhe. Spika, yeye mtu *driver* unakwenda kumwambia masuala ya afya anajuaje, *alimradi* mnawawekea mipango biashara wafanye watu wakubwa wale wadogo wasifanye biashara ndio maana yake. Au unamwambia mtu lazima aweze kuwa na Kampuni ya *Tourist* ana uwezo gani yule.

Haya ni mambo ambayo Mheshimiwa ilipaswa tukae tulete sheria ya kuwasaidia wafanyabiara, lakini tunaleta sheria ya kulinda leseni. Kwa kweli hili suala bado linasikitisha sana. Gari sasa hivi watu wanazipanga kwenye mabanda haziwezi kufanyakazi sheria ni nyingi kabisa. Jamani Mhe. Spika, mimi ningeomba kitu kimoja, fikra zangu zinanambia hivi, kifungu hapa ukurasa wa 258 kinasema hivi naomba ninukuu kwa heshima yako Mhe. Spika, kifungu 2 mabano.

"Serikali itaingilia kati masuala ya biashara ya upatikanaji leseni, vibali na ruhusa isipokuwa kama shughuli hizo za kibiashara zitapelekea kusababishwa kuhatarisha maslahi ya umma, kuhatarisha usalama wa nchi, kuvunja wajibu wa kimataifa, kukiuka masharti''. Mhe. Spika, karibuni nilikuwa mkali sana hapa watu wamepewa leseni wameleta vyakula vibaya sana Mheshimiwa, tena vibaya mwenyewe hapa naomba sana Mheshimiwa lisipigwe buti nitatoa mfano lakini mzuri tu, Mheshimiwa wangu swahiba wangu ananitizama sana Mhe. Mohammed Aboud naomba sana nisipigiwe buti.

Mheshimiwa ubaya wake sasa wafanyabiashara vile vitu vikiwa vibaya wanawapa wakubwa wakawape wananchi. Nilileta mchele hapa mimi unanuka, nilileta unga hapa unanuka. Sasa ndio maana nikasema kazi yetu ni kutunga sheria lakini hazifanyi kazi. Mhe. Spika, kuna unga mbovu sana na mpaka leo watu wanautumia ndio maana nikasema siungi mkono. Sasa naingia katika maudhui yenyewe ya kukwambia nini maana ya kutokuwa siungi mkono.

Mheshimiwa biashara hii inaendelea inazidi kukua na huko nyuma sheria zilikuwepo kabisa lakini watu waliachiwa, sijui watu wana ajenda gani leo maradhi chungunzima, maradhi ya sukari yamejaa, mapresha yamejaa, watu kila aina kwa vyakula hivi. Sasa Mhe. Spika, ndio maana nikasema sitounga mkono kwa sababu sheria hizi huko nyuma tulikuwa tunazo na leseni tumezitoa kwa makusudi hakuna hata mmoja aliyenyan'ganywa leseni. Mtu *exibity* anayo mkononi na mtu hajafungiwa leseni halafu mimi nikaunge mkono, aa wananchi watanilani, sikubaliani nao siungi mkono Mheshimiwa kwa hili.

Lakini vile vile Mhe. Spika, la kusikitisha ndio maana nikasema hatusimamii biashara zetu. Kuna mtu kapeleka Bara gari yake ndogo ya kutembelea mwenyewe alipokwenda kule Bara alitozwa kodi sawa sawa na zike alizolipa hapa, biashara hiyo iko wapi Mheshimiwa. *Wallahi* leo tunakwenda kwa kuwa Zanzibar hapa Mwenyezi Mungu yupo, maneno ya Wachina waliokuja wakaona kuku mmoja kapewa shilingi 20,000/= akashukuru yule mchina *wallahi*, kashukuru kwa hili, hajui lakini kashukuru tu akasema kweli Zanzibar Mungu yupo, kwa kuku 20,000/= akamkisia yule mtu mkaazi wa Zanzibar mshahara wake mdogo na kwa leo kuku yule ana uwezo wa kumla, aliliamini hilo suala.

Sasa Mheshimiwa hili suala ambalo kwa kweli linasikitisha sana naomba tena Mhe. Waziri njoo tuletee sheria ya kulinda biashara sasa tujiulize biashara zetu kwa nini zimekwenda chini. Tusijidanganye biashara Zanzibar hakuna sasa hivi, biashara sasa tunakwenda Bara kuchukua, tunaleta huku na ilikuwa zamani wenzetu wanakuja kuchukua huku wanapeleka kule. Mimi nafikiri Mhe. Spika, hiyo ndio ilikuwa mantiki kubwa ya kuleta mswada hapa kuweza kulinda suala hilo, lakini mpaka leo bado hatujajiuliza tu halafu leo mimi niunge mkono wananchi wa Kitope watanipiga.

Mheshimiwa kwa kumalizia ni kweli sasa hivi kodi zimekuwa kubwa sana, kodi zimekuwa nyingi hajulikani nani mwenyewe, hajulikani baba wala mama Mhe. Spika, utasikia ZRB sijui nani kila pahala wanatozwa kodi kwa nini? Mimi natoa ushauri wangu kwa nini tusiitafutie serikali vianzio vyengingine vya mapato vikaweza ku-*recover* ili zile kodi nyengine zikaachiwa wananchi wakaendelea na biashara zao wasitozwe kodi ni wazo zuri sana turuhusu, nikisema jambo mnakuwa mnanitafsiri vibaya. Sasa hivi tuna rasimu hiyo hebu sasa hivi tuing'ang'anie hiyo ituruhusu tuweze kuweka viwanda vikubwa leseni tuwe nazo wenyewe. Lakini tunasema

hapa kuwa ruhusa tunayo ya kutoa leseni lakini viwanda vikubwa hatuna leseni, tusidanganyane hatuna uwezo wa kisheria kwa mujibu wa hii katiba yetu tuliyokuwa tunayo hivi sasa mpaka tufanye marekebisho ndio tutakuwa na uwezo huo. Kwa hivyo mimi naomba sana kuwa serikali itafute vianzio vikubwa sana ili hizi kodi ndogo ndogo ziwaachie wananchi waendelee kufanya biashara yao ili waweze kuleta tija nzuri, kuondoa umaskini na kuleta utajiri. *Otherwise* sote wazanzibari tutakuwa maskini kabisa, tutaleta kila sheria, tutamuhangaisha mwanasheria akili lakini hatimae itaishia kwenye briefcase.

Mhe. Spika, niliona mimi leo nitoe maoni hayo kwa uchungu kabisa kuona jinsi gani hizi sheria tunazozileta hapa hatuziangalii mantiki yake, zaidi tunakuwa tunaleta hapa na kupitisha. Mimi nafsi yangu nasema Mheshimiwa pamoja na wananchi wa Jimbo la Kitope mswada huu mimi siungi mkono kwa sababu *time* imeshatupita kabisa. Leo tunamuundia sheria hii wakati huko nyuma tumeshawapa kasoro nyingi tumeshawakwaruza, mimi sitounga mkono. Mhe. Spika, Ahsante sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, kwanza sina budi kuweza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutupa pumzi hizi sote sisi wajawake kwa kufika katika Baraza lako hili na kutupa nguvu za kuweza kuchangia michango mbali mbali kwa maslahi ya wazanzibari.

Mhe. Spika, labda niseme kwamba katika kipindi changu kifupi ambacho wananchi wa Jimbo la Uzini walionileta humu ndani inanipa tabu kidogo katika masuala yote ambayo humu ndani kwenye Baraza letu la kutunga sheria na tukaweza kufanya mambo mengi sana. Lakini Mhe. Spika, nime-*experience* na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba haya tunayoyazungumza Wawakilishi katika Baraza hili tukufu *record* zake zipo za miaka na zitakaa kwa miaka. Lakini nataka niseme, jamani haya mambo tunayokwenda nayo na tunayoyapitisha, tukampelekea Rais atie saini ili mswada huo uwe sheria lakini Mhe. Spika, nia ipo kwa sisi watendaji na viongozi la kwanza. Kwa sababu Mhe. Spika, mambo mengi haya tulikuwa tunayazungumza na viongozi wa Serikali, mawaziri wahusika na Wizara zao walikuwa wanatupa kauli ndani ya Baraza hili, kauli ambayo ndio kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, humu ndani sote wawakilishi tumo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, humu ndani hatuko wapinzani.

Sasa Mhe. Spika, suala hili la biashara ukisema biashara maana yake ni uchumi, kutokuwa na uchumi imara nchi yoyote duniani Mhe. Spika, basi siku zote tutakuwa tunayumba. Uchumi wetu kuwa imara Zanzibar ni kujitegemea wenyewe kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunavyokwenda. Na kwa ufahamu wangu Mhe. Spika, kuna vitu vinajitokeza kuwapa mzigo wafanyabiashara, wakulima, wafugaji na wananchi ambao wanajitegemea riziki zao katika maisha yao tunakuwa tunawapa mzigo ambao sisi humu ndani tuna *mas-ul* kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa mfano Mheshimiwa, mimi ninashukuru sitaki nirejee *issue* ya jana *alhamdulillahi* tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kweli ndio maana ukakuta Wizara inayohusika jana iliteremka kilima, tulifurahi sote kwa msimamo na juhudi ya watendaji wetu kuwa wakweli katika suala na hasa lile la Kisiwa cha Fungumbaraka. Leo Mhe. Spika, miezi miwili tu iliyopita tulikutana humu humu na nnamuomba Mwenyezi Mungu akupe umri mrefu

Mhe. Spika, uendelee. Tulikutana humu humu na wewe ukatuongoza na *hansard* ipo jawabu ipo na ningelimuomba Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara Mzee wangu Juma Duni ili atapokuja hapa ningelimuomba akachukua ile *hansard* iliyokuwepo juu ili atupe maneno kama tuliyopata jana ili tushibe. Sasa Mhe. Spika, miezi miwili iliyopita ilikuwa Agosti, tulisema hapa ndani kuwa kuna kodi ya simu ambayo imekuwa *implemented* na wenzetu Bara shilingi elfu kwa wananchi wote ikiwemo Zanzibar kuanzia Micheweni, Kizimkazi, Nungwi, Uzini sehemu zote hizo tukauliza suala hili. Pesa hizi wenzetu Bara walikuwa na mapungufu kama sikosei *Astaghafirullah, over 40 billions*, sasa wakaona njia moja ya kufidia barabara zao za Tanganyika sio za Tanzania za Tanganyika, wakaona watoze shilingi elfu moja ili wafidie barabara zao.

Mhe. Spika, *Wallahi* jambo hili linahuzunisha sana kwa sababu sote humu tumekuja kwa maslahi ya wananchi. Jambo la kusikitisha Mhe. Spika, baada ya kutoa taarifa hii sisi kodi hii ya shilingi elfu inawagusa wananchi wa rika zote, mimi angalau mfanyabiashara nitasema naziweza shilingi elfu moja lakini kuna mwenzetu mkulima pengine hizo shilingi elfu moja ndio anatumia simu yake kwa mwezi. Mawaziri wanaohusika, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Fedha alitupa hapa, alitwambia Zanzibar hatukushirikishwa, Zanzibar hatujui Mheshimiwa, *hansard* ipo juu na wala haitekelezeki mpaka watu wakae. Kwa hivyo, Zanzibar hili halitogusa la shilingi elfu.

Mhe. Spika, wenzetu Bara wameli- *implement* hilo wananchi wameanza kukatwa shilingi elfu *are we serious?* Kwa sababu Mhe. Spika, tunachoomba hili ni Baraza na rekodi inabakia, kama tumekuja hapa tupige gitaa basi hakuna tatizo, lakini tunafika kwenye Baraza lako unatuongoza wewe na waziri anatoa kauli kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar halafu wenzetu huko Bara magazeti yakatoka kwamba waziri mhusika kule mwisho wake Chumbe anakuja kutoa amri ya mambo yetu ya Zanzibar ruhusa hii kampa nani na hili ni Baraza la kutunga sheria.

Mhe. Spika, mimi nashukuru makampuni mengine yameshakwenda Mahkamani, lakini bado Mhe. Spika, ningeliomba Mhe. Waziri mhusika atupe muongozo kama uliyotoka jana ili suala hili lisitishwe lifike mwisho Chumbe. Namuomba sana Mhe. Waziri, naomba tusitafune maneno tuwe wakweli na tumekuja hapa kuwatetea wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba Mhe. Spika, akapata hilo tamko lililotolewa ndani ya Baraza miezi miwili iliyopita ili tujinasue na kama kuna pesa zile zimekatwa basi zirejeshwe mara moja Zanzibar ili zitumike katika suala letu la barabara, madawa, afya na elimu hizo zilizokuwa zimeshaanza kukatwa. Mhe. Spika, ndio maana siku zote nasema hakuna mtu anayekataa udugu, hakuna mtu anayekataa umoja, lakini udugu wetu na umoja umetokana na historia. Kwa hivyo, ninachotaka Mhe. Spika, hili liweko.

Lakini vile vile Mhe. Spika, mimi naunga mkono mswada huu uliotolewa pamoja na mwenyekiti mhusika mkuu, naunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini na kuunga mkono kwangu ningeliomba taasisi hii ya biashara ambayo ndio Mwenyezi Mungu akitujaalia ikipita Rais anakwenda kutia saini, kuweko na utekelezaji wa dhati.

Mhe. Spika, mwaka uliopita na mwaka huu uchumi na biashara, hizi gari za mchanga wanazotumia ndugu zetu kwa kupata riziki zao, haya magari yetu mengine ya walalahoi wanozitumia **P 38**, kwa taarifa Mhe. Spika, mpaka leo vitu ambavyo vinawagusa wananchi walio chini maana yake kuna magari yetu haya *ling long tire*. Mhe. Spika, hapo nje Mwenyezi Mungu

katujaalia sote kwa sababu tuko bondeni tumejipangia maprado kwa sababu tushafika huko na hakuna mmoja *tire* ile anayeitumia. *Tire* zile za *ling long* zinatumika kwa gari za makokoto na mchanga.

Mhe. Spika, nasema hata katika Muungano wetu biashara haipo ndani ya Muungano. Mhe. Spika, mpaka jana ukienda nje huko kote ukitaka tairi kama hili China wanazalisha hili *ling long*, Uingereza wanazalisha **P 38** anakwambia bwana hili limesajiliwa kuna *agent* Tanzania. Mheshimiwa mimi mwenyewe nimekwenda na niruhusu Baraza liende na Wajumbe wakashuhudie hio hali halisi ambayo Zanzibar tunanyimwa uhuru na fursa yetu. Niko tayari kutoa gharama zangu Mhe. Spika, ikithibitishwa nilipwe, isipothibitishwa niko tayari kula hasara hata tiketi tano sehemu yoyote ile, matokeo yake Mheshimiwa tairi zile wanaofaidika ni Watanganyika wanasema *agent* Tanzania sisi tukienda Wazanzibari tairi lile ambalo tunatumia kwa watu wetu mpaka leo nimezungumza mpaka kwenye kikao cha *partnership* pale Bwawani ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametuongoza.

Mhe. Spika, wanasiasa au viongozi lazima tuwe wakweli, lakini tukiwa tunaogopa tutafika kuiumiza Zanzibar. Sasa mambo mengi kwa kweli ni *shaghala baghla* tu Mheshimiwa, tunakuja hapa tunaamua, tunazungumza matokeo yake hamna *implementation*, mambo hayendi kwa sababu tu binadamu anaona mimi nitaondoka hapa Mheshimiwa sote tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala la biashara hili ndio uti wa mgongo wa Wazanzibari, ninachotaka kuomba fursa za Zanzibar za biashara kama *ling lon na* **P 38** ziruhusiwe Zanzibar. Kama tunataka kupeleka Bara basi kama kuna tofauti au nini tutakwenda kutekeleza, lakini haiwezekani vitu vinataka kuja Zanzibar kama leo mipira ya China kwa taarifa Mhe. Spika na Wawakilishi wote mipira ile inabidi tununue China, tulete Dubai ni gharama halafu Dubai tupakie kwenye meli ndio ije Zanzibar. Sasa wale wauza mchanga na kokoto tunawauzia mara mbili zile tairi. Kwa hivyo, yule anayetaka kujiwezesha kujenga nyumba yake anagharamika kwa mambo ambayo hayana ulazima.

Halafu Mhe. Spika, hata mabalozi hawajatusaidia bado kwa sababu haya mambo yako wazi, hivyo serikali sio leo tu hata hiyo *partnership* ya Bwawani Katibu Mkuu Kiongozi alikuwepo pale alikuwa anatuongoza hakuna *implimentation* yoyote. Sasa Mheshimiwa tusiwe tunakuja hapa tunapitisha miswada halafu inakwenda kufungiwa kwenye kabati, inakaa miaka mitatu ikitaka kuchukuliwa ikunutwe hivi halafu iletwe tena tuanze kuzungumza. Mhe. Spika, mimi ninachozungumza ni maslahi ya wananchi, kuna biashara nyingi wenzetu waone hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, wafanyabiashara alizungumza Mhe. Waziri wa Afya, Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kuhusu benki. Mhe. Spika, Wazanzibari mimi nataka nikuhakikishie tunaweza kuwa na uchumi imara kama tutakuwa na utekelezaji wa pamoja, kama tutakaa pamoja. Kwa mfano Mhe. Spika, kwani benki ndio inayoendesha uchumi na inaendeshwa na wafanyabiashara leo tukiwa na mtandao mzuri tukiwaambia Wazanzibari walioko nje kwamba bwana, tuna benki tutatoa posho maalumu. Kwa mfano benki leo kuna *interest* ya 4% tutatoa 5% *interest*, Mheshimiwa nataka nikuhakikishie Wazanzibari walioko huko wakileta Dola elfu elfu tu au elfu kumi kumi Zanzibar tutakuwa na *Surplus* katika *reserve* zetu na kuendesha uchumi wetu imara, ndivyo wanavyofanya wenzetu nje pesa za benki ndizo zinazoendesha miradi hata huko Dar es Salaam pesa za benki ndizo zinazoendesha miradi, lakini kila mmoja

ana hofu kwa sababu ya utekelezaji, ikiwa vitu hivi vinazungumzika havitekelezwi tukienda tukirudi lazima Mhehsimiwa tukae ili kuona jinsi gani tunaweza kusaidia.

Mhe. Spika, hivi unavyoviona sehemu zote za Dubai, Hong Kong, China, Marekani, Uingereza hata hapo kwa wenzetu Tanzania Bara zinaendeshwa na taasisi za fedha. Kwa sababu Mhe. Spika, ukishakuweka *reserve* wananchi wana imani kutokana na muundo wetu huu zile benki ndizo zinazokwenda kuanzisha miradi mbali mbali.

Kuna wafanyabiashara wanaweza kupata posho nzuri wakaweka kwa miaka mitatu au minne una saini nao na hicho kinafanyika Mheshimiwa, unasaini mika minne unaweka dola yako laki moja huyu anaweka shilingi 50 elfu. Kwa hivyo, ile miaka minne posho unayompa yeye karidhika, pesa zile unaweza kuendesha uchumi imara ukapata taasisi, wafanyakazi, wananchi wakaajiriwa na maisha ya Wazanzibari ikaendelea vizuri lakini na haya yote Mhe. Spika, yanataka tubadilike sisi, tukibadilika vitu hivi vitakuja.

Sasa Mhe. Spika, kwa kumalizia bado tunawajibika sote katika biashara, kwa kweli wafanyabishara tunapaswa tuwasaidie na nataka nikuhakikishie naomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa nia nzuri kabisa wawatizame hawa wenzetu waliokuwa hali zao ziko chini.

Mhe. Spika, mimi sijisifu lakini mimi hapa nilipo nimetoka kwenye umasikini mkubwa sana, wazee wangu walikuwa wakichunga punda mimi nikila mapera, lakini siku zote namuomba Mwenyezi Mungu nitatoa mfano. Mhe. Spika, mimi sina taasisi lakini nimeshakwenda marikiti kwenye samaki, wauza mboga, wauza pilipili haja zao shilingi laki mbili mbili tu tena wanakurejeshera baadae Mhe. Spika, wale ndio watu wa kuwasaidia. Mimi Mheshimiwa nimeshafanya hivyo, sitakiwi niseme kwa Mwenyezi Mungu lakini kwa nini serikali yetu Wizara ya Biashara haisimamii hawa watu tukawaelimisha tukawapa *incentive*, muuza mboga bwana kaa nazo shilingi laki mbili hizi miezi sita ukitangulia mbele ya haki nakusamehe, nikitangulia mimi mbele ya haki utanilipa hiyo ndio njia ya kusaidiana Mhe. Spika. Hilo lipo, mimi nimefanya hivyo na naendelea kufanya kawaulizeni kule kote marikiti, Malindi sehemu zote Unguja Nzima.

Nikitangulia Mhe. Spika, mimi nawaambia mtakuja kumlipa mwanangu kwa sababu ukitangulia wewe nitakudai nini hahe hohe. Sasa Mhe. Spika, mimi nafikiri tungekuja huku kuwasaidia wananchi kwa sababu sote Mhe. Spika, sote Wawakilishi tumetoka huko, lakini leo tumekuwa na ma-prado hapa ya Shilingi milioni mia moja tunasahau kabisa kwamba tuko bondeni tunawasahau kabisa masikini. Kwa hivyo ninachoomba kwa Mawaziri vile vile nawaombeni sana mnapotoa kauli halafu kunakuwa na *implication* nyengine au utaratibu mwengine kwa kweli mnatuhuzunisha.

Mhe. Rais,Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hawa ndio wasimamizi wa sisi kuliongoza Taifa hili, lakini tukikaa tukisema umimi umimi hatufiki katika kuimarisha uchumi wetu na kuwashughulikia wananchi wetu wa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, mimi ninaomba sana na naunga mkono asilimia mia moja ya mswada huu lakini nakwambieni mna dhima kwa Mwenyezi Mungu mjue mnachukua hiyo lakini vile vile namuomba Mhe. Waziri atupe tamko hapa ambalo limetoka kwenye Baraza kuhusu hii shilingi elfu kwamba liwe mwisho Chumbe ili

tukae tuone na zile pesa zilizokusanywa ngapi, ili wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba tupate imani na sisi kwamba kweli serikali yetu imejiandaa vya kutosha. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kutuwezesha kusimama hapa katika ukumbi ya kujadili Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni. Pili nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Lakini vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu ambao madhumuni hasa ya mswada huu imesema ni kuwasaidia wafanyabiashara lakini kubwa zaidi ni kusaidia kuinua uchumi wa Zanzibar. Mhe. Spika, ikiwa uchumi wa Zanzibar utanyanyuka kwa kweli hali ya umasikini itapungua.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia naomba nieleze masikitiko yangu kidogo,

kifungu cha 79(2) cha Kanuni kinasema kwamba:

> *"Tangazo la kwanza la Mswada wa Serikali litatokea kukiwepo angalau siku ishirini na moja kabla ya Mswada huo kusomwa kwenye Baraza kwa mara ya kwanza…."*.

Mhe. Spika, huu mswada tumepewa siku nyingi lakini jana tumepewa mswada mwengine. Kwa sababu kwa marekebisho yaliyofanywa mimi nahesabu ni mswada mwengine kwa sababu kama ni marekebisho madogo usingelichapishwa upya huu. Sasa nadhani hapa kidogo pana usumbufu kwa sababu mimi najiuliza niuchangie ule mswada ambao nimepewa mwanzo nikausoma au niuchangie mswada niliopewa jana jioni? Sasa Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo.

Vile vile Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa marekebisho aliyoyafanya. Kwa sababu katika ule mswada wa mwanzo kuna vifungu mimi nilikuwa nikisoma naviwekea mkono nisivione hasa pale ilipoletwa tafsiri ya nchi za nje. Kwa sababu Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha mwanzo kinasema kwamba Zanzibar ni nchi na pale ilionesha kwamba Zanzibar imetolewa katika kuwa ni nchi. Sasa mimi Mhe. Spika, nilisikitika sana kwa sababu niliona Mhe. Waziri anatupeleka kule kwa Mhe. Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyesema kwamba Zanzibar si nchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati kwa kufanya marekebisho haya.

La pili Mhe. Spika, katika marekebisho aliyoyafanya Mwenyekiti wa Kamati kulikuwa kuna neno lilitumiwa pale, nimelisahau kidogo lakini ni neno la Kiingereza. Sasa kwa mujibu wa kanuni Mhe. Spika, inasema kwamba Mswada wa Sheria uletwe katika lugha ya Kiswahili, kwa hivyo pale Mhe. Waziri hakuwatendea haki wananchi kwa sababu wako waliokuwa hawalijui neno lile na wangelilitumia vibaya na wakatiwa hatiani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa pia nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa kuliona hilo na wakafanya marekebisho. Sasa Mhe. Spika, naomba nianze kuchangia huu mswada kwa vile ambavyo nitajaaliwa, kwa sababu mswada umetolewa jioni na leo unatakiwa kuchangiwa hapa.

Mhe. Spika, naomba nianze katika ukurasa wa 248 wa Gazeti Rasmi la Serikali pale palipoeleza Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni. Sasa hapa

Mhe. Spika, mimi nina swali kidogo, nataka kujua hii sheria ni mpya inayoanzisha Usimamizi wa Utoaji wa leseni au ni sheria kongwe inayorekebisha Usimamizi wa Utoaji wa Leseni? Nasema hivi kwa sababu hapa pametajwa mambo mawili kwa pamoja, pametajwa kuanzisha ambapo huwa ni sheria inayoanzishwa sasa na vile vile pametajwa marekebisho jambo ambalo huwa ni sheria ipo na inafanyiwa marekebisho na mara nyingi sheria tukiletewa ikiwa ni za marekebisho huwa tunaambiwa kama ni Mswada wa Sheria ya Kurekebisha na ikiwa ni mpya unaanzishwa sasa huwa tunaambiwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri kidogo aniambie hii sheria inaanzishwa sasa au ipo inafanyiwa marekebisho.

Lakini pia Mhe. Spika, katika ukurasa wa 253 kifungu cha 8(1)(a) na (b), mimi Mhe. Spika, naona hivi havifahamiki vizuri, ningelimshauri Mhe. Waziri akavichanganya na akataja Mwenyekiti atakavyopatikana na sifa zake. Kwa mfano, angelisema Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais atafaa kuteuliwa na kuwa Mwenyekiti atakapokuwa na elimu inayoanzia shahada ya kwanza ya uchumi, uongozi wa uhandisi au sheria na uzoefu wa miaka saba ya fani hizo. Mhe. Spika, nadhani hapa ingelifahamika zaidi kuliko vile ilivyo.

Vile vile Mhe. Spika, katika kifungu cha 8(c) ukurasa wa 253 pametajwa taasisi ambazo waziri atawachagua Wajumbe wa Baraza la Leseni. Mhe. Spika, hapa pia nina maswali namuomba Mhe. Waziri anisaidie. Je, kwa nini wajumbe hawa wakatoka kwenye taasisi hizi tu? Je, hakuna taasisi ambazo zinatoa leseni na hazikuwakilishwa katika Baraza hili? Ikiwa zipo hizi taasisi zitasemewa na nani katika Baraza hili?

Mhe. Spika, pia katika kifungu cha 10(3) ukurasa wa 254 kinahusiana na *quorum* ya kikao kuwa ni nusu tu ya wajumbe. Mimi Mhe. Spika, hili silikubali na silikubali kwa sababu mbili, kwanza Mhe. Spika, Baraza hili linashughulikia shughuli muhimu za biashara ambapo ndio muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar hivyo umakini unahitajika. La pili, katika wajumbe 11 ambao kwa mswada huu tuliopewa unasema hivyo, wa mwanzo ilikuwa ni wajumbe tisa ambao ndio wanaounda Baraza hili kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) ukurasa wa 253. Mhe. Spika, waziri anawadhibiti wajumbe saba ambao ni mjumbe mwenye dhamana ya biashara ambaye mjumbe huyu anatoka katika wizara ya Mhe. Waziri na wajumbe watatu wanaotoka katika Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima ambao Mhe. Spika, wajumbe hawa Mhe. Waziri ana ukaribu nao mno, kwa sababu yeye mwenyewe anatoka katika wafanyabiashara.

Vile vile kifungu cha 8(1)(d) waziri kapewa uwezo wa kuchagua wajumbe watatu. Sasa Mhe. Spika, wajumbe saba kati ya wajumbe 11 ni wale wanaomtii Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa maana hiyo, ikiwa *quorum* itakuwa ni nusu basi vikao vyote vitakuwa ni *rubber stamp* ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, leo hii ni jambo la kujivunia kuwa tuna waziri makini, muaminifu na muadilifu, lakini katika serikali hii inaweza kuja kutokezea siku moja tu tukawa na waziri wa ajabu ajabu na Baraza la Leseni ndio keshalidhibiti. Sasa Mhe. Spika, hapa hawa wanaweza wakaja wakapitisha ukorofi wa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, mimi hapa nashauri kwa namna wajumbe wanavyopatikana basi vikao vyote viwe angalau kwenye thuluthi mbili ya wajumbe, *quorum* iwe thuluthi mbili.

Mhe. Spika, tukitunga sheria tunatakiwa tutizame si kwa kuwa tutunge tu kwa sababu tunamuona waziri aliyepo ni muaminifu tukaweka sheria tukija tukipata waziri aliyekuwa kidogo ana tabu akaja akatuendesha vibaya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba hili liangaliwe.

Vile vile Mhe. Spika, katika kifungu cha 16(2) kinachotaja sifa za kuteuliwa Katibu Mtendaji. Hapa Mhe. Spika, nashauri, katika kifungu (a) paongezwe neno 'angalau' baina ya neno ana na elimu. Mhe. Spika, yaani hapa pasomeke hivi:

Kifungu 16(2)(a)

> *(a) "ana angalau elimu ya shahada ya kwanza katika usimamizi wa biashara na uongozi wa biashara au uchumi au sheria au uongozi wa umma kutoka chuo kinachotambulika".*

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu ikiwa tutaachia hivi palivyo basi itakuwa ni lazima Katibu huyu Mtendaji awe na hii shahada ya kwanza na mtu aliyekuwa na shahada ya pili na ya tatu itakuwa haruhusiki hapa kuingia. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nashauri sana hapa pafanyiwe marekebisho hayo.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, ingelikuwa mswada tunaujadili ule ule wa mwanzo nafikiria dakika 30 zisingelinitosha, lakini kwa sababu marekebisho tumeyapata jana naomba Mhe. Spika, nimalizie kwa kutanabahisha kidogo. Mimi huu mswada nimeupitia kidogo na nadhani unaweza pengine ukaleta manufaa makubwa kwa nchi yetu kutegemea na namna utakavyosimamiwa. Lakini Mhe. Spika, hofu yangu ni kuwa usimamiaji wa sheria hii ukaja ukaleta urasimu, ikiwa utatokea urasimu Mhe. Spika, wananchi watachoka nenda rudi na hatimaye patashamiri biashara za magendo, mshike mshike, kamata, shika, peleka Mahkamani na jela, baadae mswada huu sisi tulitegemea uwe ni mswada wa kutuletea neema mwisho utatuletea nakama.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono mswada ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia tukiwa hai na wazima tukiendelea na shughuli zetu katika Baraza hili la Wawakilishi.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi vile vile kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Utoaji wa Leseni za Biashara mwaka 2013. Mhe. Spika, naomba vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuja na fikra hii ya kuwa na sheria hii ambayo itasaidia kuratibu na kuyaweka pamoja masuala yanayohusu utoaji wa leseni za biashara hapa Zanzibar. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya (Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) ambaye ndiye amepewa dhamana ya kuuwasilisha mswada huu hapa Barazani.

Mhe. Spika, nitakuwa sitendi haki kama sikumpongeza sana Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambaye kwa dhati kabisa nataka nikiri kwamba hotuba yake ilikuwa nzito na imefanyiwa utafiti wa kina. Na katika hilo, vile vile nimshukuru kwamba kamati yake iliona matatizo makubwa ambayo yalikuwemo katika mswada

ule wa awali na wamejitahidi mpaka kuagiza kwamba mswada uchapwe upya, lakini Mhe. Spika, nataka niseme kwamba na mimi naungana na Mhe. Salma Mohamed Ali aliyechangia punde hivi kwamba hata huu mpya nao bado una matatizo mengi katika tafsiri. Ukiusoma mswada wa Kiingereza ambao unaeleza dhamira hasa kwa sababu ya lugha yake ya kisheria na ukiusoma huu wa Kiswahili bado kuna matatizo mengi lakini nasema wamejitahidi kamati kwa sababu ule wa mwanzo ulikuwa hata kusomeka una mashaka. Lakini vile vile kama nilivyosema nampongeza kwa sababu hotuba yake Mwenyekiti wa Kamati imekuja na takwimu za msingi ambazo zimetuongoza kujua hasa ukubwa wa tatizo ambalo tunalo.

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ya biashara ni *trading nation* na haya yameandikwa katika vitabu vingi kwa karne nyingi, moja katika maandiko ambayo yanaizungumza Zanzibar miaka mingi iliyopita ni andiko la wasafiri wa Kigiriki maafuru wanaitwa *The Periplus of the Erithrean Sea* ambayo iliandikwa takriban miaka 2,500 nyuma. Wasafiri hawa walipokuwa wakielezea Zanzibar ambapo katika maandiko yao waliipa jina kwa lugha yao wakaita *Menuthia***,** walisema kwamba walikuta tayari katika visiwa hivi na ukanda wake wa mwambao tayari vilikuwa vikifanya biashara na nchi za mbali na wakathibitisha kwamba hiyo ni moja katika vigezo vya ustaarabu kwa watu wa hapa kwa sababu wafanyabiashara na hasa ikawa na nchi za mbali kutoka pale ilipo ni moja ya kigezo cha ustaarabu na kuendelea kwa jamii ya watu. Sasa kwa sababu hiyo Mhe. Spika, kwa vyovyote vile uchumi wetu utajengeka kutokana na jinsi watu wetu walivyokulia karne na karne ambayo moja ni biashara.

Lakini pia Mwenyezi Mungu akatupa bahati nyengine kuwa ni visiwa na visiwa hivi vimekaa mahali pazuri sana kijiografia. Silipati neno zuri la kiswahili la kueleza kile ambacho waingereza wanakita *Strategic location* maana nikisema kuwa ni eneo la kimkakati naona haileti maana iliyokusudiwa. Mwenyezi Mungu ameviumba vimekaa Akatika pahala ambapo ukivitumia vizuri vina nafasi kubwa sana ya kuleta mabadiliko na tija na faida kwa wakaazi wenyewe lakini pia kwa maeneo ya jirani.

Mhe. Spika, moja katika watu maarufu sana waliotoka katika visiwa hivi Mwanafalsafa ambaye amejijengea heshima duniani Marehemu Abdulrahman Babu, aliandika waraka mwaka 1994 ambao aliupa kichwa cha maneno *Zanzibar and the future*. Katika waraka ule alizungumzia *Strategic location* ya Zanzibar na jinsi ambayo pia maeneo mengine yana nafasi kama hii kwa Zanzibar yalivyoweza kufaidika akaitaja Shangai, akaitaja Hong Kong, Singapore akataja Bombay na baadhi ya nchi kama hizo.

Lakini kama waraka wake ule Marehemu Abdulrahman Babu akasema maeneo mengine yote yamesaidia kunyanyuka kwa zile nchi husika au miji husika. Lakini pia kuleta maendeleo kwa maeneo jirani yanayozunguka. Akaitaja Shangai ilivyoifungua China na leo vile vile na Hong Kong baada ya kuwa imerejeshwa China vile vile.

Lakini akaitaja Bombay ilivyoifungua India, akaitaja Singapore ilivyoifungua hata nchi jirani za Malaysia akasema pengine katika miji na visiwa vya aina hii dunia mzima kisiwa pekee ambacho kimerudi nyuma chenyewe na kimeshindwa hata kuendeleza maeneo mengine jirani ni Zanzibar na moja alilolitaja akasema ni kutokana na ukosefu wa ubunifu wa sera sahihi. Lakini pia akasema Zanzibar kutokana na mfumo wake wa Muungano ambao umejiingiza na Tanganyika.

Na hili Mhe. Spika, nalitaja katika maeneo ya Utangulizi kwa sababu mswada umekusudia kuweka mazingira mazuri ya leseni za biashara ili kufanya Zanzibar iwe pahala rahisi zaidi kufanya biashara. Lakini kama kuna maeneo mengine ambayo bado hatujarejesha katika mamlaka ya Zanzibar tutashindwa kuyasimamia bali tutakuwa na kazi kubwa sana ya kuvutia na kukuza biashara katika Zanzibar.

Mhe. Spika, nikisema hayo nakusudia kuna mambo yamo ndani ya Sheria na Katiba na kuna mambo yanatokana na kwa tafsiri yangu mimi, na roho mbaya tu ya wenzetu ambao tumeungana nao. Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali katoa mfano wa mipira au matairi ya gari.

Lakini Mhe. Spika, mifano iko mingi sana ya bidhaa ambazo Zanzibar haizalishi wala haina sababu ya kulinda soko la ndani na kwa sababu ni kituo cha biashara tuna haki ya kuvutia na kuweka pengine masharti nafuu ya uwekaji wake yasaidie wananchi wetu lakini pia yasaidie kusafirisha katika maeneo mengine. Lakini tulioungana nao wanaweka vikwazo.

Wakati fulani Mhe. Spika, palipandishwa kodi kubwa ya saruji ili kufanya iwe ni vigumu kwa wafanyabiashara kutoka nje ya Zanzibar ili kulinda saruji ambayo inazalishwa Tanganyika. Kwa hivyo, kunalindwa viwanda vya Tanganyika lakini mwananchi wa Zanzibar anakomolewa kwa sababu inabidi wananchi wa Zanzibar akomolewa kwa sababu inabidi anunue saruji ya ghali kutoka Tanganyika kwa sababu tu hawataki saruji ya bei nafuu kutoka nje ya Zanzibar isiweze kuingizwa, leo panatajwa pia matairi ya gari.

Karibuni pia kikao kilichopita tulizungumza hapa jinsi ya hujuma zinazofanyika Mhe. Spika, mafuta ya kupikia ya *OKI* na mengine yalivyotangazwa na Bodi ya Viwango vya Tanganyika wakayatangaza kwamba hayana ubora wa kutumiwa na binaadamu kwa sababu tu kuna wafanyabishara fulani wanaagiza kule wanataka kuwahujumu hawa wenzao ambao wanaagiza kupitia Zanzibar na baadae tumeona hawakuwa wakweli kwa sababu baada ya kuingia kati hapa tukalizungumza Wawakilishi Waziri akatoa msimamo mzuri karibuni wametia ulimi puani, wametangaza wenyewe kwamba hawakuwa sahihi mafuta yale yana kila sababu na sifa na ubora kwa kutumiwa na binaadamu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo kama hatuendelei kuyadhibiti tutapata tabu sana. Kwa hivyo, ningeomba Serikali hilo ilitizame sana.
Lakini jengine Mhe. Spika, naomba hili nilizungumze ambalo limo katika mamlaka yetu. Pengine litakuwa linaguswa na hayo hayo ya mfumo wa Muungano usiotenda haki kwa Zanzibar. Lakini wenzangu waliochangia Mhe. Spika, sambamba na kuangalia sheria zinazohusu utoaji wa leseni za biashara kuna haja pia katika kumsaidia huyu mwananchi wa Zanzibar ambaye maumbile yake historia yake ni mfanyabishara kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati iwe bishara kubwa au iwe ndogo basi pia kusaidia kumuwezesha kufanya biashara huyo, na moja ambalo linafanyika ni vipi kupatiwa mikopo ili kuweza kupata mitaji ya biashara.
Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali katoa mifano yeye binafsi alivyojaribu kusaidia. Lakini nadhani ni muhimu kwa serikali pia kuangalia siku za mbele kuna pendekezo limekaa miaka mingi Zanzibar, ambalo ripoti za utafiti za nyuma zilipendekezwa kuanzishwa kwa Benki ya Zanzibar.

Benki ya Maendeleo ya Zanzibar na Benki ya Biashara ya Zanzibar. Hizi Mhe. Spika, zilitajwa katika ile ripoti ya Cast Blanc Ban iliyoletwa na Serikali ya Zanzibar kuja kuishauri Serikali ya Zanzibar kuhusu masuala ya mgao wa fedha kupitia *IMF* alizungumza kwa jumla, na bahati nzuri Mhe. Spika, nilibahatika kupata ripoti hii.

Kwa hivyo, nataka kusema hebu serikali itizame haja ya kurudisha benki hizi, vile vile ili iwasaidie kuwapatia wananchi wetu mikopo na kuweka masharti nafuu ili kuweza kuwapatia mitaji ya kuweza kufanya biashara na kupunguza umasikini.

Sasa Mhe. Spika, niende katika mswada, Mhe. Spika, kimsingi mswada unajaribu kama nilivyosema kuondosha urasimu na mpango ambao hauna mpango uliokuwepo sasa wa utoaji wa leseni. Kwamba kila mmoja anaeamua anaweka masharti kwa ajili ya leseni anaweka tozo na ada inakuwa ni usumbufu. Matokeo yake inakuwa taasisi nyingi zinakuwa zinatoa leseni na inakuwa vigumu sana kwa wafanyabishara huendi pahala pamoja ukapata leseni ukafanya biashara yako bila ya wasi wasi.

Sasa katika hii ndio maana nimemshukuru Mwenyekiti wa Kamati kwa sababu katusaidia Mhe. Spika. Kwanza katwambia kuna aina za leseni 243 na katwambia mna sheria zipatazo 68 zinazoongoza mambo ya leseni mbali mbali. Lakini pia katwambia kunahitaji kutumia siku 86 na ngazi 28 za Utawala ili kuweza kukamilisha masuala ya leseni. Lakini akaongezea pia na kwenye kulipia kodi kwenye biashara hasa pia nako kuna usumbufu huo huo. Mtu anahitaji kutumia siku 300 na ngazi 76 za utawala ili kuweza kurahisha kuingia katika mfumo wa ulipaji kodi.
Sasa katika mfumo kama huo Mhe. Spika, ikiwa watu wetu hawalipi kodi tusiwalaumu kwa sababu mazingira tunayoweka si mazingira rafiki ya kumfanya mtu akaingia kwenye ulipaji kodi. Kwa hivyo, nasema mswada huu naambiwa umekusudiwa kurekebisha hayo.

Mhe. Spika, sasa suala langu la kwanza kwa Mhe. Waziri ni kwamba sheria hii au mswada huu ukipita unasaidia kuratibu. Lakini bado hauondoshi hizi sheria wala hauondishi hizi ngazi. Mie nimejaribu sana kuupitia ule wa mwanzo na huu tangu nilipopewa jana naupitia zaidi ya kuratibu sioni vipi utasaidia ukupunguza huu urasimu ambao kautaja Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

Kwa hivyo, ningeomba hilo kwanza Mhe. Waziri akija kwa niaba ya serikali atusaidie wamejipanga vipi kupunguza urasimu kwa sababu ili kuzitia baadhi ya biashara ni lazima tupunguze urasimu huu na hautapunguzika kwa kuratibu tu ikiwa hakutafanyika hatua za misingi kabisa zikafanywa ili kupunguza hizi ngazi na pia idadi za siku ambazo zinahusika katika kupata leseni.

Na hili Mhe. Spika, linakwenda sambamba na ile ripoti iliyochapishwa mwaka 2011 ambayo ilifanya utafiti na kwa mara ya kwanza kuingizwa Zanzibar katika orodha ya nchi ambazo zinafanyiwa utafiti juu ya mazingira yake ya kufanyia biashara. Kuna ripoti zinaitwa *Doing Business in the World*. Sasa mwaka 2010 ilifanyiwa utafiti na mwaka 2011 ikachapishwa ripoti *Doing Business in the Zanzibar 2010*.

Ukiipitia ile ripoti unaona kuna mambo mengi sana yamelalamikiwa na niliwahi kusema hapa Mhe. Waziri wa Fedha alipokuja mwaka 2011 alichukuwa kipengele kimoja tu cha nafasi kwa Zanzibar na akajisifia sana. Nikasema kuna vipengele vyengine zaidi ya 10 ambavyo Zanzibar iko nyuma sana takribani iko mwisho kulinganisha na nchi nyengine za duniani, hichi hakikuzungumzwa. Kwa hivyo, nadhani hili litaangaliwa.

Mhe. Spika, sasa kwa sababu hii kwanza mimi nina tatizo na hili jina la sheria wamerekebisha kamati nimeliangalia na kwa kiengereza lakini bado napata tabu. Mhe. Spika, katika kiengereza wamesema kitaitwa hiki chombo chenyewe kifungu cha 4 kinasema kinaitwa *Business Licensing Regulatory Reform Council* na kwa kiswahili imetafsiriwa kwamba Baraza la Usimamizi wa Marekebisho ya Utoaji wa Leseni za Biashara.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kushauri kwamba inawezekana ndio malengo. Lakini napata tabu kuyaweka hayo maneno mawili pamoja *Regulatory* na *Reform*. Ingelikuwa tunao mfumo wa *Regulation* kabla na sasa tunataka kuufanyia marekebisho tukasema kwamba sheria hii ni ya marekebisho ya mfumo huo ningefahamu. Lakini ninavyojua mimi ilikuwa haipo kulikuwa na huo utitiri na ndio maana sasa kuanzishwa hiyo sheria ya kusimamia na kuratibu.

Kwa hivyo, mimi ningependekeza chombo hiki kiitwe *Business Licensing Regulatory Council* kuliko kwamba kuchanganywe na neno *Reform* haidhuru maudhui yake ni hayo ya kufanya *Reform* ya mfumo wa utoaji wa leseni na kwa kiswahili ingeitwa Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara nadhani lingelikuwa linafahamika vizuri. Hilo moja Mhe. Spika.

Pili Mhe. Spika, naomba sasa niingie katika kifungu cha Kazi za Baraza. Tafsiri ya Kiswahili katika maeneo mengi iko mbali sana na tafsiri ya kiengereza. Nitoe mfano kifungu cha 5 (1d) kimeanza na neno: Toa maelekezo nadhani imekusudiwa kutoa maelekezo. Lakini ukisoma kiengereza kifungu (d) kinasema: *To review all proposal* sitaki kukisoma chote kwa sababu ya muda. Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nadhani kwamba ku- *review* si kutoa maelekezo. Ku- *review* ni kufanya mapitio au kupitia kwa hivyo nilikuwa nadhani hilo likae sawa.

Jengine ni kifungu cha 5 (1e) hapo kidogo nimetatizwa nilikuwa nataka Mhe. Waziri akija anisaidie. Hiki kinasema kushirikiana na chombo chochote kinachofanya tathmini ya mfumo wa utoaji leseni au mfumo wa usimamizi wa biashara Zanzibar au na jambo lolote linalohusiana nalo. Sasa Mhe. Spika, nimepata tabu kidogo kwa sababu nikisoma kazi za Baraza ni pamoja na kufanya hiyo tathmini ya mfumo wa utoaji wa leseni.

Sasa baadae ni pamoja na kazi zake ni kushirikiana na chombo chochote chengine nikajiuliza kwani kutakuwa na chombo chengine ambacho kinafanya tathmini ya mfumo wa utoaji leseni zaidi ya hili Baraza. Kwa sababu kama kuna vyombo vyengine vya utafiti hili tayari limeshatajwa katika kifungu 5(1f). Lakini vile vya kufanya tathmini Baraza lenyewe limepewa kazi hiyo. Sasa nikajiuliza hapa vyombo gani vinapaswa kushirikiana navyo.

Lakini kifungu chengine ambacho nadhani kina matatizo sana Mhe. Spika, ni kifungu cha 5(1h) hichi nadhani kimeondoka kabisa kimepotea katika madhumuni iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, hichi kimeandikwa kutoa miongozo sahihi juu ya sera na maamuzi mengine yalioamuliwa na serikali kuhusiana na mfumo wa utoaji leseni za biashara. Sasa nikisoma katika kiengereza kinasema hivi Mhe. Spika,

Kifungu 5(1)(h):

> "*To give effect to policy directives and other decisions made by the government in relations to business licensing system''*

Sasa mimi nadhani *to give effect* maana yake ni kutekeleza sio kutoa tena miongozo. Baraza linafanywa kama ni chombo cha kuweza kutekeleza sera na maamuzi mengine yaliyoamuwaliwa na serikali. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hapo pana tatizo katika tafsiri.

Jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 5(1)(j) hichi ndio kabisa kinahitaji takribani kuandikwa upya. Mhe. Spika, kinasema kupitia na kuelekeza ada mbali mbali au ada maalumu zitakazolipwa kwa ajili ya leseni, vibali au mamlaka yenye kufanya hivyo kupitishwa chini ya sheria hii. Hii hata mswahili akisomewa hafahamu kiswahili hichi.

Lakini ukiisoma kwa kiengereza unafahamu kilichokusudiwa ambacho hakiingii kabisa kwenye tafisiri hii, kiengereza kinasema:

Kifungu 5(1)(j)

> *"To review and fix national or local fees payable for licences, parmits authorization approved under this Act''.*

Kwanza kiko kifupi na kinafahamika urahsi sana. Lakini kwa kiswahili kimejaa maneno mengi. Mimi nilikuwa nadhani hapa kimekusudiwa ni kupitia na kupanga ada za kitaifa na za maeneo mengine kama Halmashauri na nyengine kama hizo. Ada za leseni, vibali au ruhusa ambavyo vimepitishwa na sheria hiyo. Sasa hapo kilivyo (j) kama nilivyosema kimekorogwa mno hakifahamiki Mhe. Spika.

Na vile vile kwenye (k) kiengereza kinasema:

Kifungu 5 (1)(k)

"To maintain up-to-date and publically assessable national registers of the licences, parmits and authorization required by businesses or by those engaged or inteding to engage in commercial activities as prescribed under the relavant legislation''.

Ukisoma Kiswahili inasema:

Kifungu 5 (1) (k)

> "*Kuweka , kulitunza daftari la usajili wa leseni, vibali na ruhusa na kutoa fursa ya kuonekana na wafanyabiashara na wengine kama ilivyoelekezwa na utaratibu wa sheria*

hii kulihakiki na kuwawezesha wasajili kitaifa wa leseni, halafu limeingizwa kiengereza hapo hapo and taratibu zinazotakiwa za utoaji idhini kwa wafanyabiashara au wale ambao wamejihusisha au wenye nia ya kujihusisha na masuala ya biashara''.

Ni mkorogo mkubwa sana Mhe. Spika, hapa kilichokusudiwa ni kuanzisha na kuendeleza daftari ambalo litakuwa wananchi wanaweza kuliona ambalo litakuwa na taarifa hizo za leseni, vibali na ruhusa ambazo zinatakiwa kutimizwa na wafanyabiashara au watu ambao wanakusudia kufanya biashara na shughuli za kibiashara kama ilivyotajwa katika sheria husika. Sasa nasema ilivyoandikwa humu inakoroga mno.

Hivyo hivyo Mhe. Spika, katika (l) inasema:

Kifungu 5 (1)(l)

"*Kuandaa utaratibu utakaowezesha Baraza kufanyiwa tathmini na serikali kuendeleza yale yaliopitishwa na serikali, kuratibu na kufatilia kwa kutathmini utendaji wake na kutoa taarifa juu ya namna ya kuratibu na ufatiliaji kwa serikalini''*.

Hiyo Mhe. Spika, pia ni tofauti kabisa ya kiengereza ambayo inasema:

Kifungu 5 (1) (l)

"To develop, for approval by Government, measures and process for assessing its performances and to report on the measures and processes to the Government''.

Kwa hivyo, mimi ningesema Mhe. Spika, ili nisiendelee kupoteza muda kwamba kuna haja ya kifungu hiki cha 5 kutizamwa upya chote tafsiri yake ya kiswahili ya kulinganishwa na mswada wa Kiengereza ambao ndio unaoweka vizuri yale makusudio.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, naomba sasa na mimi nikichangie kifungu cha 8. Kwanza Mhe. Spika, ni uandishi kwa sababu kifungu cha 8(1) kinasema Baraza litakuwa na Wajumbe wafuatao na kiengereza haiko hivyo:

(a) Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais.
(b) Atafaa kuteuliwa na kuwa Mwenyekiti anatakiwa kuwa na elimu inayoanzia shahada ya kwanza ya Uchumi, Uongozi wa Uhandisi au Sheria na uzoefu wa miaka saba ya fani hizo.
(c) Waziri kwa kushirikiana na taasisi husika atawateuwa Wajumbe hao kutoka halafu imeorodhesha namba moja (1) mpaka sita (6).

Sasa Mhe. Spika, nadhani kuna matatizo kwa sababu hii a na b ilipaswa iunganishwe kama tunasema Baraza litakuwa na Wajumbe wafuatao atafaa kuteuliwa si Mjumbe, hii ni sifa ya Mjumbe ambae ni Mwenyekiti ilipaswa iunganishwe pamoja.

Lakini jengine Mhe. Spika, tatizo katika hiyo orodha ile ya Jumuiya ya wafanyabishara wenye viwanda na wakulima mswada wa kiswahili unasema Wajumbe watatu, mswada wa kiengereza unasema *two members*. Sasa mimi nachukulia kwamba ni watatu kwa sababu Mhe. Mwenyekiti alipokuwa anawasilisha katwambia kwamba wamependekeza Wajumbe watatu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa nadhani hichi kinapaswa kuangaliwa vizuri.

Halafu vile vile niungane na Mhe. Salma Mohammed Ali kuhusu kifungu cha 10(3) kuhusu...

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu muda wako umemalizika nakuongezea dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nilikuwa naomba nikubaliane nae kwamba hata kama si kwa idadi ya thuluthi mbili alizopendekeza Mhe. Salma Mohammed Ali. Lakini pia kusema ni nusu ya Wajumbe nadhani inapaswa kuwa zaidi ya nusu wa Wajumbe ni tabu pale.

Mhe. Spika, haraka haraka naomba niende sasa kuna vifungu vyengine itabidi niviache. Lakini kile kinacho matatizo sana ni kifungu cha 12 hasa 12 (2,3,4) naomba nisema kwa ujumla kutokana na muda.

Hapa napata tatizo kwanza kifungu cha 12 (2a) kinasema:

Kifungu cha 12 (2a)

> *"Mamlaka iliyomteuwa inaweza kumuondoa Mjumbe wa Baraza (a) ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa aidha Zanzibar au Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania au kwengineko kwamba kwa ushauri wa mamlaka uliemteuwa kutamfanya Mjumbe huyo kukosa sifa za kuendelea kuwa Mjumbe wa Baraza''.*

Sasa katika sheria nzima hapajatajwa sifa za Mjumbe wa Baraza. Sasa unaposema kwamba ukitiwa hatiani ukapoteza sifa unaondoka kuwa Mjumbe sifa zipi? Haielezwi.

Lakini jengine huku mbele kwenye kifungu cha 12 (4b) inasema kwamba Mjumbe ataendelea kuwa Mjumbe, kuna baadhi ya mambo yametajwa. Sasa kifungu cha 4b kinaema: sasa najiuliza kwamba hapa hapajataja sifa tena.

Kifungu 12 (4b)

"Mamlaka iliyomteua tu ikiamua kwamba haina haja anaondoka na huku inasema mpaka akipoteza sifa za kuwa Mjumbe."

Nilikuwa naomba huu mgongano uliokuwepo nisaidiwe Mhe. Spika.

Jengine naomba niulize katika kifungu cha 24 hapa tuliambiwa kuwa itasaidia kuondosha urasimu. Na maombi kuhusu leseni yanatakiwa yasikilizwe na kujibiwa kwa muda usiozidi siku

30. Kwanza kuna kujirejea kifungu kidogo cha 2 hapo hapo kinarejea tena habari ya kuwa usiozidi siku 30.

Lakini matatizo yangu Mhe. Spika, yako katika kifungu cha 24(3) kinasema kuwa:

Kifungu cha 24 (3)

> *"Ikiwa madai yaliyowasilishwa hayakujibiwa katika kipindi kilichotajwa mamlaka ya utoaji wa leseni vibali na ruhusa vitalazima kutoa tarehe ya mwisho ya kutoa jawabu''.*

Sasa nasema hapa hatujasaidia Mhe. Spika, kwa sababu mamlaka yenywe inatakiwa itoe tarehe ya mwisho. Kwa hivyo, hii siku 30 inaweza ikakiukwa halafu akatoa tarehe kwa sababu hakupangiwa tarehe ya mwisho inaweza kuchukuwa muda gani, anaweza akachukuwa muda hata mwaka mzima tena kwa sababu hatukumuekea kiwango, naomba hapa kupata maelezo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba nizungumzie kuhusu kanuni. Mhe. Spika, ukiutizama mswada kwenye kifungu cha 56 (2) kinataja orodha ya kanuni ambazo Mhe. Waziri anatakiwa kuzitunga. Mhe. Spika, kanuni hizi ni kuanzia (a,o) halafu isitoshe ndani ya hizo(a- o) kuna vitoto kwa mfano ukizungumzia (c) ina vitoto kuanzia namba 1 - 4 na (d) 1-5 (g) 1-5 na (i)1-2(j)1-3 kwa jumla Mhe. Spika, hizi kanuni zinazungumzia mambo mengi sana.

Sasa hapa nilikuwa nataka kukubaliana na ushauri uliotolewa kwamba hii sheria inaweza ikawa kama sheria nyengine tulizozipitisha hapa kwamba tutaipitisha. Lakini madhumuni na malengo yake yakachukuwa miaka kufanikiwa kwa sababu ya kutokutungwa kanuni, na tuna tatizo kubwa sana sheria nyingi tunazipitisha lakini kanuni hazitungwi.

Sasa kwa wingi wa hizi kanuni zilivyotajwa au maeneo ambayo yanatakiwa kutungiwa kanuni maana yake inaweza kuwa kanuni moja ikajumuisha yote haya. Lakini ni kanuni ambayo itabeba mambo mengi sana kama haikutungwa Mhe. Spika, sheria itakuwa na ugumu mkubwa kutekelezwa.

Kwa hivyo, niombe tu serikali kwamba kama kweli imekusudia kuweka mazingira mazuri ya utoaji leseni basi iharakishe suala la kutunga kanuni hizi ambazo zimetajwa katika kifungu cha 56(2) ili sheria ziweze kufanya kazi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nasema nategemea nitapata ufafanuzi mzuri wa mambo ambayo niliyauliza na kutegemea kwamba kutarekebishwa yale mambo ambayo nimeyataja hasa yale yenye mgongano wa tafsiri katika mswada wa kiengereza na wa kiswahili na ikiwa yatafanyika hayo Mhe. Spika, nasema naunga mkono mswada huu asilimia mia moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuzungumza machache katika mswada huu muhimu sana wa kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Mambo yanahohusiana na hayo. Mhe. Spika, kwanza nataka nikuthibitishie kwamba muda utakuwepo na Mheshimiwa anaefata ajitayarishe ili kumalizia dakika zilizobakia.

Mimi kwanza nataka nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii lakini pia Mhe. Kaimu Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwanza kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya na kuangalia sheria zetu ambazo zimepitwa na wakati, sheria ambazo zilikuwa zikikwamisha sana utendaji wa shughuli zetu za biashara kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia nilikuwa nataka niseme kwamba mara nyingi huwa nasema kwamba Zanzibar tuna sheria nyingi sana na zinakuwa nzuri tu. Lakini tatizo letu linarudi pale pale katika utekelezaji na usimamizi wa sheria ambazo tunazotunga hapa Barazani.
Mhe. Spika, tunaishukuru sana serikali wanajitahidi sana kutuletea sheria mbali mbali nyengine mpya na nyengine ambazo zinazorekebishwa. Lakini tatizo linakuja wakati mwengine kwa watendaji wetu, aidha kwa kutokujiamini au kutokufuata zile sheria ambazo na wao zilizowaweka katika hiyo mamlaka mpaka na wao wakaitwa wasimamizi wa sheria hizi.

Lakini jengine Zanzibar tumebahatika sana na ninadhani katika nchi duniani zenye viongozi wengi basi Zanzibar ninadhani hatufiki watatu kutokana na *population* yetu na idadi ya viongozi tuliokuwa nao. Leo kwa kuanzisha sheria hii tunaongeza viongozi wengine. Kiongozi si lazima kuwa ni mwanasiasa lakini ukishatungiwa sheria na sheria ikataja kwamba kutakuwa na chombo kitakachosimamia basi hiyo ni sehemu nyengine ya wigo wa uongozi.

Sasa mimi naomba sana wenzetu hawa tutakaowateuwa kwa sheria hii, ninaomba sana wajitahidi yale mapungufu yote ambayo katika sheria ya nyuma basi yaweze kurekebishwa ili nchi yetu iweze kurudisha ile hadhi yake ya biashara.
Lakini Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ninalotaka kulizungumza kwamba Zanzibar ina historia kuwa ni kituo cha biashara kwa miaka mingi. Wazanzibari tangu wakati wa ukoloni walikuwa wafanyabiashara wakubwa na hata baada ya mapinduzi, miongoni mwa wafanyabiashara hata marehemu babu yangu, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema na yeye alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa tu, akisafirisha mbata, pilipili manga, pilipili hoho na mambo mengine, alikuwa akipeleka Mombasa. Kwa hivyo hata damu yangu vile vile inahusika na masuala ya biashara.

Sasa nchi yetu hatuwezi kuimarika kibiashara moja kwa moja ikiwa bado kuna baadhi ya sheria za kodi hatuna mamlaka moja kwa moja. Mhe. Spika, msingi wa biashara ni kodi. Kama huna maamuzi katika masuala ya kodi bado utakuwa huwezi kufanya kazi kwa ile asilimia iliyohitajika na wananchi.

Zanzibar hapa tumeshatoa leseni nyingi sana na kama alivyoeleza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, kwanza na mimi naomba radhi nimpongeze kwa sababu na yeye katika kazi aliyoifanya kuupitia mswada huu, amefanya kazi kubwa sana na hata sisi ameturahasishia mambo mengi wameweza kuyatekeleza vizuri.

Tuna taasisi nyingi za kukusanya kodi lakini bado kuna taasisi moja ambayo hiyo ninadhani Waheshimiwa kwa kuwa tupo katika mchakato kwenye marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ninadhani eneo hili ni muhimu sana kuweza kulijua umuhimu wake na vile vile kuweza kutoa muongozo ikiwemo ndani ya sheria au ndani ya Katiba ili masuala ya kodi Zanzibar iweze kuwa maamuzi yake.

Mhe. Spika, tulipokuwa katika ziara zetu mbali mbali ukiwemo mwenyewe, tulipokuwa katika ziara ambayo huwa sipendi sana kuitaja lakini kila ninavyojizuia nisiitaje huwa siwezi lazima niitaje. Mhe. Spika, tulipokuwa katika mafunzo nchini China, tuliwauliza jee, kuna miujiza gani nchi ya China ambayo ukubwa wake ni mara moja na nusu ya *population* ya watu wa Bara la Afrika. Kwa sababu China wapo karibu watu bilioni moja, milioni mia nne. Bara la Afrika bado tupo *around* kwenye milioni mia nane lakini tukawauliza ni kitu gani kinachosababisha nchi ya China ikapiga maendeleo ya haraka sana kiuchumi.

Kitu ambacho walichotueleza tulifanya *reform* ya uchumi wetu na kuna maeneo tukayawekea kipaumbele. Tukawauliza ni maeneo gani ambayo mumeyawekea kipaumbele? Wakasema tuliamua kuyatangaza baadhi ya maeneo yetu ya nchi yetu kuwa ni maeneo huru ya kiuchumi. Kwa bahati nzuri sana China ni nchi moja lakini baada ya kuanzisha mageuzi ya kiuchumi waliamua kuvutia uwekezaji kutoka nje. Na ule uwekezaji kutoka nje, kitu ambacho walichovutiwa ndio hili suala nililolizungumzwa kuwa wamefungua maeneo huru ya kiuchumi. Wao walifungua baadhi ya mikoa, mkoa kwa mkoa na zaidi waliangalia yale maeneo yenye bahari ambapo kuna na bandari.

Mhe. Spika, walivyotueleza katika kila mkoa ambalo wametangaza kuwa ni eneo huru la kiuchumi, pato la mkoa ule na wenzetu wana *provinces*; serikali yao inaundwa kuna serikali kuu halafu kuna hizi *provinces*.

Mhe. Spika, mapato ya *provinces* zile kila mwaka yalikuwa yanaongezeka. Walifungua eneo la mwanzo, palipoimarika wakafungua eneo la pili, tatu. Kwa hivyo nchi moja ya China waliweza kutanganza maeneo huru katika mikoa tofauti. Nini kilichoweza kuwasababisha kuweza kumudu kufanya *reform* na kuweza kufungua yale maeneo huru ya kiuchumi.

Kitu cha mwanzo waliweza kurekebisha kodi ya uingizwaji wa bidhaa zikiwemo malighafi lakini waliweza kupunguza kodi katika masuala ya umeme na leseni. Kwa hivyo kuna mambo tofauti ambayo hivyo ndivyo vigezo vilivyoweza kuwafanya wakaweza kufungua maeneo huru ya kiuchumi. Kitu ambacho walichotwambia kwamba baada ya kufungua maeneo yale ya huru kiuchumi, wananchi wengi ambao walikuwemo mashambani, ambapo kilimo chao kilikuwa hakiwapatii tija kubwa sana na zaidi katika haya maeneo waliyofungua waliangalia zaidi yale maeneo ambayo kuna umaskini.

Maeneo yale sasa hivi yamekuwa ni maeneo makubwa kibiashara na kila eneo linajitegemea katika mambo yake ya ndani. Yale maeneo ya mambo ya kimataifa yanashughulikiwa na serikali kuu. Tumeshuhudia Mhe. Spika, eneo ambalo nilililokwenda mimi mara ya pili nchini China, tulikwenda kujifunza, wanaitwa eneo la Quingadau. Eneo lile wana mambo mengi kikiwemo kiwanda kikubwa sana cha bia ambacho kipo nchini China, wanaita *Quingadau beers*, na wenyewe wanakwambia ukenda China kama hukunywa *beer* ile basi hujatembelea China lakini mimi sikuwahi kunywa. (*Makofi*).

Lakini si hivyo tu pana kiwanda cha kuunganisha vichwa vya treni au vya kutengenezea railway na bidhaa nyengine mbali mbali. Sasa haya yote yametokana na nini? Yametokana na kuwa na uhuru wa kuweza aidha kusamehe kodi katika baadhi ya maeneo na kupunguza kodi na kuweza kupanga kodi katika maeneo mbali mbali.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa Zanzibar moja katika tatizo letu ndio hilo. Mwenzangu Mhe. Makame Mshimba kazungumza hapa, wafanyabiashara wengi walianzisha shughuli zao mbali mbali, waliamua kufunga kwa sababu ya kodi. Biashara Mhe. Spika, ni *competition*, biashara ni ushindani. Nusu shilingi inaweza ikamuondoa mfanyabiashara kumpeleka pahala na haya tunayaona kwa kweli katika maeneo mbali mbali. Sasa mimi ninadhani ili Zanzibar kuwavutia wafanyabiashara wa nje na wa ndani kuweza kuekeza katika maeneo ya biashara, basi ni kuweza kuwa na mamlaka ya kuweza kuamua maamuzi ya kodi.

Mhe. Spika, ukiangalia *nature* ya Zanzibar ni visiwa na katika ki-*geograhical* sisi tupo kwenye mfano kama ile panda, kwa sisi washamba, basi sisi ndio kijiti ya ile panda yenyewe. Yaani tupo kati kati, tupo *angle* ambayo ni nzuri sana kibiashara. Lakini jee, tuna maamuzi ya moja kwa moja ya kuweza kufanya maamuzi ya kukaribisha wawekezaji bila ya masharti yoyote.

Kama nilivyosema kwamba wenzetu wale Wachina walitwambia vipi, kama mutaweza kuwa na maamuzi katika sera za kodi pamoja na leseni, Zanzibar muna *opportunity* kubwa ya kuweza kuwa kituo kikubwa cha biashara kwa nchi za Afrika ya Mashariki.

Sasa mimi ninadhani wakati ndio huu Waheshimiwa, kuna baadhi ya mambo tukiweza kuyarekebisha, mimi ninaamini wafanyabiashara wengi wataweza kuvutiwa kuja Zanzibar.
Jengine katika masuala ya kibiashara na moja katika kivutio kuwa na mabenki ambayo yanayoweza kutoa mikopo ya nafuu. Mikopo ya muda mrefu tena yenye riba nafuu. Mhe. Spika, mimi ninataka kuendelea tena kusema kwa bahati mbaya Mhe. Waziri wa Fedha hayupo hapa, lakini suala hili nimekuwa nikimkumbusha mara kwa mara.

Zanzibar sisi ni wabia katika Benki ya *BOT*. Benki ya Tanzania, yaani *BOT* wanatoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo pamoja na wakati, yaani *Small* & *Medium Enterprises* (*SME).* Wenzetu kule wanapata mikopo mpaka ya bilioni nne, tena mikopo nafuu na ya muda mrefu.

Mpaka leo Zanzibar kupitia benki ya *BOT* bado sijasikia mfanyabiashara yeyote aliyeweza kupata mikopo ile. Ukenda sasa hivi Dar es Salaam kila siku kunajengwa mahoteli makubwa makubwa. Wengi wao au miongoni mwao wamepata mikopo kupitia *BOT*, kupitia *Small & Medium Enterprises*. *Why* Zanzibar?

Sasa hiki ni moja katika kivutio cha wafanyabiashara kuekeza katika nchi yetu. Mimi ninadhani hilo bado tuendelee kulipigia kelele. Kwa sababu kama kwa mfano jana Mhe. Waziri wa Ardhi amezungumza maneno mazuri sana kwamba kuna maeneo ambayo waliyopewa wananchi hasa katika maeneo ya uwekezaji, yamezidi zaidi ya miaka mitatu ya ile sheria ya kumiliki ardhi na kuweza kuitumia. Lakini wameshindwa kuiendeleza. Hebu yaangalie yale maeneo yenyewe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika nchi ambayo inajiuza wenyewe ni Zanzibar kutokana na maumbile yake ya *natural* na sio ya kutengenezwa. Leo maeneo ambayo Mhe. Waziri anataka kuyafuta wananchi wale kama watapata mkopo kutoka *BOT* hii ya *Small Medium Enterprises* shilingi bilioni nne, kweli washindwe kujenga hoteli kama Lagema. Hawezi kushindwa. Kuna hoteli nzuri tu ambapo

ukifanya thamani yao pengine haizidi shilingi bilioni nne. Hizi fedha zinatoka *BOT* mkopo, *why* wafanyabiashara au wawekezaji wa Zanzibar washindwe kupata fedha hizo.

Sasa mimi ninadhani na ndio maana nikasema kwamba wakati mwengine hizi fursa zilizokuwepo na sisi ndio Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar, tutoe sauti zetu ili wale wananchi ambao sasa hivi maeneo yao yamo hatarini Mhe. Waziri kuyafuta, basi wakimbilie wapige hodi kule *BOT* hiyo mikopo ili waweze kujenga mahoteli ya kitalii ambayo yataweza kutumika kwa biashara ya utalii. *Otherwise* fursa kama hizo zipo lakini tunashindwa kuzipata maeneo yale yatarudi serikalini.

Mhe. Spika, hata hawa wawekezaji wamekuja hapa wengi wao, hawana pesa. Baada ya kupata hati ya ardhi ndio wanakwenda kwao kwenda kuomba pesa kwa ajili ya kuja kuekeza, kwa sababu itakuwa yale mabenki ya kule kwao yatakuwa yanaangalia jee, hii ardhi ipo pahala fulani, anataka kuekeza mradi fulani, anajua tukimpa pesa huyu ndani ya miaka kumi au kumi na tano fedha zile zimerudi.

Sasa Mhe. Spika, fursa kama hizi kushindwa kuzipata kwa wananchi wetu wa Zanzibar, maeneo yao yatachukuliwa na kwa kweli yatarudi serikalini na watakuwa wamepoteza zile raslimali zao. Lakini jengine nilililokuwa ninataka kulizungumza Mhe. Spika, lazima tuwe *serious* katika kazi. Kwa nini tuwe *serious*. Sisi kama anavyozungumza siku zote Mhe. Waziri wa Fedha tujitahidi na sisi Waheshimiwa Wawakilishi kila tunapopata fursa ku-*convince* wawezekezaji kuja kuekeza Zanzibar. Mhe. Spika, jitihada hizo tunafanya.

Tatizo moja, wale wafanyabiashara au makampuni akishakuja kuekeza Zanzibar Mhe. Spika, tunawanyanyasa. Tunawanyanyasa na tunasema hapa lakini hakuna anayesikia na hili nitaomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu anisikilize sana pamoja na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika hili. Kwa nini wawekezaji tunawanyanyasa? Kwa nini tunaletewa sheria ili kutengeneza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara, wakishakuja tunawanyanyasa?

Nakuja. Kuna mwekezaji mmoja ameekeza na amekata leseni. Mwekezaji huyu ameamua kuekeza katika biashara ambayo inaitangaza Zanzibar, anafanya biashara ya *Airstrip*. Nikitaja tu hiyo ninajua Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshajua *Airstrip*, biashara ya anga ya kufundisha marubani Zanzibar.

Mhe. Spika, unyanyasaji anaofanyiwa mwekezaji huyu au mfanyabiashara huyu hauna maana, sisi kutuletea sheria hizi. Leo nilisema katika bajeti hapa na nikazuia mpaka fungu kwamba mfanyabiashara huyu ananyanyaswa na ananyanyaswa kwa sababu huyo aliyepewa mamlaka ya kushughulikia hilo eneo, yeye ndiye mnyanyasaji mkubwa kwa sababu ana maslahi yake, *personal interest* au *conflict of interest.*

Mhe. Spika, leo baada ya kulizungumza suala hili kwenye Baraza, akaanzisha vikwazo vipya. Kwanza yule *expert* wake kwa sababu na yeye analeta *expert* kutoka nje ili kuja kufundisha hawa marubuni wake. Mhe. Spika, alipata taabu sana katika ku-*renew* kile kibali chake, kwa sababu mgeni hawezi kuishi tu hapa.

Juzi kulikuwa kuna oporesheni kimbunga hapa cha kufukuza wageni waliokuja kinyume cha sheria. Lakini huyu operesheni kimbuga ilikuwa haimhusu kwa sababu ameingia kisheria na kuomba kibali kisheria na ni *expert* anafundisha. Leo Mhe. Spika, usumbufu anaoupata ku-*renew* kile kibali chake inachukua miezi miwili. *Are we serious*? tunatunga sheria hizi kutengeneza mazingira mazuri ya kuwavutia wafanyabiashara.

Kuna suala pia tulilizunguza na pia linamkuta. Leo huyu ni *expert* akiingia katika eneo analipa mia mitano, akitoka mia tano, eeh!...

Mhe. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma na wewe ninakuongezea dakika tano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sasa Mhe. Spika, tumeyazungumza haya leo ni mazingira gani tunayoyatengeneza kuwavutia wafanyabiashara. Wakishafika hapa tunawanyanyasa. Ninaomba sana suala hili serikali ilisikie ili wafanyabiashara hawa wasisumbuliwe, wanatupaka matope na kwa kweli hatuisaidii nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine kidogo aligusia swahibu wangu Mhe. Mohamed Razza kaondoka, kuhusu suala la *direct importation* kwa Zanzibar. Mhe. Spika, hili ni tatizo jengine kikwazo cha kibiashara. Yeye alizungumzia kuhusu mipira ya magari makubwa, ninashukuru alau anawajali wafanyabiashara waliokeza katika *transportation*, kwamba leo kuna bidhaa huwezi moja kwa moja kuileta Zanzibar. Kwa sababu mambo ya biashara sasa hivi unajua haya makampuni makubwa makubwa na wao wanatafuta branch zao. Ina maana kama wanatafuta branch wanatafuta mtu ambaye anakuwa ni wakala wao.

Sasa tatizo la sheria zetu tulizokuwa nazo za kiuchumi, katika masuala ya biashara Tanzania inahesabika ni nchi moja. Leo ndio kama hivyo huwezi ukawa na kibali moja kwa moja ukaleta mipira ya gari. Lakini mimi Mhe. Spika, nilikuwa safarini China, hii safari ya pili ukiacha ile tuliyokwenda na wewe, kuna kampuni ya HIESENCE ya China, tulikuwa na Mhe. Ali.

Mimi nilizungumza na yule *director* wa *Regional Marketing*, wanatengeneza bidhaa za *electronics*, kama simu, *IPAD* na vitu vyengine, nikawaambia nyinyi munafanya biashara kubwa, kwa nini musije kuekeza pale Zanzibar kuna soko kubwa, kuna biashara kubwa ya masuala ya *electronics*?

Wakatwambia kwani Zanzibar ipo wapi? Tukamfahamisha Zanzibar ipo Afrika Mashariki. Akasema Afrika Mashariki tunaye *agent* wetu yupo Dar es Salaam, Tanzania Bara. Tukamwambia Dar Es Salaam ni Tanzania Mainland, sisi tupo Zanzibar. Akasema kutokana na taratibu zetu wakala wetu kwa nchi anakuwa ni mmoja. Kwa hivyo ina maana Zanzibar ni Tanzania, ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itabidi mutumie wakala aliyepo Dar Es Salaam.

Sasa hayo ni maeneo ambayo ni sehemu ya vikwazo. Kwa sababu kama mfano kungekuwa na fursa ya moja kwa moja kuja kuekeza hapa Mhe. Spika, eneo lipo pale Viwanda Vidogo Vidogo kwa sababu wala hawachukui maeneo makubwa au tungetafuta eneo jengine tukampa Fumba hapa akaweza kuekeza. Sasa mimi Mhe. Spika, haya ni maeneo ambayo bado yanaendelea kukwaza fursa za biashara kwa upande wa Zanzibar.

Mimi naomba sana Mhe. Spika, sikutaka kwenda moja kwa moja katika vifungu lakini nilikuwa ninajaribu kuangalia haya mazingira tunayoyajenga, lakini lazima tuangalie na mazingira mengine yanayokwaza biashara kwa upande wa Zanzibar tuweze kuyarekebisha ili biashara ya Zanzibar iweze kukua.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, jambo ambalo ninalotaka kusema kwamba ikiwa tukiwa na fursa ya moja kwa moja Mhe. Waziri wa Fedha wa Zanzibar, akaweza kupanga kodi yeye mwenyewe. Mhe. Spika, Zanzibar itaimarika kiuchumi na tena kwa asilimia kubwa sana. Kwa sababu ukiangalia wengi unaokutana nao kwenye sehemu mbali mbali wanakwambia Zanzibar ni *natural*, kwa kweli ipo katika mazingira mazuri ya kufanya biashara. Lakini bado katika sheria, kwenye maamuzi ya kodi hatuna mamlaka nayo. Sasa mimi ninadhani hilo ni jambo jepesi sana kwa sababu sisi ndio watunga sheria na sisi ndio wapitishaji sheria, na sisi ndio tutakaoshiriki katika Bunge la Katiba ambalo maeneo kama haya tukaweza kuyarekebisha, Zanzibar itaweza kutononoka kiuchumi.

Baada ya hayo machache ninampongeza sana Mhe. Waziri lakini bado ninaendelea kuomba sana hii mikopo ya *SME*, hebu naomba sana serikali yetu iweze kuzungumza na uongozi wa *BOT* ili hawa wananchi ambao maeneo yao wanaotaka sasa hivi, sio kunyang'anywa yanataka kurejeshwa serikalini wakati kule fedha zipo waweze kupatiwa fedha hizi ili waweze kuekeza miradi ya kiuchumi itakayoweza kutoa ajira kwa upande wa Zanzibar.
Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Tunashukuru Mhe. Hamza, naona Mhe. Suleiman Khamis atapata jioni.
Waheshimiwa Wajumbe kuna tangazo moja lakini kabla ya tangazo hilo, jioni kuna Wajumbe wafuatao ambao watapata nafasi mapema. Kwa hivyo niwaombe wasije wakachelewa wakakosa nafasi.

Wajumbe wenyewe ni:

1. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
2. Mhe. Mahmoud Muhamad Mussa
3. Mhe. Assa Othman Hamad
4. Mhe. Panya Ali Abdalla

Sasa tangazo

Waheshimiwa Wajumbe mutakumbuka kwamba tuliwahi kutoa wazo kwa mabenki hasa hasa baada ya kutokea misiba miwili mitatu; mmoja wapo ni msiba wa uliomuhusu Mwakilishi Marehemu Mussa aliyekuwa Mwakilishi wa Uzini pamoja na Mhe. Salum Mtondoo aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu. Hawa walichukua mikopo kutoka benki na kutokana na kufikwa na kifo, walikuwa na madeni, tena wengine ni makubwa.

Lakini tuna mfano mzuri wa mwenzetu mwengine aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni, naye aliwahi kuchukua mkopo kupitia Benki ya *Barclays Bank*. Lakini bahati nzuri

Benki ya *Barclays* wao mikopo inakuwa ina *insurance*. Sasa alipofariki, yeye akawa hana deni kwa sababu *insurance* imelipia deni lile. Kwa hivyo katika mikutano yetu mbali mbali mutakumbuka kwamba tulitoa ushauri na mabenki mengine basi wakubali ku- insurance mikopo yetu.

Mabenki yametusikiliza na *People's Bank of Zanzibar* wamejitokeza sasa kuwa tayari ku-*insurance* mikopo yetu kwa wale waliochukua mikopo huko au wale ambao wana nia ya kwenda kuchukua mikopo huko.

Kwa hivyo jana walikuja lakini ikawa tayari Waheshimiwa Wajumbe mulikwishaondoka. Hivyo tukakubaliana kwamba leo waje watatumia kama dakika kumi na tano tuu ili kutoa maelezo kuhusu *form* za insurance za Bima kwa wale ambao wamechukua mikopo kupitia *People's Bank* of Zanzibar au kwa wale ambao wana nia pengine kuchukua mikopo hapa karibuni kupitia benki hiyo.

Kwa hivyo wapo na wamekuja na *form* zao, wanataka watupe maelezo kidogo katika ukumbi wetu wa hapo juu. Hivyo kwa wale wote ambao wamechukua mikopo kupitia *People's Bank* of Zanzibar na wale ambao pengine wana nia karibuni kwenda kuchukua mikopo hiyo tunaombwa tukutane pale watupe maelezo na hatimaye watupe fomu ili tuweze kujaza baada ya kutupatia maelezo hayo.

Kwa hivyo basi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kupitia tangazo tukutane kidogo kwa dakika chache ili waweze kutupa hayo maelezo na hatimae kugawa fomu na kutuelekeza namna gani ya kuzijaza.

Baada ya hayo basi sasa ninaakhirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 jioni Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni).*

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni na Biashara na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa kazi yake nzuri ya kuandaa mswada huu na leo hii tunao hapa kwa kuuzungumza.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu wa sheria kwa kusema kweli umelenga kuanzisha chombo cha kusimamia utekelezaji. Sasa hapa mimi namshukuru Mhe. Waziri kwamba hiki chombo zamani kilikuwa hakuna, sasa hivi inaonesha kipo chombo madhubuti ambacho kitakachoweza kusimamia utekelezaji wa mabadiliko wa mfumo wa utoaji wa leseni za biashara hapa Zanzibar. Nichukuwe nafasi ya kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kulifikiria hili suala na ndio maana tukapata mabadiliko kidogo ya marekebisho ya sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, chombo hiki kwa mujibu wa maelezo yake ni kwamba kitaweza msingi madhubuti, tena msingi wenyewe utakuwa imara, hilo ni jambo la kufurahisha. Kuendesha biashara na utaratibu thabiti wa utoaji leseni za kibiashara, hili ni jambo zuri na la kufurahisha sana na linatia moyo kwamba angalau kuweza kufikiria juu ya masuala kama haya. Jambo hili litaweza kusaidia kulenga uchumi kwa misingi ya nguvu ya soko.

Mhe. Naibu Spika, mfumo huu mpya ambao aliouleta Mhe. Waziri wa utoaji wa leseni za biashara hapa Zanzibar, pamoja na vibali, na usajili wa maeneo mbali mbali ya biashara kwa suala hili, vile vile litaweza kuwasaidia wafanyabiashara waliowengi. Pia kwa hili tunamshukuru Mhe. Waziri kuweza kulifikiria suala hili la kutoa mfumo maalumu wa leseni za kisasa.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, wazalengo waliopo hapa Unguja suala hili kama watalipokea vizuri, basi mchango wao watakaoutoa watakaoutoa utasaidia kuinua uchumi wetu wa Zanzibar hilo ni jambo zuri na watakapokuwa na nia safi katika suala hili na kuona kwamba na taifa linahitaji kusonga mbele, kwa sababu tuna mambo mengi katika nchi yetu tunataka tuendeshe, bila ya kutoa michango midogo midogo basi hatuwezi kuendesha nchi yetu. Kwa hivyo, wataweza kuchangia vizuri na kuinua uchumi wetu wa Zanzibar. Katika hili tunasema ni katika suala zima la ulipaji wa kodi zile za leseni na za biashara zote takribani ziweze kulipwa kwa wakati mzuri. Hili ni jambo zuri na wao wafanyabiashara walione kwamba hili ni suala la msingi na kila mtu anawajibika kutoa ada hizi.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu pia una malengo mazuri ya kujenga mazingira rafiki, hii ni *environmental friendship* mazingira mazuri, mazingira ambayo ni mazuri sana yatakayoweza kuwavutia hawa wafanyabiashara. Kwa sababu wafanyabiashara, kwa sababu katika biashara kama hukuweka mazingira mazuri *attractive* na ikapata ile *creativeness* ya kuweza kubuni zile biashara namna kwa namna. Kama mazingira ni mabaya hayo mambo mazuri yote hayawezi kuwa, huo urafiki hauwezi kuwa, huo mchango au ada ambayo tunategemea wafanyabishara

wataweza kuutoa basi hawatoweza kuutoa, kama ikiwa hapatakuwa na mazingira mazuri, ili ile *friendship* iwe hili litakuwa ni jambo gumu sana.

Lakini Mhe. Waziri katuahidi hapa kwamba hali ya mazingira yatakuwa mazuri na yataweza kuwavutia wafanyabiashara, bila shaka huyu waziri kaji-*timing* kweli kweli. Kwa hivyo, ni lazima atowe mbinu na njia ya kuweza kuwavutia wafanyabiashara ili wafanye vizuri katika kulipa ada zao zote zinazotakiwa.

Pia kauhisi kwamba msaada huu utaweza kupunguza gharama za usimamizi wa shughuli hizi, kwa vile ilivyokuwa mswada huu kazi yake kubwa ni kusimamia au kuzingatia misingi bora ya utoaji leseni, hili ni suala muhimu sana. Mswada huu mwisho unaonesha kwamba uko tayari kuondosha usumbufu wa aina yoyote kwa hivyo na hapa tunampa pongezi Mhe. Waziri, kwa sababu biashara haitaki matatizo, biashara haitaki usumbufu, inataka kila kitu kiwe wazi. Kwa hivyo, hapa waziri inaonesha kwamba anataka kuondosha usumbufu wa wafanyabiashara na ndio maana mswada huu ukaja. Kwa hivyo, tunampa pongezi kwa hilo na sisi tunashukuru ni jambo zuri.

Mhe. Naibu Spika, kabla mswada huu haujatolewa inavyoonesha hapo zamani kwamba mfumo wa utoaji wa leseni haukuwa ukikidhi haja au mazingira mazuri ya utoaji wa leseni na biashara zote kwa jumla, kwa sababu ilionekana kulikuwa kuna pingamizi kadha wa kadha ambazo wafanyabiashara walikuwa wakipata. Lakini inaonesha Mhe. Waziri mfumo huu utatoa kila aina ya mashirikiano na misaada mikubwa, ili kukidhi haja ya wafanyabiashara katika mambo yote ya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, mfumo uliokuwa zamani unaonesha ulikuwa na mapungufu makubwa sana na ulikuwa una udhaifu mkubwa sana, na hii kama ikitokea kuna mapungufu na udhaifu inaonesha hata utendaji wenyewe ulikuwa sio mzuri. Utendaji wake inaonesha ulikuwa na urasimu mkubwa sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunapenda kumuambia kwamba kama mambo haya aliweza kuyaona zamani, tunamuomba Mhe. Waziri aweze kuhakikisha kwamba katika urasimu huu ambao alisema anataka kuondosha matatizo, basi hili lisije likajitokeza tena baada ya huu mswada kupitishwa na kukubaliwa.

Mhe. Naibu Spika, cha msingi tuiangalie hii historia ya Zanzibar. Historia ya Zanzibar tangu hapo miaka ya awali inaonesha kwamba Zanzibar ni nchi ya kibiashara, na uko ushahidi mwingi sana wa kuonesha kwamba Zanzibar ilikuwa kweli ni nchi ya kibiashara kwa sababu ya kupata watu kuja katika nchi yetu kufanya biashara. Nafikiri sote tunakubali na tunaamini kwamba hapo zamani watu walikuwa wakitoka sehemu mbali mbali kwa kutumia pepo zetu za baharini za Kaskazini na Kusini ambazo hizi *North East Monsoon* na *South East Monsoon*, pepo hizi ambazo zilikuwa zikiwaleta wafanyabiashara hapa wakileta bidhaa hapa na wakinunua bidhaa hapa na kupeleka nje. Kwa hivyo, walikuwa wanaleta na wanachukua.

Kwa hivyo, hii biashara ilikuwepo zamani kwa historia ya asili na iliendelea kidogo kidogo. Lakini tunasema hizi biashara zinagawika katika mafungu mawili. Katika *small scale* na *large scale*, kwamba biashara kubwa na biashara ndogo ndogo. Kwa kweli baadhi ya watu wengine wa Afrika ya Mashariki wanafanya biashara, lakini biashara zenyewe zilikuwa ni ndogo ndogo za kununua na kuuza au kuuza na kununua hapa hapa.

Kwa hivyo, kwa msaada wa pepo hizi tulikuwa tunapata wageni na walikuwa wanafanyabiashara vizuri sana hapa Zanzibar. Kitu kilichokuwa kinaonesha nataka nimuambie Mhe. Waziri kwamba biashara ambayo ilikuwa imejitokeza zamani na mwenendo ulikuwa mzuri vile vile kwa miaka ya nyumba. Ilikuwa biashara zetu tunaweza kusema kwamba zilikuwa *fluctuation of prices*. Vipi *fluctuation of prices*, yaani biashara zake zilikuwa zinapanda na kuteremka, zinateremka na zinapanda. Lakini Mhe. Naibu Spika, nimuambia Mhe. Waziri kwamba hili suala sasa la *fluctuation of prices* katika nchi hii halipo tena, yaani hakuna kupanda na kuteremka. Kwa nini nikasema hivi, nina ushahidi mzuri. Kwa sababu hata hivi leo katika biashara yetu tukitoka nje kwenda kununua tunatumia *foreign* - pesa za kigeni ambazo tunatumia dola. Kwa kawaida ya dola siku zote na miaka yote dola inapanda ikiteremka. Sasa kama ikiwa dola inapanda na kuteremka kwa nini biashara zetu za Zanzibar hazipati hili neno la *fluctuation of prices*, kwa nini wanunuzi wetu hawapati hii bei ya kupanda na kuteremka, kwa nini biashara za Unguja zinakuwa ni *inflection,* yaani ziko juu tu haziteremki chini. Sasa hili ni suala la kujiuliza, wakati tunatengeneza biashara, tunatengeneza leseni na tunawapa ruhusu wafanyabiashara wakafanye biashara nje.

Kwa hivyo, tuangalie yote haya kwamba je, Zanzibar mbona haionekani *fluctuation of prices* kuna *inflection* ambapo kuna kupanda juu juu juu zaidi hakuna kuteremka chini kwa nini. Suala hili naomba Mhe. Waziri kama atakuwa na maelezo aje atueleze hapa kwa nini nchi hii haiba tuliyokuwa nayo, hadhi tuliyokuwa nayo kwa miaka ya nyuma, tulikuwa tunaona kuwa kulikuwa kuna *fluctuation of prices* hivi sasa hakuna kuna *inflection, why inflection?* tutafute sababu ya hii halafu tutafute dawa yake juu ya masuala haya, tupate tiba juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kumuuliza Mhe. Waziri kwenye suala hili atalisimamia vipi ili tuone na sisi tunafaidika matunda ya viwanda. Viwanda tunategemea ni pahala ambapo panazalisha vitu kwa wingi, *large scale production*. Sasa kama tunasema kuwa tukiwa na viwanda tutaweza kuzalisha kwa wingi. Kwa hivyo, hakuna sababu ya kuwa na *inflection.* Tunasema kwamba faida ya viwanda ni kwamba mnunuaji afaidike kutokana na viwanda. Watu wanafaidika kutokana na mtu mwenye elimu, wale wanaosoma kwa mtu mwenye elimu wanafaidika. Sasa sisi katika viwanda tunafaidika nini, ule uzalishaji mkubwa wa viwanda sisi mbona hatufaidiki ndani yake. Tunaambiwa dunia imeendelea, dunia inazalisha kwa wingi bidhaa za aina kwa aina, lakini kwa nini wananchi hawafaidiki na bidhaa zinazozalishwa katika viwanda.

Mhe. Waziri ningemuomba suala hili atakapofanya majumuisho yake na hili atupe maelezo. Ni vipi wananchi wetu wataweza kufaidika na punguzo hili, yaani bidhaa zisibakie pale pale na watu wameendelea katika sayansi na teknolojia, mambo yote siku hizi yamekuwa ni mepesi, *just press the button,* unabonyeza kila kitu kinatoka, unataka maboksi ya sigara basi unabonyeza *button* maboksi ya sigara yanakuja, haihitaji watu wengi kwa kufanya kazi ingawa pamoja na hivyo ni hasara, lakini wepesi wa kiwanda kuweza kuzalisha, unavyoiamrisha mashine ndivyo itakavyotoa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, na haya katika biashara ili hizi leseni ziwe na umadhubuti na kinga na watu waweze kulipa vizuri, basi tuangalie mambo ya msingi ambayo wafanyabiashara yanawakuta.

Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko ya wafanyabiashara na haya malalamiko ni ya siku nyingi sana. Nataka nikuambie Mhe. Naibu Spika, kutokana na zunguka yangu, nimeona kweli ipo haja ya waziri kuweza kufikiria, pamoja na yeye kutaka msimamo kwamba leseni zilipwe vizuri kwa wakati wake na pasiwe na udanganyifu. Kwa sababu kuna watu leseni hawalipi wanafanya udanganyifu. Lakini kuna mambo mengine ya *internal* Mhe. Waziri ni lazima uyafikirie. Kwa sababu yeye anahimiza kwenye kodi, lakini utakuta kuna wafanyabiashara wanalalamika kwamba kodi zimekuwa kubwa, kunakuwa na mtiririko wa ada nyingi sana.

Suala hili ningemuomba vile vile Mhe. Waziri kwamba suala la leseni liangaliwe ukubwa wake kwa kima hiki na kwa mujibu wa bidhaa iliopo na biashara yenyewe inavyotoka, sio kwamba kila duka watozwe kwa zile leseni zao. Iangaliwe na hali ya mazingira ya pahala ya biashara, kwa sababu mfanyabiashara yeyote anakata leseni yake kwa kutegemea kwamba atauza vizuri. Kwa mfano mfanyabiashara ana gunia tatu, nne au tano kaziweka ndani, anategemea kwa siku moja auze gunia mbili au tatu za mchele ili aweze kupata faida ndani yake, lakini kwa sababu ya mazingira ya mahala, mchele ule ameununua na ameuweka dukani, pengine huenda akaula yeye mwenyewe kwa sababu hautoki, unakaa muda mrefu katika duka. Sasa pia katika kutoza hizi leseni basi tuhakikishe na mazingira ya pale mahala. Mazingira ya mjini hayawezi kuwa sawa sawa na mazingira ya mtu anayeishi shamba. Kwanza watu wa shamba biashara zao mpaka waende kulima halafu ndio waje wanununuwe, je gunia hilo la mchele litakwisha, je vitu hivyo ambavyo vimetiwa ndani ya duka vitakwisha. Kwa hivyo, katika utoaji wa leseni tuangalie mazingira ya pale mahala, sio leseni ile moja itolewe kwa watu wote ni kwa mazingira ya mahala. Mimi ningemshauri Mhe. Waziri afanye hivyo. Hizi leseni ziwe na mazingira yake mbali mbali na ijulikane leseni kubwa na ndogo na mahala pa biashara.

Mhe. Naibu Spika, hawa wafanyabiashara wanapoagizia bidhaa kutoka nje huwa wanategemea faida ndani yake, lakini vile vile katika faida hii kwa sababu ya utitiri wa kodi na kwa sababu ya leseni zao ni kubwa sana, zimepitia viwango vya kutozwa na wao huku wanataka kuzinunua bidhaa zile kwa gharama kwa sababu zinataka kuingizwa nchini, zinataka kusafirishwa bidhaa zile, lakini kutokana na kupanda kwa mafuta basi vitu vinaanza kupanda bei. Kwa hivyo, ni lazima Mhe. Waziri aangalie gharama hizi zinavyokuja zinampata mfanyabiashara katika kutoa bidhaa yake bandari mpaka akaichukua kuisafirisha na kuifikisha dukani kwake ni kiasi gani cha gharama zake zina-*involve* hata biashara zile aweze kuziuza kwa bei na yeye angalau apate faida. Yeye ni mtu wa familia anahitaji kupata faida ndani yake. Tuangalie gharama za uingizaji wa biashara mpaka kufika dukani kwake, haya yote ni katika kuandaa kodi na leseni za kutoa kodi hizi ni lazima tuangalie gharama zake. Kwa hivyo, tunaamini kwamba mfanyabiashara yeyote anahitaji kuingiza faida.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuangalie mfanyabiashara huyu huyu tumuangalie kwa upande wa pili, Mhe. Waziri awe anaangalia kuna mambo ya msingi ya kuyachunguza au kabla ya kufanya matendo yote haya, kuna mambo ujuwe kama mfanyabishara aweke duka, duka lile yeye pengine hakai pale anakaa pahala pengine, duka lile linahitaji kulipwa, mlango ule sio wake ni lazima aulipie kodi, umeme anaoutumia katika duka lile ni lazima aulipie wafanyakazi ambao ni lazima awe nao kama wawili au watatu ni lazima wote awalipe. Vile vile kwa kuwa yeye hakai pale au hata kama anakaa pale ni lazima amuweke mlinzi. Haya angalia Mhe. Waziri huyu mfanyabiashara mambo ambayo yanamgusa ya lazima, ni lazima kodi ya mlango alipe, umeme, wafanyakazi, mlinzi wa kutizama ile biashara yake isiibiwe kwa siku ile. Haya ni lazima tuweke

into consideration, ni mambo ya msingi kwa mfanyabiashara yeyote kuyaangalia kabla hatujafanya hayo makubwa. Kwa hivyo, tusiangalie kwamba sisi tunatafuta kodi ya kutafuta fedha nyingi, lakini tuangalie na yule ambaye tunampa kazi ya kuleta ile fedha yenyewe, shughuli ambazo kwa wingi alizonazo.

Kwa hivyo, kinachojitokeza kwa kelele zao ni kwamba faida wanazopata katika biashara zao ni ndogo, yaani mimi naamini kwa Zanzibar yetu hii bidhaa tunazoleta hapa Zanzibar na bidhaa ambazo naamini mtu afanye biashara Zanzibar na aende Bara akafanye biashara basi ajilinganishe baina ya biashara anayoifanya Unguja na biashara anayoifanya Bara. Biashara ya Unguja kwa Bara hata shati hununui, litakushinda shati biashara utakuwanayo na wakati chakula hupati sawa sawa, lakini biashara ile ile ambayo iko Bara anapata faida kubwa sana. Kwa hivyo, katika biashara zetu za wafanyabiashara faida wanayoipata ni ndogo kutokana na gharama zilikuwepo hapa, halafu biashara ni watu. Mzunguko wa pesa Zanzibar haupo, unapotea mara moja mzunguko wa fedha. Kwa hivyo, biashara hapa kila siku inakuwa ni dhaifu. Hili ni suala la msingi, sio kuangalia kodi tu, ni kuangalia hali halisi ya biashara Zanzibar ilivyo, hivi ndio hali halisi yenyewe, kwamba faida inayopatikana ni ndogo na gharama zake za kibiashara ni kubwa sana. Mhe. Waziri hili ningekuomba kama kutakuwa na ufafanuzi wa suala hili sijui utatuambia nini, ili tumsaidie mfanyabiashara, kwa sababu unasema kwamba huyu tumfanye awe na mazingira mazuri, awe katika sehemu nzuri ya urafiki, lakini kwa suala hili urafiki naona utakuwa haupo maana faida ndogo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili ulione vile vile.

Mhe. Naibu Spika, tuone sasa nani mwenye kununua bidhaa hizi, bidhaa hizi Mhe. Waziri ananunua mwananchi na ndio pale tunapopiga kelele kwamba mazingira ya kimaisha Zanzibar ni magumu, bidhaa ziko tele dukani lakini watu zinawashinda kununua bidhaa hizo kwa sababu ni ghali na huyu ana mambo mengi ya kugharamia ili na yeye aweze kupata faida. Je, huyu mwananchi ukimfanya kwa kutwa nzima anataka kula asubuhi, mchana na usiku na akiangalia pesa yake aliyonayo ni ndogo, lakini bidhaa zimo ndani ya maduka na yeye anazitamani na roho inamtoka, lakini hawezi kuzinunua maana yake ni nini. Ni lazima tuwagawe watu kwa makundi yao, kuna wale ambao kidogo wana uwezo wa kimaisha, kuna wale wa kati na kati na pengine ni walalahoi. Angefanya Magret Thatcher wakati katika *monitor system* ya kuweka *Euro,* aliwaambia mimi sitofanya kosa hilo, *I will never do that mistake never.* Anasema Magret Thatcher ikiwa mnataka kufanya *Euro* ya upande wa Europe, fanyeni nyinyi peke yenu, mimi bado *styling town* yangu itakuwa vile. Alikuwa na sababu zake za msingi. Alisema hii *styling town* itaweza kuwasaidia walalahoi, kwa sababu hii wanaangalia TV namna pesa inavyopanda na kuteremka. Kwa hivyo, pesa ni biashara, pesa ni maisha, mzunguko wa pesa unavyokwenda dola. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, haya ni masuala ya msingi ni lazima uyazingatie na tutahitaji maelezo baadae utupe kidogo.

Mhe. Naibu Spika, huu ugumu wa maisha Zanzibar tunauelewa sote na upo, tukitaka tusitake ugumu wa maisha Zanzibar upo, hakuna mtu aliyekuwa hapendi starehe, hakuna mtu aliyekuwa hapendi kula vizuri, hakuna mtu aliyekuwa hapendi kula mboga na samaki. Kuku ni shilingi 12,000 haya mazingira ya Zanzibar tunakwenda vipi. Huyu mlalahoi tunayemzungumza ataishi vipi sawa sawa na wewe waziri, sawa sawa na mimi mwakilishi ataishi vipi huyu, kuna ugumu sana wa maisha jamani tuwaangalieni. Tusione tunapandisha tu kwa ajili ya kupata pesa, lakini tuangalie hali halisi ya wananchi wetu, hali ni ngumu ya kimaisha. Mhe. Waziri suala hili utalisaidia vipi.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na hayo yote aweke angalau masharti nafuu, masharti ya kibiashara yote yawe nafuu, bado Zanzibar haijawa huru ya kutosha, biashara tunayo, lakini tukizungumza neno huru kibiashara Zanzibar bado hatujafikia kwenye *stage*. Tunahitaji kuangalia biashara zetu, hao watu wetu wana uhuru wa kiasi gani wa kuweza kuagizia bidhaa zao nje ya nchi. Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Waziri mzunguko huu wa pesa huko Bara, hii pesa yote hapa Unguja inayochumwa asubuhi mpaka jioni inatiwa ndani ya kapu inakwenda Dar es Salaam, mzunguko hapa wa pesa hatuna, kwa sababu hatuna viwanda, hatuna uzalishaji, uzalishaji katika sekta ya kilimo bado ni mdogo, tunanunua kila kitu mpaka mboga, pilipili na kila kitu tunanunua kutoka Bara, hebu niambie hiyo pesa itabakia Unguja mimi na wewe tuipate. Kwa hivyo pesa iko kule.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo bidhaa ambazo tunazinunua sisi kutoka Bara ni mara mbili ghali kuliko nchi nyengine yoyote. Mimi nakumbuka hapa wakati tunanunua vitunguu maji kutoka India, ni rahisi zaidi vitunguu maji kutoka India kuliko vitunguu maji kutoka Bara. Kwa hivyo, uhuru wa kununua bidhaa nje ya nchi bado haujakuwepo, ni lazima saa nyengine bidhaa zako zipitie Bara kwa ajili na wao wafanye mambo yao. Kwa hivyo, bado nasema pamoja na watu wetu wanataka kukuza mtaji wao wanakwenda India na China kwa kuchukua bidhaa, lakini bado utaratibu wa kupata masuala haya inakuwa ni ngumu sana.

Mhe. Naibu Spika, biashara tunazitaka na watu wetu wanasema maisha ni magumu, uagiziaji hali yake ni kama hivyo hauko huru ni lazima upitie huko kama hukupita huko basi biashara huna na ukifika kule ukirudi kuuza hapa biashara haina faida. Kwa hivyo, kuna mambo ya msingi ya kijamii ni lazima yazingatiwe ili tuone ule uhalali wa kuishi Zanzibar kwa usalama na amani, maana usalama ukiwa umeshiba, ukiwa hukushiba basi usalama hapana.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nimuambie Mhe. Waziri ni kwamba pamoja na biashara ambazo watu wetu wanafanya, lakini bado mtaji wao wa kufanya biashara haujapangwa, kuna watu wanapenda. Sisi watu wa Zanzibar hatuna kazi nyengine ya kufanya hapa zaidi ya biashara. Hebu niambie iko kazi gani nyengine, zaidi ya kuwa mfanyakazi wa serikali. Huyo mfanyakazi wa serikali hivi sasa anapiga kelele, mpe leo pesa kesho atakuambia sina pesa. Kwa nini huna pesa. Mhe. Naibu Spika, hapa Baraza la Wawakilishi tupe leo shilingi 200,000 au shilingi 300,000 au shilingi 400,000 kesho asubuhi kila mtu ukimuuliza atakuambia mimi shilingi sina. Wapi zimekwenda pesa hizi nani kazichukua.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wetu wasipewa pesa ndogo, huwezi kufanya biashara kwa shilingi 100,000 au shilingi 200,000, tuwawekee pesa katika benki ili waende kukopa hawa waweze kunyanyua mtaji wao na waweze kwenda nje kuchukua biashara walete. Tunaamini wakifanya hivyo, basi wafanyabiashara wetu watauza viru kwa urahisi na sote tutafaidika, hili ni jambo la msingi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru kwamba katika wizara ya Mhe. Waziri kutakuwa na ukaguzi wa leseni. Mimi naamini kuwa hili suala la ukaguzi wa leseni ni lazima zipitiwe kwamba kila mmoja leseni awe nayo. Vile vile tunasema kwamba tupate usimamizi mzuri wa shughuli zote za biashara, bila ya kuwa na usimamizi au bila ya kuwa na utekelezaji hatwendi. Hapa tunafanya mambo mengi, tunafanya makabrasha na kila kitu. Lakini unapoingia ndani ya wizara hakuna

utekelezaji, watu hawataki kutekeleza, chauro tu, hakuna uwajibikaji, hapa tunakwenda tu. Hawataki watu kufanya kazi, *they seem to be very lazy, I dont known why,* kwa nini? wamekuwa wavivu hivi. Kwa nini wafanyakazi wetu tunawalipa vizuri, lakini bado utendaji ni mbovu. Magaham magaham mengi, haya magaham ya nini, uende wapi, unataka nini tena. Pepo hutaki, unataka ya dunia tu.

Mhe. Waziri mambo mazito hayo. Kwa hivyo, tunasema jambo jengine la msingi ni kwamba tunataka usalama wa bidhaa za wafanyabiashara wetu. Pia tunasema katika suala hili zima kwamba bidhaa zinazokuja Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo ya wafanyabiashara na wananchi wanaoletewa bidhaa *wallah laadhim* leo tunasema tuna *canser, pressure,* sukari, vyakula vibovu vinaletwa mtu atafanya nini anakwenda kula hivyo hivyo.

Mhe. Waziri, kazi kubwa sana katika suala la biaashara hapana kukaa ofisini akasema nafanyabiashara. Kwanza mfanyabishara na waziri sawa sawa, ukitaka kazi ya biashara kama ni waziri uende na wafanyabishara hii si kazi ya ofisi *field work*. Mhe. Waziri aende *field work* asikae ndani akaangalie huko wananchi wanavyokufa. Nendeni mkachukuwe takwimu za afya mkaangalie watu wangapi wenye *canser,* ziko takwimu zimejaa katika wizara yake Mhe. Waziri *canser* iko imejaa vyakula vibovu na vinaletwa, unga mbovu, mchele mbovu unaletwa hapa watu wanakula.

Mhe. Waziri hiyo ni *very affective* kwetu sisi inaathiri afya yetu ninavyozungumza hapa na Mhe. Waziri wa Afya na kasema tushughulikie afya za wananchi. Vyakula vyako Mhe. Waziri vibovu, unga mbovu, mikate haiwi, chapati haziwi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia umeshatumia nusu saa.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: (anaendelea) Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, leseni lazima zichunguzwe na ziidhinishwe vizuri. Tunamshukuru vile vile Mhe. Waziri kwamba mswada huu utaondosha vipingamizi. Pingamizi ziko nyingi sana katika masuala haya ya biashara. Kwa hivyo, hizi pingamizi kama Mhe. Waziri anachukuwa ahadi ya kwamba vipingamizi vyote vya kibiashara ataviondosha mwaka huu na pasiwe na vipingamizi.

Sisi tupo tunapita humu madukani tutaona kama kuna pingamizi zozote. Msaada huu utaondosha mambo haya. Urasimu jamani tuuondoshe. Huu urasimu tuwape nafuu wafanyabiashara pasiwe na *long process* mtu anakwenda hapa mpaka akifika kijasho kinamtoka siku kumi hajapata analolitaka *wh?* Kwa nini hatufanyi *short cut* ya mambo haya, uwezo tunao wa kufanya hivyo.

Tunatafuta watu wenye elimu watu wazuri wamekaa ndani ya maofisi anakwambia *after 30 days* ndio utapata *why after* 30 *days* kwa nini? Tunataka huduma za haraka katika biashara tunataka ku-*fieled up life*. *Life* iwe nzuri watu wapate chakula kizuri, biashara ziwepo ungumu wa maisha uondoke.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Kwa hivyo, namshukuru Mhe. Waziri kwamba anasema ataondosha mambo yote.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu. Ahsante sana mwisho naunga mkono hoja hii mia kwa mia na wananchi wangu wote. Ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa madhamuni makubwa ni kuja kuwatumikia wananchi wa nchi hii ya Zanzibar ndani ya Baraza lao hili tukufu, lakini Wajumbe waliokwisha tangulia wamekidhi haja juu ya mswada ulioko mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuombe, nadhani utakubaliana na mimi Mhe. Waziri wa Biashara amesikia na inapotokea mtu mzima tena akilia ujue kuna jambo. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba yale yote ambayo Mjumbe aliekaa sasa hivi mtayachukuwa na kuyazingatia vile ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tuna bahati na upendeleo maalumu, Mwenyezi Mungu kaijaalia hivyo na ni mataifa kadhaa duniani, Mwenyezi Mungu ameyajaalia na rasilimali zao ili wazitumie rasimali hizo ni pamoja na rasilimali watu. Zanzibar Kijiografia ina nafasi nzuri sana kwa shughuli za biashara na miaka 50 – 60 iliyopita tulikuwa na sifa hiyo hapa kati kati tena ni kwa hayo mazoe ya watu wetu na *nature* iliyopo kama alivyosema Mjumbe hatuna shughuli nyengine zaidi ni biashara na barabara yetu kuu ni njia ya Anga na njia ya bahari. Tuitumie bahari yetu twende na shughuli zetu za kibiashara, tuitumie anga tufanikishe masuala yetu ya biashara tuwatumie watu wafanya biashara.

Sasa katika hilo Mhe. Naibu Spika kazi kubwa ya serikali ni hii ambayo sasa imetajwa ndani ya mswada huu wa sheria kufanya *reform* ya mfumo utakaoleta haja iliyokusudia ili wafanyabiashara wetu waweze kufanikisha malengo yao na malengo ya serikali yao.

Mhe. Naibu Spika, tuna rasilimali ambazo baada ya mfumo huu kama vizuri kama unavyokusudiwa na zenyewe zikasimamiwa vizuri tatizo letu kwa maoni yangu mimi suala la uchumi kwa wananchi na tukipata chombo cha kusimamia uchumi huo sasa mambo haya yanayolalamikiwa itakuwa ni hadithi.
Mhe. Naibu Spika, nakusudia kusema kwamba kuna *part two* ya mswada huu kuanzishwa kwa Baraza sehemu ile ya kazi za Baraza kifungu cha 5 (2) katika utelekezaji wa kazi zake Baraza litafanya kazi kwa mujibu wa madhumuni ya Sera ya Serikali ya Utoaji wa Leseni.

Mhe. Waziri jambo hili tunalo hapa tunayo Sera ya Serikali ya utoaji leseni? Kwa sababu kadiri tutakavyofanya kama ni kinyume nyume au ni mbali ya Sera ya Serikali au hatuna sera hiyo. Hata hii sheria nzuri, malengo mazuri bado yatabaki kuwa ni ndoto. Utekelezaji kuwalenga watu dira yetu ni ipi. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri hilo hebu awasiliane na watu wake awe na jibu sahihi katika hili. Tufanye kitu tukiwa tunajuwa tunapita wapi.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wetu Zanzabar wengi wao wanafanya kwa uzoefu nani anakwenda India, baba mdogo anakwenda Thailand na yeye kapata chochote chake

haya na hoja si kutoa leseni au kibali au ruhusa lakini tunasema kujenga mazingira mazuri kama yanavyodaiwa humu ni pamoja na taaluma kwa wafanyabiasha wetu ya kufanya hii biashara kusudi iende sambamba na tija kwao na faida ya taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, tutakuwa na wafanyabiashara baada ya kutoa leseni hizi kwa njia inayotakiwa sasa ambao hawa hawatobadilika, watakuwa na daraja lile lile la chini, hii ngazi ya wamachinga sina hakika kwamba utaratibu wao umeelezwa vizuri hapa. Lakini kutakuwa na kada ya pili na kada ya tatu. Lakini wote hawa ni juu ya serikali ndio niliposema hii sera iwaweze makundi yote matatu na wafaidike na sera yao.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu nchi nyengine wamachinga wanapata mikopo kutoka mabenki, vyombo hivi vya fedha zinatoa mikopo mpaka ya kutwa, iko ya wiki, mwezi kufatana na mahitaji. Sasa Mhe. Waziri isiwe wizara ni kusimamia leseni tu lakini lazima tuwasimamie na hao tunaowapa leseni zinatumikaje leseni hizo, vibali hivyo, ruhusa hizo si ukishampa yafanyike yafanyikavyo kama hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kukosa serikali mkono wake hapa ndio maana leo tunapokea vifaa na bidhaa feki, mbaya, sumu, tupu. Zanzibar sasa imekuwa ni jaa na vinapita bandari na vinapita viwanja vyetu vya ndege vimejaa.

Mhe. Naibu Spika, ukiuliza hivi leseni imetoka, yule anaetuletea mafuta yale yanayoharibu magari na vyombo vya watu hapa kapewa leseni afanye hivyo kweli? Sasa nianchosema si tu kupewa leseni hapana tuwe na sera ya kusimamia leseni hiyo au ruhusa hiyo na kibali hicho na yule ambaye atakwenda sivyo basi kuwe na namna.

Mhe. Naibu Spika, *BOT* hii ni Benki ya Tanzania, Watanzania wafaidike na *BOT* yao. Wenzetu Bara wafanyabiashara wanapata mikopo mikubwa, mahoteli yake tunayolala Kariakoo si tu kwamba ni ujanja wao bali ni mikopo na inayotoa mikopo ni benki hii.

Hebu Mhe. Waziri twambie sasa umejipanga pangaje ili mipango hii mizuri ya leseni na vibali na fursa zako utakazotoa kwa wafanyabiashara? Utawawezeshaje na wao wafaidike na mikopo kwa sababu biashara ni pamoja na mbadiliko huu wa kukopa na kulipa na bila Taasisi zetu za Fedha kutoa mikipo kwa wafanyabiashara wetu hatuna safari ndio pale Mhe. Naibu Spika, serikali inapohesabu hatua moja ya 6.5, 7.2 ya uchumi umekua, lakini wananchi huku wanalalamika kwa sababu sisi tunahesabu majumba na barabara lakini mwananchi mfukoni hana kitu analala na njaa.

Kwake suala la kukua kwa uchumi hapo halipo na ni kweli halipo kwa sababu ana njaa hana pa kulala, hanunui daftari la mtoto, hawezi kulipa huduma za afya, huwezi kumwambia uchumi umekuwa. Uchumi utakuwa kama mtoto wake kamletea gari kutoka Uengereza ama pahali pengine anakwenda nalo Dar es Salaam limelipiwa ushuru Bandarini Zanzibar imeleelezwa kwamba popote ndani ya Tanzania ukisha lipa umelipa. Leo asubuhi hapa tunaambiwa kalipa ushuru Zanzibar akifika tena Dar es Salaam analipa tena ushuru mbona mnatuchanganya, nani anasema ukweli sasa.

Sasa hali hii hujamsaidia mfanyabiashara huyu. Kwa hivyo, tunaomba sana na Mhe. Naibu Spika, mimi na wewe tumeshakuwa Kamati moja ya Baraza hili na Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwenyekiti wa sasa, bado tuna tatizo na *BOT*. kutokana na hali hiyo, bila ya suala hili kukaa sawa wafanyabishara wetu pamoja na serikali yetu suala la uchumi tutaendelea kulizungumza humu ndani, basi hatuwezi kwamwe kusogea wala kupiga hatua, hatuna chombo cha kusimamia uchumi wa nchi hatuna *BOT,* hilo haijaweka mkono wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mipango mizuri hii na vyombo utakavyokuwa navyo vya kukusanya kodi za wafanyabiashara wetu. Lakini hatuna chombo cha kufanya *monitoring and supervision,* sijui tutakwenda wapi katika suala zima tulilosema kukuza uchumi kufuatana na ubora wa soko pamoja na mambo mengine na hayo mambo yawepo hapo na sehemu ya kukopea ni Benki of Tanzania. Kwa kweli wazanzibari hawafaidiki na benki hii na suala letu la uchumi bado lina matatizo.

Mhe. Naibu Spika, sheria imetaja chombo cha kusimamia na kutoa hiyo leseni. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tumuombe Mwenyezi Mungu kwamba dhamira yake iende sambamba na mabadiliko ya chombo hichi ya mfumo huu.

Lakini mimi huwa ninajiuliza kwani chombo hichi kinataka kusimamiwa na watu kutoka wapi na tatizo letu sisi hapa ni sheria, kwa sababu tatizo ni utekelezaji au usimamizi wa hizi sheria tunazozitunga.

Mhe. Naibu Spika, hivi Mhe. Waziri amejipanga vipi kutuhakikishia hili kwamba litakwenda kama hivi ambavyo anavyotueleza humu, nadhani tunazidi kuongeza mambo tu yanakuwa mengi zaidi na sijui pengine kama hautakuwa mzigo zaidi. Kwa hivyo, hautakuwa mzigo kama dhamira itafikiwa, ufanisi ukapatikana, isipokuwa ninajiuliza chombo hichi kwani kitasimamiwa na nani *seriousness and commitment* Mhe. Naibu Spika ndio inayokosekana hapa katika masuala yetu yote.

Sasa kama Mhe. Waziri anayo namna aliyojipanga kwamba atahakikisha kuwa mabadiliko haya yataleta madhumuni na maudhui yalikusudiwa basi nitashukuru.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala hili la aliyekuja na akapewa leseni akapata ruhusa ya uwekezaji. Kwa hivyo, nadhani ni vyema tutizame vipengele ni vipi mzalendo atapata kuingia ubia na huyu aliyekuja hebu tutafute vipengele wa kumpa leseni mwekezaji lakini kwa kushirikiana na mzanzibari kuwe na hali hiyo, ili kule Uroa, Potoa, Micheweni na kwengineko na yeye aondoke pale alipo baada ya kukalia kigoda saa 9 au 10 anacheza bao, basi ashughulike na huko.

Katika hali hiyo, ndio kukuza uchumi ule ambao atauona kwamba amebadilika na kulikoni kutujengea barabara hii na ukamwambia tunakua kiuchumi, lakini hana cha kusafirisha kutumia barabara ile.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, na hili ni jambo la mwisho na kwa bahati nzuri Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria *Alhamdulillah* wamo wote.

Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Hamza Hassan Juma asubuhi alipokuwa akichangia ametaja huyu mwekezaji mzalendo kuna neno ametumia *airstrip* nikisema hivi Mhe. Mwanasheria Mkuu anajua tunazungumza nini. Sasa huyu ameekeza mahala na kitu ambacho Zanzibar yenyewe inapata ile *proud*.

Lakini jambo la kusikitisha serikali sijui haifahamu hivyo na hata tunashindwa sijui tuseme vipi. Kwa kweli mpaka juzi wakati tulipokuwa tukichangia hotuba za bajeti tulilizungumza sana hili, kwamba jamani eneo hili ni muhimu kwa Zanzibar tunapata vijana hapa na wala si vijana tu wazanzibari, lakini mpaka kutoa nje ya Zanzibar wanakuja hapa wanafunzwa na kinachoingia si yule bwana peke yake anafaidika, isipokuwa na Zanzibar yenyewe inafaidika, lakini nimesema moja *is aproud for Zanzibar*.

Mhe. Naibu Spika, sasa kwa nini serikali haitaki kutusikiliza pamoja na usikivu wa serikali ni kwamba eneo hili limekamatwa na mtu ni lake yeye maana hivi sasa imekuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwanasheria Mkuu alitoa maelekezo pamoja na maelezo. Lakini tunamwambia tena kwamba bado ni tatizo hapa na huyu mtu sijui munamfichia siri ipi, kwa sababu yeye sijui ni nani ndani ya serikali na wala mimi sifahamu ana mamlaka gani sijui au ameegemea wapi anajua yeye.

Kwa hivyo, tunachokisema sisi kwamba Zanzibar ni ya wazanzibari na huyu ni mwekezaji mzalendo na serikali inapaswa kumlinda kwa namna yoyote ile, basi ni vyema imlinde kwa sababu wanaofaidika ni wazanzibari na heshima inayoletwa hapa ni ya Zanzibar, yaani amejitolea yeye hivi kwa nini tunamuangusha namna hii.

Kutokana na hali hii, hatumuangushi yeye tu isipokuwa tunawaangusha na vijana wetu jamani tunatoa *pilots*, lakini leo munam-*frustrate* mpaka atafute mahala aende. Mhe. Naibu Spika, wazanzibari wanakimbia kutokana na maudhi kama haya, sijui kuna watendaji wanachoyo au ubaya wa kiasi gani, yaani hawataki kabisa na wao kuchangia maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ujumbe huu Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tunasema hivi huyu mtu kama ameitwa na Mhe. Rais amemwita na wala hatuna ugomvi na uteuzi wake, isipokuwa tunachokitaka ni ufanisi wa mtu huyu uonekanwe na aheshimu hii nchi kwamba wenyewe ni wananchi si yake yeye.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Asaa Othman Hamad ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, naona tunatoka kwenye mswada, hivyo ni vyema tuchangie mswada naomba sana. kwa hivyo, nafasi sasa tunampa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na baadaye afuatie Mhe. Panya Ali Abdalla. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika mswada wetu huu muhimu, mswada ambao

unazungumzia kuhusu Kuanzishwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na mambo yanayohusiana na hayo hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kufika hapa na kuendelea na mambo ambayo tulikuwa tumejipangia.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na kwa leo hapa Kaimu Waziri ambaye anafanyakazi hii kwa niaba yake pamoja na timu nzima ya wizara kwa kazi kubwa na nzito, ambaye wameifanya na hatimaye kuweza kukamilisha ile ndoto ya miaka karibu 25 iliyopita nyuma katika suala zima la kuratibu shughuli za leseni ndani ya wizara hii.

Kwa kweli napenda kutoa shukurani na pongezi za pekee kwa ndugu yetu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kutimiza njozi ambazo tulikuwa tunazo tokea kipindi ambacho tunafanyakazi katika Taasisi ya Wafanyabiashara - *Zanzibar Chamber of Commerce*. Mhe. Naibu Spika, taasisi hii kwa kipindi kirefu tulikuwa na kilio hichi cha kutaka masuala ya biashara yasimamiwe na Wizara ya Biashara yenyewe na hatimaye sasa leo nimefarajika sana kuona kwamba zile njozi zetu zimetimia na leo tupo hapa tunajadili mswada unaohusiana na jambo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia kuchangia mswada wetu hii nataka nianzie kwenye kifungu cha 11 ambacho kinazungumzia masuala ya maslahi ya wajumbe wa Baraza. Katika suala zima la maslahi ya wajumbe wa Baraza hapa kuna maelekezo kwamba watalipwa maslahi na posho kama ilivyoamuliwa na waziri mwenye dhamana.

Sasa mimi nataka kufahamu tu haya masuala ya maslahi yao na posho yatakwenda kwa mujibu wa matakwa ya Waziri au toleo ambao litakuwa lipo katika masuala haya ya ulipaji wa posho na mambo mengine kama yalivyo katika taratibu zetu za sheria zilizokuwa zimetangulia nyuma.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 254 katika *bullet* ya 12 kuhusu kuwa wazi kiti cha Mjumbe wa Baraza, lakini kwenye kifungu (2)(b) katika mswada huu wa kiingereza. Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu cha (b) kulikuwa na maeneo matatu ambayo yamezungumzwa yalikuwa ndio maeneo ambayo, yaani mamlaka iliyoteua inaweza kumuondoa mjumbe wa Baraza ikiwa atakosa sifa hizo. Sasa tukiangalia ule mswada wa Kiingereza kuna sifa tatu pale, lakini mswada wa Kiswahili (b) iko moja tu.

Kwa hivyo, naomba kupata ufafanuzi hapa zaidi ni vipi au ipi ambayo ni sahihi, ni hii yenye *translation* ya Kiswahili ambayo ina (b) tu ama ile iliyozungumzwa kwa Kiingereza ambayo ina (b) lakini numbari za Kirumi (i), (ii) na (iii), Mhe. Naibu Spika naomba kupata ufafanuzi katika suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea mbele kidogo ningependa pia Mhe. Waziri aje atusaidie kifungu cha 15 ukurasa wa 255 kifungu kidogo cha (1) huku mbele tumeainishiwa kazi za *secretariat*, lakini tukija tukiangalia humu ndani kwenye kifungu chenyewe cha 15 kwa kuzingatia masharti chini ya sheria hii kamati, sasa ni kamati au *secretary*, hivyo naomba kupata maelekezo katika hili.

Jengine tukija chini yake *bullet* ya 16(c), ambapo kinaeleza kwamba hakutiwa hatiani na makosa yanayohusu maadili ya ufisadi au rushwa. Mhe. Naibu Spika, kuna makosa yanayohusu maadili ya ufisadi au rushwa na hapa pia naomba kupata ufafanuzi je hapa imekusudiwa nini hapa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufaya majumuisho kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, atusaidie nini hasa wamekusudia kutueleza hapa.

Vile vile tukija kwenye ukurasa wa 257 kifungu cha 20(2) naomba kupata ufafanuzi juu ya serikali haitaingilia kati masuala ya biashara ya upatikanaji wa leseni, vibali au ruhusa isipokuwa kwamba shughuli hizo za kibiashara zitapelekea au kusababisha. Kunamtiririko wa nambari (a) - (k), ningeomba ufafanuzi kidogo nini hasa malengo yaliyokusudiwa kwenye hili.

Nikiondoka hapo vile vile naomba kueleweshwa, nimejaribu kuungalia huu Mswada adhabu zake kwa wale ambao watashindwa kutii haya mambo zipo vipi. Ukiangalia adhabu ambazo zipo, ukurasa wa 267 Kifungu cha (49) adhabu zilizotolewa hapa ni kutolewa kwa onyo, kuzuiwa kwa leseni, kibali au ruhusa, kufuta leseni yenyewe, kibali au ruhusa, kutoa fidia kwa washirika kwa waathirika kutokana na athari ya kosa lake. Hasa hii ya (e) nilikuwa nataka ufafanuzi wake ni namna gani ya fidia ambayo itakuwa inatolewa kwa hawa waathirika ambao watakuwa wanapata hayo mambo yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu katika kifungu cha 56, ukurasa wa 269 (i) hapa kuna maelekezo kwamba waziri anaweza kutunga kanuni. Kinaposema kwamba waziri anaweza ina maana ana hiyari kufanya au kutokufanya. Tukiliweka hili kwamba waziri tunapomwambia kwamba anaweza kutunga sheria, baadaye muda si mrefu tunategemea huu mswada utakuwa ni sheria, haitoweza kufanya kazi zake vilivyo au kufanya kazi zake vizuri, kama hii kanuni ambayo itakuwa inatoa ufafanuzi wa hizi sheria itakapokuwa haipo.

Tuna sheria nyingi sana katika nchi yetu, lakini nyingi ya sheria hizo zinashindwa utekelezaji wake kutokana na kwamba hakuna kanuni zinazoweza kutoa muungozo juu ya namna bora ya utekelezaji wa sheria hizo. Kwanza hili ningelipenda kwamba badala ya kwamba waziri anaweza, tutamke bayana kwamba waziri atatunga sheria, sio kwamba anaweza kutunga sheria. Tunapozungumza kwamba waziri anaweza inamaana ana hiyari, hata hatuwezi kumlaumu inaweza ikapita miaka miwili, mitatu, minne, hata lolote linawezekuwa kwa mujibu atakavyohisi mwenyewe linawezekana.

Lakini la ziada zaidi ya hayo, hizi kanuni ni nyingi sana ambazo zimetungwa hapa. Hivi kweli huu Mswada wa Sheria tunaotaka kuupitisha tunakusudia kweli uweze kufanya kazi kwa sasa. Baada ya maelekezo hayo sasa Mhe. Naibu Spika, jengine la kuongezea ambalo ninalo ningeiomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanapofanya hizi *translations* za Miswada hii wajitahidi kuangalia na kuowanisha namna ya yale maelekezo ambayo yamo kwenye Mswada wa Kiingereza na Mswada wa Kiswahili ili maana halisi inayokusudiwa iweze kutimia na iweze kulenga kama vile ambavyo inakusudiwa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni naunga mkono Mswada huu kwa asilimia kwa mia, lakini na maeneo hayo naomba yafanyiwe kazi ipasavyo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia machache kwa sababu wenzangu wengi ambao wameanza wamenifilisi baadhi ya maneno.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu na mimi nimshukuru sana na kumpongeza Waziri kwa kutuletea mswada huu ambao utaweza kuwasaidia sana wafanyabiashara wetu pia itaweza serikali kuingiza kipato wafanyabiashara hawa watakapokuwa wapo katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu katika madhumuni na sababu ya kuletwa Mswada huu. Madhumuni hapa yameonekana ni mazuri sana iwapo serikali itajitahidi kuwa makini katika utekelezaji au usimamizi mzuri wa sheria hii. Nasema hayo kwa sababu mara nyingi tunashindwa katika mambo yetu kwa kutokuwa na usimamizi mzuri wa sheria. Mhe. Spika, mimi niisisitize serikali kwamba ikisimamia vizuri basi tujue neema itaweza kupatikana kwa wafanyabiashara lakini pia serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 257 Kifungu 21(1) (J) Sheria hii inasema:

"Kutoa mafunzo ya utoaji wa leseni na yote yanayohusiana na vibali au ruhusa"

Mimi napongeza kwa kuliona suala hili katika huu Mswada kwa sababu saa nyengine tunakwama au tunafeli au tunalaumu lakini pengine kukosekana kwa hii elimu ya kuwapa hawa ambao tutawapa leseni.

Mhe. Naibu Spika, nikija tena katika kifungu cha (k) pia kuna neneo kuondosha urasimu. Neno hili mimi napongezwa kwa kuwekwa lakini nataka nimsisitize Mhe. Waziri kwamba neneo hili tuweze kulitumia vizuri kwa sababu linaweza likaondosha mianya ya rushwa, tukiliacha neno hili kulitumia maana yake urasimu ukipatikana basi watu wanaweza kweli ili mtu afanikiwe kupata analolotaka atatakiwa atoe kitu kidogo ili baadaye afanikie ile haja yake, hapo tunaweza tukasababisha rushwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nije tena katika ukurasa wa 263 katika kifungu cha 38(1) katika

Kifungu cha 38(2)

"Mamlaka ya leseni inaweza isizingatie maombi hayo endapo muombaji au muwakilishi wake watashindwa kuhudhuria katika mkutano huo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka hapa paongezwe kitu kidogo, kwa sababu tukiacha hivi hivi inawezekana muombaji akawa ameshindwa kuhudhuria katika mkutano lakini kukawa kuna sababu muhimi ambayo imemzuia. Basi hapa kungeombezwa nano katika Mkutano kwamba iwapo kama hakutoa dharura yoyote.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 265 katika kifungu cha 45 (1)(a) pia hapa mimi nilitaka Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kunifafanulia.

Kifungu cha 45(1) (a)

"Kwamba mwenye leseni hawezi tena na sio mtu sahihi wa kuwa na leseni, kibali, au ruhusa hiyo;"

Mimi hapa nilitaka kujua huyu mtu aliyekuwa si sahihi, yaani ana mapungufu gani ili akawa hayupo sahihi wa kuweza kupewa leseni. Nilikuwa naomba ufafanuzi Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie ili na mimi niweze kufahamu vizuri sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika ukurasa wa 269 katika Sehemu ya Saba, masharti mbali mbali. Hapa kifungu hichi cha 54 kinasema kwamba,

Kifungu cha 54

> *"Waziri anaweza kutoa kwa Baraza miongozo ya jumla au maalum kwa maandishi kuhusu utendaji au utekelezaji wa majukumu yake na Baraza litalazimika kuitekeleza miongozo hiyo".*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Waziri ni binaadamu kama walivyo binaadamu wengine, inawezekana na yeye akaja akafanya kosa kama hichi kifungu ndio tutakiacha tu hivi hivi bila ya kusema kwamba yale atakayoyatolea muongozo basi yawe yameambatana na sheria hii. Lakini tukiacha akaja akatoa ya moyoni mwake ambayo yatakuwa hayaendani na hii sheria basi anaweza kifungu hichi akaweza na yeye kukitumia vibaya kwa maslahi yake. Ningeomba tuzingatie sana juu ya hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema mchango wangu hautokuwa mkubwa lakini pia katika sheria hii labda kwa kuwa tumeipata muda si mrefu sana kwa vile hatukupata kuipitia vizuri, pia mimi sikuona adhabu itakayotolewa kwa mfanyabiashara atakaekwenda kinyume na yale ambayo yamezungumzwa humu. Kwa hiyo Mhe. Waziri naomba anipe ufafanuzi huo, lakini la kusisitiza pamoja na mfanyabiashara huyo ambaye atapatiwa leseni pamoja na kuchangia wafanyabiashara katika kuinua uchumi lakini pia naiomba serikali iweze kuzingatia isije ikawakandamiza wafanyabiashara wadogo wadogo kwa malipo makubwa nao wakaja akashindwa kumudu kutokana na udogo wa bishara zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni mdogo lakini kwa umuhimu wa sheria hii nilipaswa kusema hayo machache naiyunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 ili iweze kuwasaidia wafanyabiashara lakini pia kuweza kuingia mapato katika serikali. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Mswada huu, Mswada ambao umelenga kuanzisha chombo cha kusimamia utekelezaji ya mabadiliko ya mfumo wa leseni za biashara Zanzibar. Mimi Mhe. Naibu Spika, nitachangia katika maeneo matatu tu. Nitachangia katika ukurasa wa 255 katika kifungu 16 (1) naomba nikinukuu

Kifungu cha 16(1)

"Kutakuwa na katibu mtendaji wa Baraza ambaye atateuliwa na Rais"

Hapa Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naushauri tu nafasi hii ya Katibu Mtendaji tungemuachia Waziri ateuwe, tumpunguzie mzigo Mhe. Rais. Nitakwenda kwenye ukurasa wa 256 Kifingu 2(c) Mtu atafaa kuwa Katibu Mtendaji ikiwa hakutiwa hatiani na makosa yanayohusu maadili ya ufisadi au maadili ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba niulize je, yapo hayo maadili yanayohusu ufisadi au kuna makosa ya maadili ya rushwa. Kama yapo maelezo yake naomba niyaheshimu na kama hakuna naomba nitoe ushauri. Baada ya kuandika makosa ya maadili ya ufisadi au makosa ya maadili ya rushwa naomba tuandike makosa ya jinai.

Halafu kwenye ukurasa wa 260 kifungu cha 26 (2) ambacho kinasema

"Muombaji hatobaguliwa kwa misingi wa kabila, asili, rangi, utaifa, dini, imani ya kisiasa, familia au sababu zozote zinazofanana na hizo".

Hapa nilikuwa nashauri kipengele kimoja ambacho kinawahusu walemavu. Nikuliwa nashauri isomeke hivi: Muombaji hatobaguliwa kwa misingi ya kabila, asili, rangi, utaifa, dini, imani ya kisiasa, ulemavu, familia au sababu zozote zinazofanana na hizo. Nilikuwa nashauri kipengele cha ulemavu kijitokeze katika sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo sina mengi naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi jioni hii ya leo kupata fursa na nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada unaoelekeza kusimamia mageuzi ya mfumo wa utoaji wa leseni.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda nianze Sehemu ya Pili kifungu cha 5, kazi za Baraza. Mhe. Naibu Spika, kazi za Baraza zimeorodheshwa kuanzia (a) - (n) ambazo kazi zake kubwa ni kutayarisha Sera za kuendesha mfumo wa utoaji wa leseni kitaifa. Tatizo langu ni kwamba Baraza hili ambalo linatayarisha sera, miongozo na taratibu za utoaji wa leseni miongozo kama haitofuatwa na vyombo au mamlaka hizo za utoaji wa leseni. *Mathalan* mwananchi ameathirika, hili Baraza linamsaidia vipi.

Mimi fikira zangu kwamba Baraza hili lingepewa uwazo wa kuwa ni chombo cha rufaa kwa muongozo na taratibu za Baraza ili mwananchi aweze kupeleka malalamiko yake kwa Baraza hili. Kwa hivyo ningeomba kiongezwe kifungu cha kulipa uwezo Baraza kuwa ni chombo cha rufaa kutokana na malalamiko yatakayotolewa kwa Mamlaka za kutoa leseni. Kwa maana hiyo itabidi kifungu cha 6(2) kifutwe kwa vile hizo ndio kazi za Baraza litatakiwa zifanywe ili kuwasaidia wananchi watakaopatwa na matatizo au ikiwa hawakuridhika na maamuzi ya mamlaka za utoaji wa leseni.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kifungu cha 12(3)(4)(5), vifungu hivi vidogo vifutwe kwa kuwa hakuna haja ya mjumbe wa Baraza aliyemaliza muda wake kuendelea kulitumikia Baraza kwa kipindi cha miezi sita zaidi. Kwa maoni yangu kwamba kifungu cha 9 cha Mswada huu kinajitosheleza kwa kuwa muda wa mjumbe wa Baraza uwa wa miaka mitatu na anaweza kuongezewa, kwa hivyo hakuna haja ya kuwepo vijifungu hivi vidogo cha (3), (4), na (5).

Kifungu cha 54 kinazungumzia uwezo wa waziri, Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kwamba maneno yafuatayo yaongezwe baada ya neno "maandishi" lililokuwepo mstari wa pili kutoka juu katika kifungu hichi na maneno yenyewe ni haitopingana na uwezo wa kazi za Baraza kwa mujibu wa sheria hii. Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Basi Wajumbe kama tumetosheka na michangio na Wizara hii Waziri anakaimu kwa hivyo nimpe muda wa kwenda kujitayarisha zaidi ili kesho baada ya Maswali na Majibu afanye majumuisho na kupitisha vifungu. Kwa hivyo kwa kuwa muda haujafika namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu ili aweke utaratibu ili kuakhirisha hadi kesho.

KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli iliyopangwa leo ya hoja ya Mswada haijakamilika lakini michango ya Waheshimiwa Wajumbe imekamilika na kwa ajili ya kumpa muda Mhe. Kaimu Waziri kufanya majumuisho ya michango ya Wajumbe. Kwa hivyo naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ya muda ili tuweze kuakhirisha Baraza hili kabla ya wakati wake. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Nawashukuru Wajumbe kwa ushirikiano wenu na baada ya hayo naakhirisha Kikao chetu hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 11/10/2013, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:22 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi kesho
tarehe 11/10/2013 saa 3:00 za asubuhi)